# Huru Kuwa Wewe

Na Larry Chkoreff

Version 2.1 Mei 2009
ISBN-978-0-9823060-1-7

Tole la Kiswahili © 2010

Kimetafsiriwa na kuchapishwa na:
Cistern Materials Translation & Publishing Center, Nairobi, Kenya
Barua pepe: info@cisternmaterialscenter.com
www.cisternmaterialscenter.com

*Huru Kuwa Wewe* kimechapishwa na International School of the Bible-ISOB, Marietta, GA USA
info@isob-bible.org
www.isob-bible.org

Haki ya kumiliki © 2008 na Larry Chkoreff - Mwandishi

Wahariri wa kuchangia - Micheal na Karen Vincent

Kitabu hiki ni mali ya mwandishi. Kinaweza kuchapishwa tena, iwapo tu kitachapishwa chote, kwa ajili ya kukisambaza bure (bila malipo). Hairuhusiwi kukibadili au kukiharirir kwa njia yoyote ile. Kikichapishwa tena ni lazima kiwe na tangazo la miliki.

Vifungu vyote vya Biblia vimetolewa kutoka The Holy Bible in Kiswahili Bi UV052 BST/BSK © 2003 published by Bible Society of Kenya and Tanzania.

## YALIYOMO

UTANGULIZI .................................................................... 6

SURA YA 1 - MAONO YA KUPONYWA ............................ 18

SURA YA 2 - KWA NINI MUNGU HUKUWEKA HURU .... 31

SURA YA 3 - NGUVU ZA MAONO .................................. 39

FAHIRISI A - UJUZI WA URAFIKI ...................................... 42

SURA YA 4 - MAJERAHA KUTOKA KWA WENGINE… 46

SURA YA 5 - MAJERAHA KUTOKANA NA LAANA............. 64

SURA YA 6 - MAJERAHA KUTOKANA NA DHAMBI ZETU 81

SURA YA 7 - HUKUMU NA NADHIRI ............................... 97

SURA YA 8 - MAMBO YANAYOFUNGA ROHO .............. 108

SURA YA 9 - KUSONONEKA .......................................... 118

SURA YA 10 - MSAMAHA .............................................. 129

SURA YA 11 – KIGAGA NA KOVU .................................. 142

SURA YA 12 – AIBU - HATIA ............................................. 149

SURA YA 13 - VITA VYA AKILI ZAKO ..................... 165

SURA YA 14 - KUISHI JINSI ULIVYO ............................. 176

SURA YA 15 - VITA VYA KIROHO ...................................... 188

SURA YA 16 - JIWE LAKO LIMEVINGIRISHWA ........ 197

MANENO YA MWISHO ................................................. 205

# UTANGULIZI

*Yoeli 2:25,26 inasema ya kwamba, "Nami nitawarudishia hiyo miaka iliyoliwa na nzige, na parare, na madumadu, na tunutu, jeshi langu kubwa nililolituma kati yenu. Nanyi mtakula chakula tele na kushiba, na kulihimidi jina la BWANA, Mungu wenu, aliyewatendea mambo ya ajabu; na watu wangu hawatatahayari kamwe."*

Unaweza kutambua ya kwamba, miaka yako ya nyuma imepotea na kuliwa na dhambi zako na za watu wengine. Tena, kama vile madumadu hubadilika na kuwa kipepeo kupitia metamofosisi, Mungu hutoa metamofosisi ya rohoni, mabadiliko (metamorphoo kwa Kigriki), ambayo yanaweza kutokea.

Kupitia kwa nabii Yoeli, Mungu anasema ya kwamba, atarudisha mambo ambayo yalikuwa yameharibiwa na kupotea. Bwana hajatuahidi maisha bora yatakaokuja tu, bali ameahidi kutumia uharibifu uliopita ili kubadilisha hasara yako kuwa faida.

Kipepeo hakikumbuki kuna wakati kilikuwa madumadu. Vile vile wewe hutaomboleza kwa sababu ya miaka yako iliyoharibiwa na iliopotea. Bwana atafanya maisha yako yatakao kuja kuwa mema kwa njia ya ajabu. Madumadu huanza kama mdudu mharibifu, lakini baadaye hubadilika na kuwa kipepeo, mdudu wa maana na aliye na faida.

Mungu alimnenea mwandishi wa kitabu hiki, ambaye ni mume wangu Larry, kifungu hiki, mda mfupi baada ya kumpokea Yesumnamo mwaka wa 1979. Larry alikuwa akiomboleza kwa sababu ya miaka aliyopoteza. Hivi sasa, karibu miaka 30 baadaye, anaweza kushuhudia ukweli na utimilivu wa ahadi hii.

Kitabu hiki kinapeana maelezo mwafaka pamoja na ukweli ulio na nguvu za kuponya majeraha vyako vya ndani na pia vile ambavyo havionekani vilivyo sababishwa na dhambi zako na hata za watu wengine. Uponyaji wa Mungu utakufanya uwe huru, mtu anayeweza 'kupaa juu,' na pia aliye na faida kama vile imeashiriwa na kipepeo ambacho kimepigwa picha katika jalada la kitabu hiki.

Carol Chkoreff
Januari 2009

## MAONI

Kichwa cha kitabu hiki "HURU KUWA WEWE" kinafaa kwa sababu *mtu wa ndani* wako amejeruhiwa na kubanana na hatia. Sasa unaweza kubomoa ya kale na ujenge upya kwa sababu ya maisha yako yatakaokuja. Waisraeli waliotoka Misri walihama kutoka Misri, lakini Misri haikutoka ndani yao. Shida kubwa imekuwa jinsi yakutoa Misri iliokua ndani yao. Kitabu hiki kina kipande cha uponyaji wa ndani. Chukua na ukisome kwa sababu ya msaada wako mwenyewe na wa wengine ambao bado wanaserereka kwa maumivu. Chagua uhuru na uponyaji wa Mungu.

John Brown Okwii, PhD
Raisi,
The Apostolic church LAWNA, Theological Seminary Jos,
PL930001, Nigeria.

## SIFA

Tumewataja Michael na Karen Vincent kama *Wahariri Waliochangia* baada ya kukosa ufasiri bora kwa wajibu wao katika kitabu hiki.

Bila shaka, Karen Vincent alifanya kazi muhimu sana ya uhariri wa msingi. Hata hivyo, kwa miaka sita ambayo imepita (tangu 2003), Michael na Karen wamenifunza mengi kuhusu oponyaji wa ndani kutokana na yale ambao wamepitia katika maisha yao na pia kunipa mazoezi. Kwa hivyo ni na hisi wao ni zaidi ya Wahariri Waliochangia. Tumefanya kazi na kuhudumu pamoja mara nyingi na tumerekodi mfululizo wa video 18 zinazojulikana kama *ISOB Bondage Breakers.*

Pia, walipokuwa wakihariri kitabu hiki, niliwapa Michael na Karen uhuru wa kuongeza shuhuda zao wenyewe na mazoefu yao. Waliongeza mashauri mengi katika sehemu nyingi za kitabu hiki.

Utukufu wote umuendee Yesu, lakini pia shukrani nyingi kwa Michael na Karen.

Neno la shukrani kubwa kwa Tracey Diaz kwa sababu ya kutengeneza picha maridadi ya jarida.

Larry Chkoreff

# Huru Kuwa Wewe
# Utambulisho

Je, umewahi kujipata katika hali ya kuwa mfungwa lakini hauoni mlango wa gereza? Umewahi kujipata ukiwa na uzito mwingi wa moyo? Umewahi kukabiliana na mafadhaiko? Je, wewe unaishi katika hali ya hasira ama woga, na hujui vile unaweza kuwa huru? Je, wewe hujipata kila mara ukifanya mambo ya kukuaibisha na hupati nguvu za kubadilika? Je, una mazoea ya kuwaambia rafiki zako 'mambo yote ni shwali' hali ukijua husemi ukweli? Je, wewe ni mtawaliwa wa madawa ya kulevya, pombe, ponografia, ulafi, au unatawaliwa na jambo lingine lolote? Je, umechoka na "vipindi" ambavyo huahidi mambo mengi lakini hayatimii?

Wahariri wangu wawili waliochangia kuandika kitabu hiki pamoja nami tumejipata katika hali hii lakini tumewekwa huru! Tutakupeleka katika njia ambazo tumepitia. Tunaomba ya kwamba njia yako itagongana na njia ya Mungu na kupitia kanuni za Biblia ambazo sisi tulitumia, wewe pia utakuwa mtu huru.

**Kuna tumaini**

Yesu, Muumba wa vitu vyote, alikuja hapa duniani kama mwanadamu ili akupatie nguvu za kubadilika na uwe huru. Ujumbe maalum wa Yesuulitabiriwa katika Isaya 61 miaka mingi kabla ya kuzaliwa kwake. Alipokuwa tayari kuanza huduma yake hapa ulimwenguni, Yesualidondoa maneno haya kutoka kitabu cha Isaya.

"Roho wa Bwana MUNGU i juu yangu; kwa sababu BWANA amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao. Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa na siku ya kisasi cha Mungu wetu; kuwafariji wote waliao. Kuwaagizia hao waliao katika Sayuni wapewe taji ya maua badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito; wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na BWANA, ili atukuzwe. Nao watajenga mahali pa kale palipoharibiwa, watapainua mahali palipokuwa ukiwa zamani,

watatengeneza miji iliyoharibiwa, mahali palipoachwa kizazi baada ya kizazi" Isaya 61:1-4.

"Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo, akatafuta mahali palipoandikwa, 'Roho wa Bwana yu juu yangu; kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema; amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa, na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.' Akakifunga chuo, akamrudishia mtumishi, akaketi; na watu wote waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho. Akaanza kuwaambia, 'Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu'" (Luka 4:17-21).

***Tazama Alitaja msaada kwa:***

Maskini
Waliovunjika moyo
Wateka
Wafungwa

Mwaka wa Bwana uliokubaliwa ni mwaka wa yubile kama vile imeandikwa katika Mambo ya Walawi sura ya 25. Ulikuwa mwaka ambao madeni yote yaliondolewa na walio na deni na wasiojiweza wakawekwa huru.

Aliahidi vipofu kupata kuona tena. Hii ni pamoja na walio vipofu kiroho.

Alisema atawafariji wote waliao. Kilio ni uchungu wenye mhemuko wa huzuni inayotokana na kupoteza kitu au jambo. Wengi wetu hulia katika moyo kwa sababu tumepoteza, au hatujakuwa "sisi wenyewe". Pia tunaweza kulia kwa sababu ya kupoteza ndoto na matumaini, au labda tumepoteza wapendwa wetu.

***Yesuiliahidi haya, na alikuwa na uwezo wa kutimiza ahadi zake***.

Kwa hivyo shida iko wapi? Pengine wewe ni MKristo ambaye unasumbuliwa na shida inayotawala maisha yako au unajihisi kana kwamba umefungwa. Labda umemfanya Yesukuwa mwokozi wako lakini bado hajakuwa BWANA katika maisha yako. Kuna tofauti kubwa tati ya Yesukuwa mwokozi wako na Yesukuwa BWANA wako.

Kuwa na mwokozi kunahusu “mimi’ na ni maisha ya ubinafsi. Sisi ambao tunapambana na dhambi, ambao ni sisi zote, ni lazima tumfanye Yesukuwa Bwana katika maisha yetu. Tunapotoa maisha yetu kabisa na kumpa Yesunafasi ya kutawala maisha yetu, hata kama tutakosea mara kwa mara, hatutakuwa wafungwa wa dhambi tena. Tuna nafasi ya kuamka na kuendelea mbele na safari yetu.

Labda umekuwa mfuasi wa Yesuna MKristo kwa miaka mingi, lakini bado umefungwa, wewe ni mfungwa. Basi, kitabu hiki kinakufaa. Tunatarajia kukuonyesha jinsi ya kunyakua ahadi za uridhi ambao Yesualikufa ili uweze kuupokea.

Unaweza kubadilika sasa hivi. Mwambie Yesuya kwamba unaamini alisulubiwa na akafufuka katika wafu kama malipo ya uhuru wako. Tena mwambie umemfanya kuwa Bwana na kiongozi maishani mwako. Mhuruhusu atawale maisha yako yote. Hatimaye kuwa tayari kuchukua msalaba wako, ‘ufe,” na umfuate. Matokeo hayatakuwa utumwa wa kidini, lakini utamuona Yesuna utapata utukufu na upendo wake. Mwishowe, atakuwa vyote katika vyote kwako. Kumtafuta kwako kutabadilika kutoka hali ya kutafuta ukombozi wake na faida zinginezo, hadi kumtafuta yeye pekee kwa ajili ya vile alivyo. Atakuwa vyote katika vyote katika maisha yako yote. Utatambua ya kwamba utatamani sana kuwa karibu naye, na uwe na shauku kubwa la kumtafuta.

### *Hesabu Gharama*

“Maana ni nani katika ninyi, kama akitaka kujenga mnara, asiyeketi kwanza na kuhesabu gharama, kwamba anavyo vya kuumalizia? Asije akashindwa Kuumaliza baada ya kuupiga msingi, watu wote waonao wakaaza kumdhihaki, wakisema, Mtu huyu alianza kujenga, akawa hana nguvu za kumaliza. Au kuna mfalme gani, akitaka kwenda kupigana na mfalme mwingine, asiyeketi kwanza na kufanya shauri, kwamba yeye pamoja na watu elfu kumi ataweza kukutana na yule anayekuja juu yake na watu elfu ishirini? Na kama akiona hawezi, hutuma ujumbe kutaka sharti za amani, mtu yule akali mbali. Basi, kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu” (Luka 14:28-33).

Kuna gharama unaporuhusu Roho Mtakatifu afunue majeraha vya kale na mambo mengine ambayo yanaweza kuwa na uchungu mwingi. Ni lazima tupite uwongo unaozuia ukweli uletao toba, msamaha, na uhuru. Ni lazima tuhesabu gharama ya kuwachilia kujitawala na turuhusu Roho Mtakatifu apate nafasi ya kutawala maisha yetu yote. Ni watu wachache sana ambao wanatamani kuhesabu gharama hii, je, wewe mmoja wao?

**Shida iko katika majeraha vya ndani ambavyo havionekani.**

Mara kwa mara, wanadamu wanaweza kuathiriwa na majeraha visivyoonekana, katika nafsi zao. Watu wengi, na hata WaKristo wengi, hawafahamu hivyo, na hawajui ya kwamba Yesualikuja kuponya majeraha hizi na kufanya nafsi zao kuwa na afya. Badala ya kumuendea Yule aponyaye, watu walio na majeraha katika nafsi zao hujaribu "kutibu" majeraha vyao kwa aina zote za "matibabu" yasiofaa. Baadhi ya matibabu haya ni madawa ya kulevya, pombe, mazoea mabaya ya ngono, hisia za udini, au shughuli nyingi. Wengine hujipeana kabisa kwa kazi zao au hujishughulisha na mambo ya ulimwengu kama njia ya kutibu majeraha vyao. Pia wengine pia hujaribu kuzima na kuzika majeraha kupitia hali ya kutokubali, na wanaishi maisha yanaoonekana kuwa ni mazuri na ya kawaida. Lakini ndani yao, wanajihisi kufinyika na wakiwa na uzito. Wanajua kwa hakika, kuna jambo mbaya kabisa, na wanapatwa na mfadhaiko, hasira, na wanaishi maisha yasiyo na matumaini.

Baadhi ya watu wanaishi katika ulimwengu wa ndoto za kubuni, ambapo wao ni washindi kila wakati kwa sababu ukweli unaumiza sana. Kwa hivyo wanaishi katika ndoto ambazo huwafanya watumwa wa kutofanya jambo lolote lenye manufaa. Ninaweza kushuhudia ya kwamba maisha yangu yalikuwa hivyo kabla ya kuokolewa na Yesumnamo mwaka wa 1979. Kuwa na ndoto za kubuni ni hatari sana kwa mwanadamu. Ni majaribu halisi kwa watu wengi kama njia ya kuepuka.

Mambo haya yote hutuzuia kupata lengo halisi la maisha yetu.

Tumetengeneza kanda nyingi za video[1] kwa kusudi la kuwasaidia wachungaji na viongozi kuunda vikundi vidogo na kuvielekeza katika uponyaji wa ndani kama vile mwenyezi Mungu alivyokusudia. Lakini sio wote wanaohitaji uponyaji wa ndani watapata kanda hizi. Kwa hivyo, tumeandika kitabu hiki kwa madhumuni ya kuwapa watu binafsi na pia vikundi vidogo nafasi ya kuwa huru kutokana na majeraha vya kale na waweze kuwa na mazoefu ya uzima tele kama vile Yesualielezea.

**Je, majeraha hutoka wapi?**

Kuna chanzo tatu za majeraha ya ndani ambayo hukufunga na kukukandamiza:

(i) Majeraha yanayosababishwa na wengine. Katika kitabu hiki tutayaita "Dhambi dhidi yako"

(ii) Majeraha ya kujiletea. Majeraha haya yanatokana na hali yetu ya maisha ya dhambi

(iii) Laana za ukoo. Majeraha haya husababishwa na dhambi za mababu zetu.

Ni vyema kuelewa ya kwamba chanzo cha majeraha yote matatu ni aina fulani ya dhambi. Watu wengi hawapendi kutumia neno "dhambi." Wao huchukulia dhambi kama aina fulani ya ugojwa wa kidini na hudhani ni laana.

Lakini jambo la muhimu hapa ni dhambi. na kazi ya kuondoa dhambi ni ya Yesu. Tunaweza kulinganisha kuondolewakwa dhambi na kuondolewa kwa ugojwa wa kansa kupitia upasuaji. Kuondoa dhambi pia kunajulikana kama toba na msamaha.

**Shikilia imara, Yesu alishinda dhambi.**

Msamaha humeonyesha hali ya kumrudia Mungu na kuwa na ushirika wa kibinafsi na wa karibu naye. Kwa hivyo, msamaha ni

[1] Kwa maelezo kuhusu video, angalia www.isob-bible.org

mlango wa kufanyika mkamilifu na kurithi vyote ambavyo vina Mungu kwa ajili yetu.

Matendo 26:18 hutufunulia thamani ya msamaha inaposema, “.....uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuelekea nuru, waziache na nguvu za shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi.”

***Kazi ya Yesuya kuwaweka watu huru ni ya kuwafungua kutoka kwenye na dhambi; huu ni msamaha.***

“Yesu akawajibu, amin amin, na waambia, kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi” (Yohana 8:34).

“Naye atazaa mwana, nawe utamwiita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao” (Mathayo 1:21).

“… tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia. Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake” (Ufunuo wa Yohana 1:5).

Unaweza kufikiri unajua mambo yote kuhusu msamaha au hupendi kuwaza juu yake. Kitabu hiki kitakuonyesha njia mpya, tofauti, na ya kukufariji utakaporuhusu Yesu akusaidie kusamehe ili aondoe mzizi wa kansa ya dhambi. Kwa wakati huu, fungua mawazo yako ili uweze kuelewa msamaha kwa njia nyingine.

Katika kitabu hiki tutaangazia majaliwa ya Mungu na nguvu zake katika kuponya majeraha yote matatu yaliotajwa hapo awali.

Katika kitabu, tutazingatia mambo haya ya msingi kuhusu uponyanji:

*Kazi ya Yesu Msalabani*
*Mamlaka thabiti ya Yesu*
*Msamaha*
*Kubadilisha mawazo yako kuhusu maisha*
*Uhusiano wa kusikia kutoka kwa Mungu*
*Ubatizo wa Roho Mtakatifu*

## Kazi ya Yesu Msalabani

"Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kipigwa kwake sisi tumepona" (Isaya 53:5).

Yeye alichukua na kustahimili majeraha yaliokuwa yetu ili sisi tuwe huru.

"Kujeruhiwa" hakumaanishi kuchubuliwa tu, lakini pia kunamaanisha kuambiwa maneno machafu, kuchafuliwa na hata neno malaya limetumiwa katika ufasiri. Lina maanisha kunajisiwa, kuchafuliwa, na kuwekwa mawaa, kuwa kinyume na utakatifu.

Kuchubuliwa kunamaanisha kugandamizwa, kuvunjwa, kufanywa uwe na majuto, kuruhusu mtu apigwe kabisa, kuteswa.

***Haya ndiyo unaweza kutarajia.***
***Yote yako katika uhusiano!***

Sema nami, "Yyote yako katika uhusiano." Rudia mara tatu kwa sababu singependa usahau hivyo. Haya yote yanahusu uhusiano wako na Yesu. Hii nakala si chombo cha kukufanya wewe mwenyewe ya uponyo wa kisaikologia. Uponyaji halisi si hoja yako mwenyewe.

Yesu alisema katika Yohana 15, tunastahili kukaa ndani yake. Maandiko mengine katika Agano Jipya yanasema, Yesu anakaa ndani yetu. Mungu anatamani wewe nay eye muwe na umoja, na unaendelea kukuwa unapotililia maanani uhusiano wako na yeye. Uponyaji wa ndani sio tiba ambayo tunauliza Mungu atufanyie. Uponyo wa ndani huja kwa hali ya kawaida tunapoendelea kukaa ndani ya Yesu, naye ndani yetu.

***Watu wengi hawathamini uhusiano vilivyoo.***

Wanawake ni bora zaidi kuliko wanaume. Mara nyingi watu kutoka bara la Asia, Afrika na mataifa yenye desturu za Mashariki ni bora katika mahusiano kuliko watu walio na mawazo ya desturi za Magharibi. Lakini hata katika desturi hii inayozingatia mahusiano, mara nyingi wanaume huwachukulia wake wao kama mali tu. Dhambi zimeharibu ustadi na maana ya mahusiano katika kila utamaduni. Uhusiano wa kibinafsi na Mungu ni muhimu kwa sababu, tutakapo

kua katika uhusiano wetu na yeye, atatuweka huru, na pia tutakuwa na uhusiano mwema na wengine.

***Yesu alisema yote yako katika uhusiano***.

Katika Yohana 15, kabla ya kusulubiwa kwake, Yesu aliwaambia wanafunzi wake jambo muhimu la kuweka maanani. Aliwaambia ya kwamba, la muhimu zaidi katika maisha ni kumtukuza Baba Yake, Mungu. Aliwaambia wataweza kufanya hivyo kupitia kuzaa matunda. Tena watazaa matunda ikiwa wamekaa ndani yake kama vile tawi hukaa katika mzabibu. Hii ilimaanisha uhusiano wa karibu na wa ndani.

“Mimi ni mzabibu wa kweli, na Baba yangu ndiye mkulima. Yeye huliondoa ndani yangu kila tawi lisilozaa matunda, na kila tawi lizaalo hulisafisha lipate kuzaa zaidi. Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya ule ujumbe niliowaambieni. Kaeni ndani yangu, nami nikae ndani yenu. Tawi haliwezi peke yake kuzaa matunda lisipokaa katika mzabibu hali kadhalika nanyi hamwezi kuzaa matunda msipokaa ndani yangu. "Mimi ni mzabibu, nanyi ni matawi yake. Akaaye ndani yangu, nami ndani yake, huyo atazaa matunda mengi, maana bila mimi hamwezi kufanya chochote. Mtu yeyote asipokaa ndani yangu hutupwa nje kama tawi litupwalo nje hata likakauka. Watu huliokota tawi la namna hiyo na kulitupa motoni liungue. Mkikaa ndani yangu na maneno yangu yakikaa ndani yenu, basi, ombeni chochote mtakacho nanyi mtapewa. Baba yangu hutukuzwa kama mkizaa matunda mengi na kuwa wanafunzi wangu” (Yohana 13:1-8).

Tangu 1998 tumewaona watu kote ulimwenguni wakiwekwa huru kutoka utumwa na majeraha, na kuwa wanafunzi wazao kwa ajili ya Yesu kupitia vitabu vyetu vya ufuasi. Vitabu hizi zinahimiza uzaaji wa matunda kupitia uhusiano wa karibu kwa kutumia ustadi wa mahusiano na Mungu ya kila siku.

Inasikika ikiwa rahisi sana, sio ya udini, na imekataliwa na watu wengi kwa sababu ya ukweli wake. Hata hivyo, huu ukweli ni kutoka kwa Mungu wala sio kutoka kwa vitabu vyetu au kwetu wenyewe.

"Lakini naogopa kwamba, kama vile yule nyoka kwa hila zake za uongo alimdanganya Hawa, fikira zenu zaweza kupotoshwa, mkauacha uaminifu wenu wa kweli kwa Kristo" (2 Wakorintho 11:3).

**Tutazingatia mafundisho haya muhimu ya nidhamu katika kitabu hiki.**

1. Ustadi wa uhusiano na Mungu kila siku
2. Kuwa mtiifu kwa Mungu unapotembea pamoja naye.

Katika kitabu hiki tunakusudia kukufunza mambo ya kukusaidia kusikia sauti ya Mungu na kutembea kwa utiifu

Kutoka 15:26 inasema, "Akawambia, Kwamba utasikiza kwa bidii sauti ya BWANA, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele zake, na kutega masikio usikie maagizo yake, na kuzishika amri zake, mimi sitatia juu yako maradhi yo yote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa Mimi ndimi BWANA nikuponyaye."

**Upande wa manufaa wa Uponyanji wa Ndani**

3 Yohana 1:2 Inasema, "Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo." Fahamu, kufanikiwa nje kunauhusiano na kufanikiwa kwa roho.

Kuwa mtu huru ndani kutafaidisha hata maisha yako ya kawaida. Wakati huu, 2008-2009, mambo mengi ulimwenguni yanaanguka na kusababisha hofu nyingi. Hata Marekani ambayo kwa kawaida inajulikana kwa kutoa nafasi nyingi za msaada wa kufanikisha kiuchumi ina tikisika. Mashirika makubwa ya kifedha yanaanguka, Mamilioni ya jamii wanateseka kutokana na ukosefu wa misaada ya kifedha. Ulimwengu wote umekuwa katika shida za ukosefu wa fedha, na inaendelea kuwa mbaya zaidi. Vita kubwa vinaendelea katika mataifa kadhaa. Kuna uhaba wa chakula kote ulimwenguni, na mitetemeko mikubwa ya adhi imeathiri mamilioni ya watu. Hukumu isiowahi kutokea inaendelea hapa duniani.

Tumeahidiwa, "BWANA atakuwa ngome kwake aliyeonewa. Naam, ngome kwa nyakati za shida. Nao wakujuao jina lako wakutumaini Wewe, maana Wewe, BWANA hukuwaacha wakufuatao" (Zaburi 9:9-10).

“Bali utafuteni kwanza ufalme Wake, na haki Yake; na hayo yote mtazidishiwa” (Matayo 6:33)

Unapomtafuta Yesu akuponye ndani, mambo mengine ya kawaida katika maisha yako yatashughulikiwa. Uhusiano wako na mkeo au mmeo na watoto utastawi. Yesu atayashughulikia mahitaji yako ya kifedha na pia atafanya miujiza ya mambo ya kifedha. Mimi pamoja na wahariri walionisaidia kuandika kitabu hiki ni washuhuda wa mambo haya.

**Yesu hakuja kufanya watu kuwa Wakristo; alikuja kuwafanya wanafunzi.**

Mwanafunzi ni mtu ambaye amejitoa kabisa ili afunzwe na atii mtu mwingine.

Kwa wakati huu ningependa kukuondolea mawazo unayoweza kuwa nayo unapowaza juu ya nidhamu. Unaweza kuuliza “Je waandishi hawa wataniambia ninapaswa nijiombee kuhusu nidhamu yangu binafsi ili nikomeshe tabia fulani ama jinsi ya maisha isio ya kiungu?” Ndio na la.

Hauwezi kujiwekea nidhamu ili ukomeshe hasira, au utibu majeraha yako kwa madawa, au shida yeyote. Kama ungeweza kufanya hivyo, basi haikuwa na maana kwa Yesu kujitoa dhabibu msalabani kwa ajili yako. Hauwezi kujiwekea nidhamu kwa sababu ya maisha yako ya dhambi. Hauwezi pia kuadhibu matokeo ya dhambi za watu wengine dhidi yako. Hauwezi kuponya dhihirisho la laana za kizazi kwa kujiwekea nidhamu.

***Biblia ni wazi kwamba nidhamu ya aina hii hufanya shida kuwa mbaya zaidi.***

“Basi, ikiwa mlikufa pamoja na Kristo mkayaacha yale mafundisho ya awali ya ulimwengu, kwa nini kujitia chini ya amri, kama wenye kuishi duniani. Msishike, msionje, msiguse, (mambo hayo yote huharibika wakati wa kutumiwa); hali mkifuata maagizo na mafundisho ya wanadamu, mambo hayo yanaonekana kana kwamba yana hekima, katika kunyenyekea, na katika kuutawala mwili kwa

ukali; lakini hayafai kitu kwa kuzizuia tamaa za mwili" (Wakolosai 2:20-23).

***Jibu ni kwamba, ni lazima ujiwekee nidhamu kufanikisha uhusiano wako na Yesu na ukumbali aweke utaratibu mpya katika mawazo yako.***

"Basi, ikiwa mmefufuka pamoja na Kristo, yatafuteni mambo ya juu, kule Kristo aliko, ameketi upande wa kulia wa Mungu. Muwe na hamu ya mambo ya huko juu, na siyo mambo ya hapa duniani. Maana ninyi mmekufa na uzima wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Uzima wenu halisi ni Kristo, na wakati atakapotokea ndipo nanyi pia mtakapotokea pamoja naye katika utukufu" (Wakolosai 3:1-4).

Kuishi maisha ya nidhamu na kuweka uwelekevu katika uhusiano wako na Mungu kunaweza sikika kama ni jambo rahisi sana. Nina amini, sio rahisi isipokuwa pengine uwe umekata tama jinsi nilivyokuwa wakati mmoja. Wahariri wasaidizi wangu Michael na Karen Vincent ambao pia walikuwa wamekata tamaa wanashudia ya kwamba, walijua suluhisho lakini haikuwa rahisi kulipata. Walikuwa na vita dhidi ya 'miili' yao na mapepo yalijaribu kuingilia kati ustadi wao wa uhusiano ambao walijua utawakomboa. Lakini mwishowe walishinda.

Ninajua maisha yangu yalikuwa yameangamia na hakuna lolote nilijaribu lilifanikiwa. Nilikuwa nimevunjika moyo hivi kwamba singengoja kukutana na Yesu kila asubuhi. Alinipa uhai, na kweli nilihisi uhuru na upendo wakukutana Naye. Wakati wa mchana nilihisi kudhulumiwa hadi nilipopata nafasi Naye tena, kisha yote yakawa sawasawa. Huo ulikuwa mwaka wa 1979 na leo, miaka ishirini na tisa baadaye, siwezi kungojea kukutana Naye. Nimepokea uponyaji kutokana na mambo mengi yalionidhulumu. Kwa hivyo mchana wangu huwa ni wa raha wakati mwingi. Hakuna lolote maishani linalotosheleza kama kuwa na Mungu maishani mwako.

Ni vigumu kuelezea matukio niliyopitia. Ni kama kujaribu kukuelimisha ya kwamba maji yana $H_2O$. Utakubali ukweli huu, lakini isipokuwa uyanywe maji, $H_2O$ haitakuwa na maana kwako.

**Fanya uamuzi wako sasa!**

Ikiwa umevunjika moyo kwa miaka mingi na sasa unahisi umekosa tumaini kuwa wewe au Mungu anaweza kufanya lolote juu ya hali yako, basi sikia maneno haya. Usikisome kitabu hiki ukiwa na uzito wa moyo na unataka kutumia nguvu zako mwenyewe mara nyingine na uanguke tena. Swali langu ni hili, Je, utajitoa katika kuujenga uhusiano wako na Mungu na umngoje afanye muujiza katika maisha yako?

Ikiwa hauko tayari kuchukua muda unaohitajika kila siku, hata lisaa limoja kufanya uhusiano wako na Yesu kuwa dhabiti, basi, tunakushauri ukome kusoma kitabu hiki pahali hapa na umpe mtu mwingine.

**Dondoo kutoka kwa Watchman Nee kutoka kwa "The Joyful Heart May 15th"**

*"Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni, roho I radhi, lakini mwili ni dhaifu."Mathayo 26:41*

*Wanafunzi wako Gethsemane. Kwa namna fulani, hili lilikua tukio la kabla ya Pentekoste. Inatukumbusha ya kuwa Mkristo hawezi kuishi kwa utashi wake mwenyewe. Utashi unaweza kumfanya mtu awe tayari tu, na hapo ndio mwisho. Kuwa tayari hakuwezi kuongeza nguvu mwili wako dhaifu. Kitu ambacho ni zaidi ya kuwa tayari kinahitajika. Utashi ni kama gari lisilo na mafuta. Ni lazima lisukumwe au livutwe kwa kamba. Likiachiliwa linasimama. Kutumainia uwezo wa kibinadamu kutimiza mambo ya kiroho kunasababisha kushindwa. Nguvu za kiroho hazitokani na uwezo wa kibinadamu, lakini hutoka kwa maisha mapya ndani ya Kristo. Maisha haya huandaa nguvu nyingine ya ndani zaidi ya uwezo wetu na kupitia nguvu hii tunajipata tumebebwa na utukufu wa ushindi Bwana.*

# Sura 1
# Maono ya Kuponywa Ndani

Kama utangulizi wa ziada wa kitabu hiki, ningependa kuanza kwa kufichua sura ya tabia na ubinafsi wa Mungu

Katika Mathayo 12:1-21, Yesu anadhihirisha tabia moja muhimu ya Mungu. Anaonyesha kuwa Mungu anahaja sana na watu wanaoumia kuliko jinsi alivyo katika sheria na amri.

**Mafarisayo walimpa Yesu wakati mgumu kuhusu kufanya mambo fulani siku ya Sabato.**

Yesu alipomkaribia mtu aliyekuwa na mkono ulionyauka katika sinagogi yao; Mafarisayo wakataka kushindana Naye tena kwa kumuuliza kama kwamba sheria ilimkubalisha kuponya mtu siku ya Sabato. katika mstari wa 12, Yesu akasema kuwa mwanadamu yule alikuwa wa maana zaidi kuliko wanyama wanaookolewa siku ya Sabato. Katika mastari wa 13 alisema, “Nyosha mkono wako.” Mkono ukawa kama ule mwingine. Sasa elewa hivi; Mafarisayo walipanga jama ya kumwangamiza Yesu.

Ufunuo halisi unapatikana katika Mathayo 12:18-21, kifungu ambacho kimetolewa katika Isaya 42:1-3. “"Hapa ni mtumishi wangu niliyemteua, mpendwa wangu anipendezaye moyoni. Nitaiweka Roho yangu juu yake, naye atatangaza hukumu yangu kwa mataifa yote. Hatakuwa na ubishi wala kupiga kelele, wala sauti yake haitasikika barabarani. Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi ufukao moshi hatauzima, mpaka atakapoifanya hukumu ya haki itawale. Katika jina lake mataifa yatakuwa na tumaini" (Mathayo 12:18-21).

***Watoto walikuwa wakienda kando ya mito na kukata unyasi ili wakatengeze filimbi:*** Walipoweka jeraha kwatika unyasi, hawangejaribu kuutengeneza tena. Waliutupa na kurudi mtoni na kukata unyasi mwingine. Utambi utokao moshi ulikuwa kama utambi ndani ya taa la mafuta. Ulipoanza kutoa moshi badala ya mwangaza bora, walikuwa wanakata utambi uliotoa moshi kwa haraka na kuutupa mbali.

Ufafanuzi wangu ni ya kwamba, "Siwezi kutupa watu kwa sababu wamejeruhiwa. Watu hao ni wa thamani sana kwangu. Kwa sababu maisha yako yamejeruhiwa, ama maisha yako hayaonyeshi mwangaza wa Mungu kwa kusudi fulani lakini ni utambi unaotoa moshi, mimi sitakufa moyo kwa sababu yako. Nitakuja na nitibu majeraha yako ili maisha yako yaweze kung'aa tena kulingana na kusudi la Mungu. mimi sitaachana nawe, wala kusudi lako halitatupiliwa mbali. Uponyaji wa majeraha yako ya ndani utakuwezesha kupanda hadi mahali pa juu sana katika maisha yako na kusudi la maisha yako."

Wanadamu wana moyo mwepesi, tabia ya kiroho na misisimuko ambayo wengi wetu tunatambua. Kusudi la Mungu la kumuumba Adamu lilikuwa uhusiano. Mungu alimwambia daima awe akila kutoka kwenye Mti wa Uzima, Neno la Mungu, na awe akikutana Naye katika Bustani la Adeni. Akaleta Hawa mbele ya Adamu ili awe rafiki wa mahusiano ya hali ya juu. Aliumba Adamu ili awe akimtegemea Mungu kama Baba na mpaji.

Wakati Adamu na Hawa walichagua mti wa Ufahamu wa Mema na Mabaya kwa ujuzi wao na vipawa vyao, bila kumhusisha Mungu, waliharibu uhusiano wa maana sana na Baba yao na wakafa. Walikufa kiroho papo hapo, na baadaye wakafa kifo cha mwili.

***Kuharibika kwa mahusiano kati yao na Mungu kulisababisha hatia, aibu na hata kujikataa.*** Badaye dhambi hii iliwafikia watoto wao na pamoja na wewe na mimi kama udhalimu, au dhima ambayo tulizaliwa ndani yake. Hii ni laana ya kizazi.

**Mahusiano yaliovunjika na jamii zizizofaa zinaweza kuonekana katika uzao wa Yesu**.

Mambo yasiofaa na mahusiano yaliovunjika yanapatikana katika kizazi baada ya kizazi. Sisi wenyewe tumezaliwa katika jamii ambazo zimejaa mahusiano yaliovunjika, na kwa vyovyote tunakula matunda ya dhambi za babu zetu. Watu wengi wanaoishi katika jamii mabazo hakuna baba wanajipata wakidhulumiwa kimapenzi na mfano wa akina baba. Wengine wana baba, lakini mama hatakubali baba aweze awaadhibu watoto wake. Wengine wameteswa na baba zao.

Kwa hivyo, wao hujipata wakiishi maisha yasioelezeka. Hii pamoja na mitindo ya maisha ambayo Mungu hakukusudia watu wake wapitie. Pengine tuna mazoea ya ulafi, madawa ya kuleyva, pombe, labda sisi ni wakamilifu au ni wa kidini kishaeria. Haya yote ni njia tu za kujaribu, "Kuponya" majeraha yetu ya ndani. Yote husababishwa na mahusiano yaliovunjika. Labda kwa sababu ya kufanikiwa au pesa tunazotumia, ama mapenzi yasio na mpaka na mahusiano ya kujamiana. Kisha tunapata matunda ya tiba na mahusiano yaliovunjika, mengi yao yakiwa ni aibu, kujikataa, mfadhaiko, hasira, hisia za kujiua, chuki, ubinafsi, kutaka kuoa mtu kwa kusudi lisilofaa, na mengineo.

Watu wengi hugeukia dini, wengine watalaamu wa akili na moyo, na wengine wataalamu wa kawaida. Wengine wanatumbukia kwa njia zao za kuponya, wakitaka kukemea kila mtu na wanaishi maisha yanayolenga kupata faida katika haya maisha, na mengi unayoweza kupokea, ya kufurahisha, ya ajabu, ya kufaulu, pesa, mamlaka na mengineo.

Ulikuwa ufunuo wa kweli kwangu nilipogundua ya kwamba mengi kati ya maradhi haya ya wanadamu yamesababishwa na sababu moja, ambayo ni uhusiano uliovunjika na utengano uliohusika nao, uwe umepita ama ni wa sasa, na hasa ikiwa unamhusisha baba. Tukitambua ya kwamba, mapenzi ya Mungu kwetu ni uhusiano wetu naye na mahusiano mema kati yetu na watu wengine, sio la kushangaza eti uhusiano uliovunjika unasababisha shida hizi zote.

Hata tukiwa na baba wazuri kiasi gani, ama tumetoka katika jamii ilio na msingi dhabiti, ikiwa uhusiano wetu na Baba wa Mbinguni sio sawa, lazima tukakutane na mambo yote ambayo nimetataja.

**Sisi kama watumishi wa kanisa tunapaswa kuwa na uponyo wa Mungu katika mawazo yetu!**

Ni ombi langu Mungu atatupa upendo kwa wote waliojeruhiwa na ya kwamba, tutawaona kama watu wanaostahili rehema na upendo.

Maandiko ya Kihibrania yanatuonyesha hadithi za watu ambao hawakufaa kwa njia fulani. Hebu fikiria juua ya Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Daudi, Musa na wengineo. Hadithi hizi ni za kweli na

zinatuonyesha ya kwamba Mungu ha kukata tamaa juu ya viumbe wake, ingawa wakati mwingine mambo yalikuwa mabaya na ilimdidi afikirie mara ya pili. Hata hivyo hajawahi kufa moyo kwa sababu hakupatwa na jambo lolote kighafla.

Maandiko ya Kihibrania yanaleta matumaini. Yananena juu ya Mkombozi, Masihi, atakayekuja na suluhisho la mambo yote yaliovunjika kati yetu na baba zetu, hasa Baba wetu mabaye ni Mungu. Yananena juu ya damu ya mwanakondoo asiyena mawaa aliyemwaga damu kwa ajili ya dhambi zetu.

Zaburi 103 inatupa matumaini kama inavyosema katika mistari ya 1-4 na 12-13. "Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA. Naam, vyote vilivyo ndani yangu vilihimidi jina lake takatifu. Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA Wala usizisahau fadhili zake zote. Akusamehe maovu yako yote. Aukomboa uhai wako na kaburi, Akutia taji ya fadhili na rehema." "kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi. Kama vili baba awahurumiavyo watoto wake, Ndivyo BWANA anavyowahurumia wamchao."

**Mtazamo mypa na ulio na nguvu wa aina ya msamaha**

Dhambi na makosa hayatuathiri tu wakati tumeyatenda, bali hata wakati tumekosewa na na watu wengine. Elewa ya kwamba Mungu ana matibabu ya dhambi ambazo tumetenda na hata zile zimetendwa dhidi yetu na watu wengine. Kwa kawaida, baadhi ya watu wanaona msamaha kama jambo ambalo Mungu hututendea wakati tumefanya dhambi, lakini tutajifunza mengi tunapo endelea kusoma sura hii.

**Ni vigumu sana kufahamu upendo wa Mungu**

Katika kitabu chake "Songs of Songs,"[2] (Wimbo ulio bora" Watchman Nee amefanya kazi inayofaa kabisa. Jitihada yake moja

[2] Nee, Watchman. Song of Songs. Christian literature Crusade. Fort Washington PA. 1965, ukurasa 115.

katika uandishi kuhusu upendo wa Mungu umetolewa Katika ukurasa wa 115

> *"Kiwiliwili chake kama kazi ya pembe, iliyonakishiwa kwa yakuti samawi" (Wimbo ulio bora 5:14b).*
>
> *Neno kiwiliwili linaeleweka vyema kama kikao cha mchomo wa moyo, neno sawa na hisia za ndani ambazo zinapatikana katika sura 5:4 ambapo inasema "moyo wangu ukachomeka kwa ajili yake." Sura hii inashiria ya kwamba Yesu alikuwa Mwanadamu aliyekuwa na hisia za moyo, na hata moyo wake ukachomeka kwa upendo mkubwa aliokuwa nao kwa watu wake. Kinyume na vito vingine ambavyo havina uhai, pembe hutolewa kwenye ndovu. Pembe matokeo ya uchungu na inaonyesha ya kwamba upendo wake ulizaliwa na uchungu mwingi na mateso yake hadi kufa kama mwenye dhambi. Kuchomwa moyo kwake kwa ajili ya watu wake kuliota ndani hisia zake za kipekee kwa sababu ya ukuu wa mateso na kifo alichopitia kwa ajili yao. Hisia zikiwa "zimepambwa kwa dhahabu" ni kama picha za kuchongwa kuto kwa pembe zinazodhihirisha ustadi na ubora wa kazi ya anayechonga.*
>
> *Uchongaji wao ulionyesha hisia zake na upendo wake haukuwa wa kawaida. Yalifanyizwa "kwa yakuti samawi", ili kuonyesha usafi wa mbingu kama vile Kutoka 24:10 inavyosema: "Wakamwona Mungu wa Israeli; chini ya miguu yake palikuwa na kama sakafu iliyofanyizwa kwa yakuti samawi, kama zile mbingu zenyewe kwa usafi wake." Yakuti samawi yalizingira hisia zake za ndani: hatimaye, wakati hisia hizi za upendo zilitoka ndani ya Mpenzi wake, zilikuwa safi kiasi gani!*

**Tiba**

Zaburi 68 inatoa matumaini ya uponyo wa ndani, katika uhusiano uliovunjika kati yetu na baba, ambao ni chanzo cha kukataliwa kwetu. "Baba wa yatima na mwamuzi wa wajane, Mungu katika kao lake takatifu huwakalisha wapweke nyumbani; Huwatoa wafungwa wakae

hali ya kufanikiwa; bali wakaidi hukaa katika nchi kavu" (Zaburi 68:5-6). Hapa, Mungu anatuonyesha anajua mahitaji yetu. Ni jambo la kushangaza kuona upungufu wa watu wengine. Walikaa kama watu waliopotea, lakini walipogundua Mungu ndiye Baba wao aliyemkamilivu, maisha yao yakabadilika.

Kumbuka, Yesu alichukua majeraha ya kukataliwa kwetu, akakataliwa na Baba yake pale msalabani. Saa tisa alasiri Yesu akalia kwa sauti kubwa, "Eloi, Eloi, lema sabakthani?" Maana yake, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" (Mariko 15:34)

Mungu ananena maneno ya kushangaza kupitia nabii Malaki katika kitabu cha mwisho cha Agano la Kale: "Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya BWANA, iliyo kuu na kuogofya. Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana." (Malaki 4:5-6).

Nimekuwa nikitazama Maandiko kwa miaka nikitafuta ufunuo. Ni kama nilielewa, lakini mara mingi nimekuwa nikitamani kuona mengi kuliko yale ninaona hata yale ninayojua. Haya Maandiko yamesemwa kwa tafsiri iliyopanuliwa kwa maneno ya Kihibirania kma ifuatavyo:

"Nitawatumia ninyi ambaow mnabeba Jina la Eliya ama kwa maneno mingine (ambalo jina Eliya linamaana kenu) ambao husema "Yehova ni Mungu" wao. Nitaufunua moyo wangu kwa hawa watu, ili niwafanye manabii wa ufunuo nitakaowapatia. Ufunuo na unabii huu utakuwa uso wa wakati wa mateso ya mwisho wa dunia na mataabiko ya siku hizi. Hawa watu watatangaza ujumbe wa wale wanajihisi wamekataliwa mifano ya baba zao. Na huo ujumbe ni "Yesu, Mwana Wangu, amechukua kukataliwa kwenu kwa sababu, nilimkataa pale msalabani. Alichukua haya kwa ajili yako, na sasa ninaweza kugeuza moyo wangu kwenu kwa upendo wangu, na kwa wengi watabadilisha mienendo yao ya uhalifu na kunirudia mimi kama Baba yao wa kweli."

Sina nafasi ya kukueleza haya yote, lakini nina hisi ya kwamba nimeweka maana ya ufasiri wa Kihibirania.

Malaika alimwambia Zakaria, babake Yohana Mbatizaji ujumbe kama huu. Atamtangulia Bwana akiongozwa na nguvu na roho kama Eliya. Atawapatanisha kina baba na watoto wao; atawafanya wasiotii wawe na fikira za uadilifu, na hivyo amtayarishie Bwana watu wake" (Luka 1:17).

**Yesu alitenda muujiza kama ilivyoandikwa katika Marko sura ya 2, na ninamaani Marko inasimulia hadithi hii kuliko teologia ingine yeyote. (Marko 2:1-12).**

1. *Baada ya siku kadhaa, Yesu alirudi Kafarnaumu, watu wakapata habari kwamba alikuwa nyumbani.*
2. *Basi, wakaja watu wengi sana hata nafasi yoyote ikakosekana mlangoni. Yesu alikuwa akiwahubiria ujumbe wake,*
3. *wakati mtu mmoja aliyepooza alipoletwa kwake akiwa amechukuliwa na watu wanne*
4. *Kwa sababu ya huo umati wa watu, hawakuweza kumpeleka karibu na Yesu. Basi, wakatoboa sehemu ya dari iliyokuwa juu ya mahali alipokuwa Yesu. Walipokwisha pata nafasi, wakamteremsha huyo mtu akiwa amelala juu ya mkeka.*
5. *Yesu alipoona imani yao, akamwambia huyo mtu aliyepooza, "Mwanangu, umesamehewa dhambi zako."*
6. *Baadhi ya walimu wa Sheria waliokuwa wameketi hapo wakawaza mioyoni mwao,*
7. *"Anathubutuje kusema hivyo? Anamkufuru Mungu! Hakuna mtu awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Mungu peke yake."*
8. *Yesu alitambua mara mawazo yao, akawaambia, "Mbona mnawaza hivyo mioyoni mwenu?*
9. *Ni lipi lililo rahisi zaidi: kumwambia mtu huyu aliyepooza, `Umesamehewa dhambi zako`, au kumwambia, `Inuka! Chukua mkeka wako utembee?`*
10. *Basi, nataka mjue kwamba Mwana wa Mtu anayo mamlaka ya kuwasamehe watu dhambi duniani." Hapo akamwambia huyo mtu aliyepooza,*
11. *"Nakwambia simama, chukua mkeka wako uende nyumbani!"*

12. *Mara, watu wote wakiwa wanamtazama, huyo mtu akainuka, akauchukua mkeka wake, akaenda zake. Watu wote wakashangaa na kumtukuza Mungu wakisema, "Hatujapata kamwe kuona jambo kama hili."*

***Tazama mstari wa 5 Yesu aliposema "mwanangu."*** Jina "mwanangu" kwa Kingiriki ni "teknon" ambalo maana yake ni "Yule ambaye ana baba na jamii, lakini hawana uhusiano na yeyote." Tazama watu wa jamii ya mtu huyu hawakumleta kwa Yesu, lakini aliletwa na watu wanne waliokuwa na imani. Yesu alimsamehe dhambi zake kwanza, baadaye akashughulikia uhusiano uliovunjika, na hatimaye akapokea uponyaji.

***Tazama yale Yesu alimwambia afanye katika mstari wa 11.*** "Nakwambia simama, chukua mkeka wako uende nyumbani!" Ni nafikiri Yesu alitaka mtu aende na awarudie watu wa jamii yake, awasamehe na kisha awaelekeze kwa Yesu.

Nina amini hii ni picha ya kanisa halisi, linalotumia imani kuwaleta watu waliopooza kwa Yesu. Je, tutawapeleka watu kwa Yesu tu, na kumwachia afanye kazi, badala ya sisi wenyewe tujaribu kuwarekebisha, jambo ambalo husababisha majeraha zaidi.

"Teknon" haimanishi hakuna uhusiano, lakini kwa kawaida ina maanisha mmoja aliyezaliwa. Nina amini Yesu alimaanisha kama vile nimekueleza. Kuna maneno mengine ambayo Yesu angetumia.

***Unaweza kuwa hujapooza mwili lakini umepooza katika roho au mienendo yako.*** Pengine umepooza ndiposa hauwezi kuacha tabia yako ya mazoea ya madawa ya kulevya, ulafi, kutazama ponografia, ama tabia zinazozidi kiasi. Labda unakula ilikuponya utupu wa uhusiano wako; au unaumiza mwili wako kama vile kujikata ama kujiumiza kwa njia yeyote ili usikie uchungu. Labda umeshindwa kuwacha tabia ya kufanya ngono isiozuiliwa vizuri, kutazama ponografia, hasira, mfadhaiko, na mengineo. kupooza kwako kwa nje kuna uponyo wa ndani kwa sababu Yesu alilipa gharama yote.

Tena Yesu akasema, "Umesamehewa dhambi zako." Kwa maneno mengine, Mimi (Yesu) nimechukua dhambi ambazo zilikuwa zimevunja uhusiano kati ya baba, mwana, na familia. Kusamehe kuna

maanisha kutupilia mbali. Kukataliwa na utupu wa uhusiano ambao hufanya mtu apooze kumebebwa na Yesu pale msalabani. Yesu angesema kwa urahisi, “Mwanangu, ninaenda pale msalabani kwa miaka kadhaa na pahali ambapo nitakataliwa na Babangu ili usamehewe na dhambi zako zitupiliwe mbali.

Isaya 53:5 inasema, Yesu alijeruhiwa kwa makosa yetu; Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.

Yerenia alisema, Siku zile hawatasema tena, Baba za watu wamekula zabibu kali, na meno ya watoto wao yametiwa tganzi. Bali kila mtu atakufa kwa sababau ya uovu wake mweneyewe; kila mtu alaye zabibu kali. meno yake yatatiwa ganzi” (Yeremia 31:29-30). Kwa maneno mengine, katika Agano Jipya, Yesu atachukua yale hayangewezekana katika Agano la Kale. Laana za kizazi cha kale hazitadhulumu watu tena, kwa sababu Yesu ameteseka kwa ajii yetu.

***Tazama jinsi ilivyotendeka!*** Mara, watu wote wakiwa wanamtazama, huyo mtu akainuka, akauchukua mkeka wake, akaenda zake. Watu wote wakashangaa na kumtukuza Mungu wakisema, "Hatujapata kamwe kuona jambo kama hili."

Unapomwachilia Yesu aingie ndani kabisa na akusamehe mambo ambayo umefanyiwa na wengine, au pengine dhambi za uzinzi zilipitishwa kwako kupitia ukoo wa babu zako na ukubaliane naye akupe huo msamaha, pia hizo hali za nje zitaponywa. Ukiishaelewa picha hii kubwa kuhusu msamaha, itakusaidia kuwasamehe wale wanaokukosea ama jamii waliokuambukiza dhambi kupitia kizazi.

***Uponyaji huanza ndani na kujidhihilisha kwa nje.*** Kuna njia ambayo tunaweza kufanya kazi pamoja na Roho Mtakatifu, ili tuweze kumruhusu aingie ndani, pale kilindini, katika majeraha yetu ya ndani.

## Wakosaji au Waathiriwa

Hadi pahali tumefika tumekuwa tukitazama waathiriwa wa kukataliwa, jinsi wanavyopata majeraha. Pia tutazingatia ukweli ya kwamba wanao sababisha hali ya kukataliwa kwa wengine wanaweza pia kupata huruma na msamaha. Kuna uwezekano, ikiwa wewe ni

mmoja wa wakosaji pia wewe ni muathiriwa. Unaweza kuwa na hisia ya kwamba umekosa unapoendelea kusoma kitabu hiki. Haufai kujihisi umehukumiwa. Hukumu yako ya mwisho inastahili kuwa kusamehewa kupitia kazi ya Yesu Kristo. Ndio, alichukua dhambi zako, na sasa amesimama ili akusamehe. Anakuita, kubali msamaha unapokili na kuomba msamaha na kujipatiana mikononi mwake ili upokee uponyaji wako. Unaweza kuona kama uponyaji wako hauji kwa haraka, lakini endelea kufuatilia kwa dhati.

Usiku uliopita kabla ya kuandika mambo haya, mtu mmoja ninayemfahamu alikuja kwangu akiwa na ushuhuda. Nilipomaliza kuandika ukurasa huu, kulikuwa na shuhuda zingine tatu. Nilijua mwanfunzi huyu wa Yesu alikuwa amekata kauli na tena alikuwa kwenye utumwa wa dhambi za kujamiana. Hata kama ni mwaminio, alijaribu kabisa kuwa huru. Alinishuhudia ya kwamba, majeraha yake yalitokana na babake, ambaye hakumlea vyema. Hata hivyo., alimsamehe babake. Sasa babake ni mfuasi kamili wa Yesu. Ni mtu ambaye ana shauku la Neno lake Mungu. Rafiki huyu wangu aliniambia babake ni kama ‘mfalme Daudi” ambaye alitenda dhambi mbaya sana na mwishowe akawa na moyo ulioelekea kwa Mungu.

**Usitawi/Ufanisi wa roho**
**(3 Yohana 1-4)**

*1. Mzee, kwa Gayo mpenzi, nimpendaye katika kweli.*

*2. Mpenzi naomba yote na kuwa na afya yako kama vile roho yako ifanikiwavyo.*

*3. Maana nalifurahi mno walipokuja ndugu na kuishuhudia kweli yako, kama uendavyo katika kweli.*

*4. Sina furaha iliyo kuu kuliko hii, kusikia ya kwamba watoto wangu wanakwenda katika kweli.*

**Kamusi ya maneno muhimu ya Biblia ya Strong’s imefasiri usitawi/ufanisi katika Yohana 3 kama:**

> *Kuwa na uwezo wa kusafiri bila shida, vizuri, vyema, na barabara bora, safari njema. Kusitawisha/kufanikisha, kuongozwa katika njia ilio ya ufanisi, ushindi. kuzaa*

*matunda, kufika mwisho, kinyume cha kuangamia, kushindwa.*

Hii haikuwa ahadi kwa Gayo, ambaye aliandikiwa barua hii. Lakini yalikuwa mapenzi ya mwandishi, Yohana, kama vile sisi tunavyoweza kuandika na kusema, "Natumai u salama na mahitaji yako yote yametoshelezwa." Katika mstari wa tatu, Yohana ameongeza kwa ile tumaini, jambo moja, ya kwamba wakati unaishi katika ukweli wa injili kamili ni lazima ufanikiwe.

***Ufanisi wa roho unaanza kama vile umeelezwa katika mstari wa 3 hapo juu na "kuishi katika ukweli wa injili kamili."***

Tunastahili kwanza kufunganisha imani yetu na vile Yesu alifanya kwa ajili yetu na aliyetufanya tuwe vile tulivyo. Kisha, tufanye kulingana na imani hii, kama vile neno "amini" katika Biblia ni neno la kitendo.

***Ufanisi wa roho unakamilishwa kwa kuuchukua msalaba wako kaatika maeneo matatu katika roho yake.***

***1. Hiari:*** Je, una uhakika Yesu ndiye kiongozi wa maisha yako? Umemfanya kuwa Bwana wako? Hii ni sharti ya wokovu, kumfanya awe Bwana wako. Kuokolewa ni kukombolewa kutokana na hatari.

***2. Nia:*** Je, wewe huchukua msalaba wako na kuchukua mateka mawazo yako yasio ya kiungu yale na unaruhusu neno la Mungu liponye mawazo yako?

***3. Hisia:*** Je, unaruhusu hisia zako zitawale maisha yako ama unachukua msalaba na kuambia hisia zako zirudi nyuma yako?

***Hii ni kuishi maisha yako katika ukweli wote wa injili.*** Hii ndio itaponya roho yako. Ufanisi wako wa roho utafuata baada ya kuchukua msalaba wako, kama ilivyoilezewa hapo juu, hatimaye, ufanisi katika maisha yako utafuata.

**Msaada wakati wa shida za kifedha.**

Watu wengi hufika "mwisho wao" hasa katika maeneo ya kifedha. Ni kupitia mlango huu ambapo Yesu anafanya watu wengi wamuamini pamoja na Baba yake. Mimi huyaita mabadiliko haya, kubadilishwa kupitia hitaji kubwa. Ikiwa umeshindwa kufanya maisha yako mema

kifedha, wewe ni mmoja na wale wanaotaka kuponywa kama yule aliyepooza katika Marko sura ya 2.

Hebu fikiria: Mtu aliyepooza hangeweza kufanya jambo lolote maishani mwake. Hakuwa anawategemea wengine kwa maisha yake tu, bali hata hangeweza na kupata watoto. Hata heshima yake ilikuwa duni sana na ukweli ni kuwa alikuwa akiishi maisha bila matumaini.

Ukijipata kwenye hitaji kuu, aanza kuishi maisha ya "maisha ya ushindi" ambayo tutaelezea katika kitabu hiki na utabadilishwa kutoka mwana/binti wa *teknon* (yule aliyezaliwa bila uhusiano wa karibu) hadi mwana/binti wa *huios* kama inavyoelezewa katika Ufunuo 21 hapo chini.

Mungu anatuonyesha katika Ufunuo ya kwamba, baada ya kupitia katika mambo magumu na kusimama na Neno lake katika hali za mateso, mashaka, na kujaribiwa tusiamini Mungu, ya kwamba mwishowe wetu tutashikana pamoja kwa nia ya ajabu na Mungu, Baba wetu, mwenye kututosheresha.

"Yeye ashindaye atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu" Ufunuo wa Yohana 21:7. Sisi tunarithi vitu vyote. sasa sisi sio wana wasio na uhusiano wa karibu na baba, teknon, lakini katika Andiko hili, mwana anatafsiriwa *huios*.

***Tafsiri ya Huios kulingana na Kamusi ya maneno muhimu ya Biblia ya strongs***

*Wale wana mcha Mungu kama baba yao, wale kwa tabia na maisha yao yanakaa yake Mungu, wale wanongozwa na Roho wa Mungu, wana upole na furaha ya kumwamini Mungu kama vile watoto wanafanya kwa wazazi wao ( Warumi 8:14, Wagalatia 3:26), baadaye katika baraka na utukufu wa maisha ya milele watavalishwa heshima za wana wa Mungu. Jina ambalo limetumiwa kumuelezea Yesu Kristo, kama yule ambaye anafurahia pendo la Mungu, aliyeskikamana Naye katika upendo wa karibu, anayetii mapenzi ya Baba katika matendo yake yote.*

**Mimi pamoja na whariri  wenzangu tuna shuhuda juu ya vile Mungu, kupitia uhusiano wetu wa huos pamoja Naye, umefanya miujiza kwa fedha zetu na haja zingine maishani mwetu.**
Nina nena kuhusu Mungu anayekuja kupitia maisha yetu ya fedha, kupita vile tunaweza kufanya kwa nguvu na vipawa vyetu na hata na roho zetu. Tulivyokuwa tunapitia hali hii ya uponyaji, ni kama inakaribia kufanana katika mambo fulani tuliokuwa kukipitia katika hali ya fedha zetu. Tulianza biashara kubwa, madeni zetu yaliondolewa, tukapata pesa za huduma, tukapata nyumba, na wasiwasi wa kukosa pesa kila siku ukaisha kabisa. Tulimwona Yesu akitushughulikia maishani mwetu na hata kati hali yetu ya kifedha. Hata sasa tunamwona kama Mfalme wa Ufalme wa Mbinguni. Tunaweza kushuhudia ya kwamba, tulioutafuta kwanza ufalme wake, na haki yake; tulizidishiwa mambo yote tuliohitaji (Mathayo 6:33).

**Katika sura zinazofuata, tarajia himizo letu katika mambo haya matatu muhimu:**

1. Kuimarisha uhusiano wako na Mungu, ubinafsi, na wengine
2. Kushirikiana na Mungu anapofunua majeraha yako ya ndani na anapokuponya, ama kwa lugha ya Biblia, anapokusamehe.  haya yote ni katika uhusiano!

# Sura ya 2
# Kwa Nini Mungu Hukuweka Huru Kutoka Utumwa?

Tumekuwa tukiangazia uponyaji wa majeraha ya ndani kupitia msamaha unaoleta kufunguliwa kutoka kwenye utumwa. Tuliona ya kwamba majeraha yetu yanatokana na dhambi za aina tofauti; dhambi dhidi yetu kutoka kwa watu wengine kama kukataliwa, au kunyanyaswa, dhambi zetu wenyewe, na dhambi za kizazi ambazo tunaweza kurithi kutoka kwa babu zetu. Tumeona vile Yesu alichukua dhambi zetu zote. Akachubuliwa kwa majeraha yetu, na tukiamini haya, tutatoka kwenye utumwa na tuwe huru. Pia tumeona ya kwamba, ili sababu yetu kufunuliwa ni ili tuwe na uhusiano bora na Mungu.

Tumefunika mawawazo yanaosema ya kwamba, upendo wa Mungu ndio ulio na nguvu kuu na dhahiri na ya kwamba kukataliwa kuna nguvu hasi. Kukataliwa na baba, mfano wa baba, ama pengine kurithi laana ya kukataliwa, aina moja ya jeraha baya sana. Aina hii ya jeraha la ndani hutuzuia kuona kusudi la Mungu, ambalo ni kuwa na uhusiano wa karibu sana na Mungu, aliye Baba wetu.

## Kwa nini Mungu anataka tuwe huru?

Watu wengi wanatazamia hali ya "kuwa huru" tu, na baadaye wapoteze kusudi halisi, uhusiano na wao na Mungu. Agano Jipya limesema wazi ya kwamba, tuliumbwa ili tuwe mtumwa kwa mtu Fulani; hatuna chaguo. Chaguo letu la pekee ni tuwe watumwa wa shetani au watumwa wa Yesu na Baba. "Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mme kuwa watumwa wake yule mnaye-mtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki? (Warumi 6:16).

***Mungu anataka tuwe huru ili tumchague, na tuishi kwa ajili Yake..***

"… tena alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao" (2 Wakorintho 5:15).

Mungu anajua njia ya pekee ambayo tunapaswa kuishi ili tuzae matunda na tufanikiwe maishani ni kuishi kwa ajili Yake tu. Anatupenda sana na angependa tuishi kwa ajili Yake yeye, na tukifanya hayo tutakuwa tukitafuta yale yatatufaidi pekee.

**Ndoto zilizopotea? Je, unahisi maisha yako hayana kusudi?**
***Mungu anataka "Wewe Uwe Huru"***

Watu wengi, hata waaminio wamepoteza (ama hawajawahi kuwa) na ndoto na maono, kwa kusudi la maisha yao. Mungu amekufunganisha na kusudi la kushangaza maishani, ambayo itakuwa "tele" machoni mwako. Anakuweka huru, sio kama mtu ajitegemeaye, lakini kama mtu aliye chini ya utawala wa Yesu Kristo. Matokeo ni kwamba utatoka kwenye utumwa na kuingia kwenye uhusiano na Yeye. Utarithi kusudi asili la maisha na ndoto za Mungu zitafufuka na kuwa kweli. Mimi pamoja na wahariri wangu waliochangia katika uandishi wa kitabu hiki tumeshuhudia mambo haya yakitendeka maishani mwetu.

Sisi sote tumeona Mungu akifanya mambo zaidi ya ufahamu wetu, kupita ndoto zetu, ambazo hatuwezi kuandika yote.

Waefeso 3:20 inasema, "Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu."

**Jifunze kutokana na utumwa katika Misri na kutoka**

"Nawe umwambie Farao, BWANA asema hivi, Israeli ni mwanangu mimi, mzaliwa wa kwanza wangu; name nimekuambia, Mpe mwanangu ruhusa aende, ***ili apate kunitumikia***, nawe umekataa kumpa ruhusa aende; angalia basi, mimi nitamwua mwanao, mzaliwa wa kwanza wako" (Kutoka 4:22-23)

Tazama neno "kunitumikia." kwa Kihibrania ni *abad* ambalo linamaanisha kuabudu na pia kufanya kazi ngumu kama mtumwa. Katika kutoka, Mungu alitumia maneno haya ili kuelezea utumwa ambao watu wake walikuwa mikononi mwa Farao. Hii haimanishi kuwa Mungu ni mkuu wa kazi ngumu kama vile Farao ama kama jinsi sheteni alivyo. Lakini, hakuna uhuru kwa manadamu. Unaweza tu

kuwa huru kama mtumwa wa Yesu, anayekupenda na aliyetoa maisha Yake kwa ajili yako.

***Mungu anataka watu wake wawe huru.***

Mungu alikuwa ameamua kuchukuwa hatua Yake, hata kama Farao (shetani) ama watu wangeshiriakana Naye au la. Shetani hakuwa na chaguo. Mungu alikuwa anaenda kujeruhi adui ili aweke watu Wake huru hata kama ni wao waliokuwa wachukue hatua hiyo nyingine na kumtumikia Yeye na kuwa na uhusiano mwema na Baba yao, Mungu.

Mungu hakutaka wa mtumukie tu, bali alitaka wamtolee dhabibu pia. "Nao watakusikia sauti yako, nawe utakwenda, wewe na wazee wa Israeli kwa mfalme wa Misri, na kumwambia, Bwana Mungu wa Waebrania, amekutana nasi, basi sasa twa kuomba, tupe ruhusa twende mwendo wa siku tatu jangwani, ili tumtolee dhabihu Bwana Mungu" (Kutoka 3:18).

Sasa wewe jiweke katika hali ya Mungu na maelezo yake ya ufasiri wake wa uhusiano. Maana ya dhabihu ni kufa. Hiyo inamaanisha agano la damu na hakuna uhusiano wa Mungu (hata katika ndoa) pasipo na agano la damu. Na hakuna agano la damu, bila kufa kwa wahusika wote wawili. Vile tunasema hapa, ni lazima tuchukue msalaba wetu kila siku ili tuweze kuwa na uhusiano mwema na Mungu. Hatuwezi kumwaga damu ya mwili, lakini damu ya roho zetu za kale, vile tulivyokuwa wachoyo na ubinafsi usiobadilika kabla ya kupatana na Yesu. Tutaona hivi karibuni vile Mungu mwenyewe alimwaga damu Yake kwa ajili ya uhusiano huu.

***Musa alifika mwisho akili zake.***

Alimwambia Mungu katika Kutoka 5:22-23 ya kwamba, tangu alipomwendea Farao na ujumbe wa Mungu wa kuachilia watu waende, Farao hakuwaachilia, ila aliongeza mateso kwao.

Mungu akajibu, "Bwana akamwambia Musa sasa utaona nitakavyomtenda Farao. Maana kwa mkono hodari atawapa ruhusa kwenda zao. Na kwa mkono hodari atawafukuza katika nchi yake. Kisha Mungu akasema na Musa akamwambia, mimi ni Yehova nami nilimtokea Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, kama Mungu Mwenyezi,

bali kwa jina langu Yehova sikujulikana kwao. Tena nimelithibitisha agano langu nao, la kuwapa nchi ya Kanaani; nchi ya kukaa kwao hali ya ugeni. Na zaidi ya hayo, nimesikia kuugua kwa wana wa Israeli, ambao Wamisri wanatumikisha, nami nimeikumbuka agano langu" (Kutoka 6:1-5).

***Kwanza Mungu alitaka kabiliana na adui na baada ya kushinda adui, azingatie uhusiano Wake na watu Wake.*** Tazama katika Kutoka 6:1-5, Mungu alisema atajitambulisha kwa mara ya kwanza kwa jina tofauti. Badala ya El shaddai atatokee kama Yehova, avunjae utumwa. Jina Yesu linamaanisha "Yehova ndiye wokovu." Mungu alikuwa akimaanisha, "Mlinijua kama Mungu Mkuu lakini sasa nitawaonyesha upande wangu mwingine. Mimi ni Yesu, mvunja utumwa. Mtaniona niki mwaga damu ikukuweka huru."

***Mungu alikuwa analete Mwanawe katika picha ili aweke watu wake huru ili wazeze kutoka na wakamtumikie, Baba***. Kila wakati Yesu hutuelekeza kwa Baba. Yesu alposema, Yeye ndiye njia ya kwenda kwa Baba, ni sawa na hadithi iliyo katika Kutoka. Yehova ndiye aliyekuwa mvunja nira ili watu wawe huru kwenda kuabudu, kutoa dhabibu, na kuwa na uhusiano na Mungu. Hata kama tumefungwa hivi kwamba hatuwezi kukubali nguvu za Mungu za kuvunja nira, Yeye bado anaendelea mbele kutusaidia.

"Musa akawaambia wana wa Israel maneno haya; lakini hawakumsikiliza Musa kwa ajili ya uchungu wa moyo, na kwa ajili ya utumwa mgumu" (Kutoka 6:9). Hii inaonyesha jinsi utumwa wa vizazi vingi uliathiri wana wa Israeli

Kutoka sura ya saba kuendelea, Mungu alianza kuweka tauni juu ya miungu ya Wamisri. Tauni ya kumi na ya mwisho ilikuwa ni Pasaka. Hii inasimamia msalaba, damu ya Yesu, na damu ya agano. Hii inamanisha kwamba hasira zote za Mungu ziliwekwa juu ya mwana kondoo wa Mungu. Pasaka ni mfano wa msamaha na pia wa kumpokonya Farao na shetani silaha kwa sababu dhambi zote zilizamehewa. Hivyo ni kusema, makosa yote uliofanya na uliofanyiwa na wengine yalikuwa juu ya Yesu. Alijeruhiwa kwa sababu yo maovu yetu. Kukataliwa kwako kuliwekwa juu ya Yesu msalabani.

Sasa watu wakawa huru kwenda kuabudu, kutoa dhabibu na kumtumikia Baba Muumba wao mle jangwani. “Akawaita Musa na Haruni usiku, akasema, Ondokeni tokeni katika watu wangu, ninyi na wana wa Israeli; endeni, kamtumikieni BWANA kama mlivyosema” (Kutoka:12:3). Mungu aliwashauri watu watoke Misri kwa haraka kabla ya mikate yao kuchacha. Wakati tunaona tumepata uhuru wetu ni chaguo letu kukimbia kutoka kwenye utumwa wetu wa kale na kujenga uhusiano wetu na Mungu.

***Ni watu wawili tu kutoka kikundi cha kwanza walifika nchi ya ahadi.***

“… ila Kalebu mwana wa Yefune, mke nizi, na Yoshua mwana wa Nuni; kwa kuwa wao wamemwandama Bwana kwa moyo yote” (Hesabu 32:12). “Kwa kuwa Bwana alisema juu yao, Hapanabudi watakufa nyikani. Napo hapakusalia mtu mmoja miongoni mwao, isipokuwa Kalebu mwana wa Yefune na Yoshua mwana wa Nuni” (Hesabu 26:65).

Tukiangalia katika Kitabu cha Hesabu ni wazi kuwa Yoshua na Kalebu walitumia wakati wao mwingi katika hema ya makutano kuliko watu wengine. Walikuwa na imani walipokuwa wakipeleleza nchi kwa maana imani huja kwa kusikia Mungu akiongea. Ni lazima walikua na uhusiano wa karibu na Mungu. Hii pia ilimsaidia Musa na akasimama mahali pa Mungu wakati aliugonga mwamba kuonyesha Mungu alikuwa amekasirika nao.

***Kuna chaguo mbili tu kwako***

Chaguo hizi ni kukuleta katika uuhusiano wa ndani na wa kudumu na Yesu ama ufe katika jangwa.  Kwa sababu hii, tuna sisitiza uhusiano mwelekevu sana. Karibu watu 2,000,000 walikimbia kutoka utumwa wa Misri na ni wawili tu katika hawa wote ambao hawakuangamia jangwani. Hawa ni Yoshua na Kalebu. Walitumia wakati wao katika hema ya makutano. Walizingatia uhusiano wao na Mungu kwa bidii.

**Yesu alitoa dhahibu ili tuwe watu huru.**

Hata hivyo, chaguo letu ni kuitikia wito wa uhusiano wa agano la damu liloanzishwa na Mungu. Pasipo kuzingatia uhusiano huu tutabaki tukiwa watumwa au wafungwa.

Imesemekana "Wazimu ni kufanya jambo moja mara nyingi na kutarajia matokeo tofauti." Pasipo kujenga uhusiano mwelekevu na Mungu kama vile Yoshua na Kalebu, tutabaki katika utumwa tofauti tofauti.

***Nidhamu yetu si kufuata sheriafulani au utaratibu wakujisaidia, lakini ni lazima tufanye ambayo ni yetu.***

Ingawa hatuwezi kujiadhibu ili tuache tabia fulani ama tujifananishe na mfano wa Kristo, kuna nidhamu ambayo ni lazima tuishike. Ni lazima tujifunze njia za kujenga uhusiano mwema. Ikiwa hatujazoea njia hizi, kufanya mazoezi ndio nidhamu yetu. Tuliumbwa kwa uhusiano, hasa na Mungu. Kushikana na uhusiano huu kunalete matunda yasio ya kawaida maishani mwetu. Uhusiano huu wa wakaribu utaleta tabia yake Mungu kwetu na matunda mengine maishani mwetu bila kujisumbua. Nguvu zake zitatubadilisha kabisa. Bidii yetu ni kuweka huu uhusiano sawa na kusimama kinyume na adui.

Yesu alisema katika Yohana sura ya 17 ya kwamba uzima wa milele ni "Kumjua" Yeye pamoja na Baba yake. *Kujua* ni maelezo ya uhusiano. Paulo alisema katika Wafilipi sura 3 ya kwamba shauku yake ni kumjua Yesu. Hata alisema, halihesabu mambo yote kuwa hasara ili amjue Kristo na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake. Ninaweza kushuhudia ya kwamba nimemjua Mungu kupitia mazoefu yaku karibu sana na "kifo na kufufuka" katika maisha yangu.

**Maono kutoka kwa Mungu hulete nidhamu ya kibnafsi.**

"Pasipo maono, watu huacha kujizuia; Bali ana heri mtu yule aishikaye sheria" (Mithali 29:18). Utafiti wa maisha ya watu ambao wamefaulu katika maisha kutoka kwa watalamu wa upasuaji hadi kwa watu wa vibarua huonyesha jambo tu moja sawa katika hao wote. Wako na nidhamu ya kibinafi. Si ni nidhamu ya kibinafsi ya kuapa

kutofanya jambo, lakini ni kama ilivyokuwa na wanafunzi ya kufanya jambo njema.

Mtume Paulo aliteseka kutokana na uzoefu mmoja wa kujihesabu kuwa muadilifu. Maono na shauku la kumjua Yesu imeelezewa katika Wafilipi sura ya tatu. Hii iliweza kumtoa Paulo katika mazoea. Ikiwa ilifanyika hivyo kwa Paulo pia itafanyika hivyo kwako. Utaongeza bidii kwa nidhamu yako kinyume na kukataa. Hii pia itakusaidia kuvunja tabia zingine.

Petero aliweka mambo kadhaa ya nidhamu katika 2 Petro 1:5-9. Katika mstari wa 10, alisema "Kwa hiyo ndugu, jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe." (2 Petro 1:10)

**Ustadi wa mahusiano.**

Mwanadamu amepoteza njia zote za uhusiano. Uhusiano wetu ni jambo la kwanza kulingana na Mungu.

Ikiwa una uhusiano mkuu na Yesu na Mungu, wacha maoni yafuatayo yawe ukumbusho wa kukuhekimisha. Ikiwa uko katika njia ya kueneza uhusiano, pengine maoni haya yatakusaidia.

***Ni lazima tukutane na Mungu katika ukumbi wa ukweli***.

Yesu ni kweli; Roho Mtakatifu ni Roho wa kweli; Na ninaamini kuna mambo mawili muhimu ya ukweli.

***Kwaza: Ukweli wetu uko pale tulipo.***

Hii ni kutambua ugojwa wetu, makosa, dhambi, kiburi, hisia, kutosamehe na pengine hukumu kinyume na Mungu. Nilazima tulete yote kwa Mungu. Tufungue roho zetu kabisa. Tukifanya hivyo tumesamehewa na kuoshwa (1 Yohana 1:9). Tunachukua msalaba wetu tunapomenyana na kuungama dhambi zetu mara kwa mara, lakini hatutoshereki katika sehemu ambazo hatuonyeshi tabia ya Yesu. Hebu tuhakikishe hatulaumu wengine na kujihesabu kuwa sisi ni wenye haki, lakini tuungame dhambi zetu kwa mwingine ili tuweze kuponywwa.

Na tena wacha tuweze kutambua kwamba hakuna anaye hukumiwa (Warumi 8:1-2) tunapoendeela na imani katika Roho kwa

Bwana Yesu! 1 Wakorintho 11:31 inasema, "Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu tusingehukumiwa."

***Ukweli halisi ni neno la Mungu.***

Neno la Mungu ni Yesu. Na neno la Mungu ni kuu na sio la kawaida, ni chombo cha agano la damu na pamoja Mungu, na ni msingi wa kumsikia Mungu na kuwa na ushirikia na yeye. Na neno lake litatufanya tuwe na picha na begu ya kiungu ndani yetu. Hutuletea imani. Na tunashikanishwa na Mungu kupitia Yesu aliye Neno.

Neno linalochukuliwa na kusemwa kwa shetani litamfanya shetani akutorokee pamoja na pepo wachafu, maishani mwako na hali zako zote. Tunaponena neno la Mungu kutoka kilindini cha moyo wetu, mawazo yetu yanafanywa upya na Mungu anapewa mamlaka kuachilia malaika na nguvu zote kwa niaba yaetu,

**Tunapeana vitabu vya mafunzo juu ya ustadi wa mahusiano ukitaka.**

[3]Mto unaotiririka ni sura moja katika kitabu chetu "Kukua au Kufa"[4] na inapeana hisia kadhaa ambazo zimewekwa kwa njia za uhusiano unapooenekana katika hekaru la Agano la Kale. Haya mafunzo yamesaidia watu wengi kerekebisha uhusiano wao na Mungu. Mto unaotiririka ni nidhamu ya kushangaza na ya kawaida yakutuwezesha kufikia uwepo wa Mungu.[5] Daily Moral Inventory imetumiwa na watu wengi sana wale wameamua kuuliza Mungu awaonyeshe wapi maishani mwao wanafaa kuomba msamaha kwake. Hiyo karatasi imefunganishwa katika mwisho wa sura hii.

Tafadhari jua ya kwamba uhusiano wako wa kipekee hauna utaratibu katika njia hizi kama vile zimeandikwa. Chukua ustadi huu kama mwongozo.

Somo lilaofuata ni kwa ajili usadi wa mahusiano haya.

[3] Tovuti ya Mto Utiririkao htpp://www.isob-bible.org/flowingriver.htm

[4] Tovuti ya Kukua au Kufa, htpp://www.isob-bible.org/openlessons.htm

[5] Tovuti la Daily Moral Inventory htpp://www.isob-bible.org/innerheal/moralinventory.htm

# Sura ya 3
# Nguvu za Maono
## Ustadi wa Mahusiano

Ningependa kupanda maono katika moyo wako, ambayo yatakupa nguvu za kushikiria na kuweka nguvu uhusiano wako na Mungu.

Uhusiano wako na Mungu kupitia Yesu Kristo na Roho Mtakatifu utaleta amani, uhuru, ufanisi wa kila aina, na zaidi ya yote utakuleta katika uhusiano wa karibu sana na Yesu. Atakuwa halisi kwako; utamsihi na usikie akikunenea mara kwa mara. Hata hivyo, uhusiano kama huu unahitaji nidhamu ya kweli kwa upande wako. Mahusiano yote yanastahili nidhamu, lakini yakiwa sawa, mahusiano mambo yanayotosheresha na ya kufurahia.

**Maono huleta nidhamu**

“Pasipo maono, watu huacha kujizuia; Bali ana heri mtu yule alishikaye sheria” (Mithali 29:18).

*Moyo wa mwanadamu umeumbwa ili uweza kufanya kazi juu ya maono, ama kwa maneno mengine matumaini*

Jambo la kwanza ambalo Mungu alimwambia Adamu kama njia ya kubarikiwa, ni kunena maono.

“Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi” (Mwanzo1:28).

Wakati kitabu hiki kinazungumza zaidi kuhusu kuwa huru kutoka kwenye utumwa ambao unaonyeshwa kwa njia isiyo ya Mungu, utaona unapoendelea kusoma ya kwamba ukweli halisi unaochangia katika uhusiano wako na Mungu unaendelea kuimarika. Jambo hilo pekee litakuweka huru.

Kuanza na kuimarisha uhusiano wako na Mungu kunastahili nidhamu kwa upande wako. Mungu amefanya mambo tyoye, sasa upande wako kujitwalia kazi yake ya kushangaza kupitia uhusiano wa karibu na yeye.

Nidhamu inahitaji maono kama vile imeelezwa katika Mithali 29:18. Watu wengi wamegundua ya kwamba, ili wafaulu maono yanatakikana.

Wakati daktari amekupatia dawa, ni lazima uwe na nidhamu ya kumeza dawa hizo kwa sababu una maono ya kupona.

Unapoenda pahali unapofanya kazi kila siku, unafanya kazi hata kama huipendi, kwa sababu uko na maono utalipwa.

Unapoenda shambani kuvuna unafanya hiyo kazi kwa sababu uko na maono ya utakula.

Nataka kuweka maono ndani ya moyo wako na ninaomba itakufanya wewe na mimi tuwe na nidhamu ya hali ya juu katika uhusiano wetu na Mungu. Angalia ahadi zilizoandikwa hapo chini kuhusu nidhamu:

**1. Maono ya amani na uhuru**

2 Petro 1:2

"Neema na iwe kwenu na amani iongezwe katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu."

Tazama, faida hizi kuu zinakuja kupitia kumjua Mungu.

**2. Maono ya ufanisi wa kiungu**

"Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo. Maana nalifurahi mno waliokuja ndugu na kuishuhudia kweli yako, kama uendavyo katika kweli. Sina furaha iliyo kuu kuliko hii, kusikia ya kwamba watoto wangu wanakwenda katika kweli" (3 Yohana 1:2-4).

Tazama ufanisi wa mambo ya kuisha, unaleta ufanisi wa roho yako. Ufanisi wa roho unakuja kwa kulingana na uhusiano wako wa karibu na Mungu.

**3. Maono ya uhusiano wa karibu; Mungu kuwa halisi kwako. *Waefeso 3:17-19***

"Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo, ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana na urefu, na kimo, na kina, na kuujua upendo wake

Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulilvyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.

***Wafilipi 3:10***

"Ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wamateso yake, nikifananishwa na kufa kwake."

**4. Maono ya kutoshereka katika mwito wako, kusudi na mwisho wako**

"Yeye alituokoa, akatuita tuwe watu wake yeye mwenyewe, si kwa sababu ya matendo yetu wenyewe bali kwa sababu ya kusudi lake na neema yake. Alitujalia neema hiyo katika Kristo Yesu kabla mwanzo wa nyakati" (2 Timotheo 1:9).

**5.** Maono ya kuwa kama Yesu na kuwa safi.

2 Petero sura ya pili inasema tuendele kumjua Mungu ili tuweze kurithi ahadi Zake, ambazo, kati ya mambo mengine zitatufanya tufanane na Yesu. "Kwa kuwa uweza wake wa uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa (2 Petro 1:3,4).

**6.** Maono ya thawabu za milele

"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima amini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao" (Waebrania 11:6).

"Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mabo aliyotenda kwa mwili kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya (2 Wakorintho 5:10).

"Na kila ashindaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo bali sisi tupokee taji isiyoharibika" (1 Wakorintho 9:25).

"Tazama naja upesi; na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo" (Ufunuo wa Yohana 22:12).

**Maono ya kutoka kwa Mungu yalmtoa Gideoni kutoka kwenye utumwa na kuwa huru, kusudi na ufanisi**.

Gideoni alikuwa anaishi maisha ya kushindwa kama mwana wa Israeli hadi Mungu alimpompa maono. Alikuwa na heshima duni sana kwa sababu adui wa Israel walikuwa wanashinda. Alikuwa na picha mbaya yake maishani. Mungu alijua jinsi nguvu Zake zingeweza kubadilisha. Mpango wa Mungu alikuwa anene mambo ambayo yalionekana kama hayawezekani. Uhusiano wake wa karibu na Mungu unawezesha Mungu kutupatatia mfano wake kamili jinsi tuonavyo sisi. Vile yeye anatuona ndio ukweli wa vile tunajihisi. Hii ni tumaini, maono!

"Malaika wa Bwana akamtokea, akamwambia, Bwana yu pamoja nawe, Ee shujaa (Waamuzi 6:12).

Katika sura zinazofuata za Waamuzi utaona vile Gideoni na Mungu waliweza kujenga ushusiano halisi wa ndani na wa kipekee. Hii ilimfanya Gideon ajazwe Roho Mtakatifu na akaweza kusikia Mungu kwa njia ya karibu sana. Tena Mungu akamtumia kushinda adui ambao walikuwa wameweka watu wake katika utumwa.

**Jukumu lako**

Mimi naonelea ni vyema utafakari Maandiko ambayo nimeandika hapo juu. Nena, tafakari, na uyaruhusu yaweze kuingia kilindini cha moyo na nafsi yako. Pia, anza kujiunganisha ndani ya njia za uhusiano kama vile imetajwa katika kiambatisho "A".

Ikiwa unaanza kuchukua hatua ndogo. Hatua hizi ndogo zitanjenga uhusiano wako. Nguvu zina sababisha hatua hiyo nyingine kuwa rahisi. Fikiri kuhusu motokaa, inachukuwa nguvu kidogo kuweza kufanya gari iende kutoka maili ishirini na tano kwa lisaa moja, kwa mailii arobaini kwa saa moja. Kuliko vile inaweza isha kutoka maili kumi kwa lisaa moja.. Hii ina maanisha "mwili unao enenda unabaki kwa mwenendo na mwili unaokaa, unaobaki, ama ulio pumzikoni. Tena mwili unaoenda unaweza kuweka mwenendo sawa na ikibadili

nguvu nyingi zahitajika. Ikiwa wewe uko "pumzikoni" na huenendi katika uhusiao wako na Mungu, sasa tumia nguvu za nidhamu yako ili uweze kuenenda kwa njia sawa. Ikiwa huna kiu cha uhusiano huu, ama kiu cha neno la Mungu, mwambie Mungu atende jambo jipya ndani yako.

## Kiambatisho "A"
## Njia za uhusiano

**1. Kata kauli imara ya kufuatilia uhusiano.** Jipeane kabisa kwa Mungu. Tafakari Warumi 12:1-2. Hii ni jibu la agano letu la damu kwa agano la damu kuu iliyopeanwa na Mungu kwa ajili yetu.

**2. Chukua muda wa kusikiliza: Ni lazima uchukue Neno Lake** Maneno ni kama kitu cha kuchukua agano la damu. Neno la Mungu ni Yesu mwenyewe, siokitabu cha ahadi cha kuchukua na kuchagua kutoka. Ni lazima Neno la Mungu lifuatiliwe mara kwa mara na uhusiano wa kila siku, na kuweza kuutazama kwa njia kama kusikiliza Mungu wako. Mwambie Yesu mwenyewe akunenee. Neno lake si la kawaida na linazaa imani kama vile chakula cha kawaida kinazo nguvu za kuzaa. Yesu alisema, chakula cha ukweli ni kile kinapatiana uzima wa milele.

**3. Chukua muda wa kunena: Maneno yako.**
Kuwa mwandishi wa pande mbili na kuwa na kiwango cha hali ya juu cha uaminifu ni njia muhimu ya kuongeza uhusiano wako na Mungu. Andika yale unayohisi kwa uaminifu. Uaminifu wako mwenzako katika agano la damu, Yesu, kutasababisha dhambi zako ziende kwake. Hauwezi na hautashinda jambo lolote maishani mwako bila kuwa na kiwango cha uaminifu. Tunapendekeza uandishi wa pande mbili. Hii ni njia bora sana ya kuruhusu "Kutiririka" kwa Roho Mtakatifu aseme nawe kwa njia ya kipekee na aseme mambo ya karibu. Kwanza, tafuta pahali pasipo na kelele, na uelekeze mawazo yako kwa Yesu, na uanze kumuabudu. Andika yale unataka kumwambia ama kuuliza Yesu. Kisha andika yale unasikia ndani ya

roho yako. Mara ya kwanza, unaweza kufanya makosa, lakini kwa imani na mazoezi, Yeye atakuwa halisi kwako.

***Jinsi ya kutambua ni sauti ya nani unayosikia.***

Sauti ya Mungu: ina thibitisha, inarekebisha, hutoa mwelekeo (ni kweli).

Sauti ya shetani: Inatuweka katika utumwa wa kushindwa na uongo na lawama.

Sauti yako au mwili wetu: Hujitetea, hujipa moyo, hukana, na husingizia au kulaumu wengine.

***Kutahini kama tunasikiasauti ya Mungu***

Je, inakubaliana na Maandiko?

Je, inamtukuza Yesu?

Je, kuna ushahidi katika roho yangu?

Je,inajenga ama inabomoa?

Je, inalete uhuru ama ni utumwa?

***Njia ambazo Mungu hutunenea nazo***

Biblia: Ufahamu wa ufunuo kupitia Roho Mtakatifu

Mwili wa Kristo: Kupitia Waumini wengine, wachungaji washauri. Jihadhari usitegemee hawa peke yao.

Wakati mtulivu: Sauti ya Roho Mtakatifu. (Zaburi 139:23-24, 1 Yohana 1:9).

Mazingira na hali za kila siku maishani: (Yeremia 32:8).

Rafiki unayeamini: Mara kwa mara ni busara kuwa na rafiki unayeamini atakaye kuwa na ujasiri wakukuambia ukweli wa mambo katika maisha yako.

**4. Chukua muda wa kunena: Maneno ya Mungu**. Maadui, shetani, na mapepo mara nyingi huwa kinyume na bidii yetu, uhusiano wetu na Yesu, na ushindi wetu. Wewe mwenyewe ndiwe unaweza kuwakataa. Yesu alikupa mamlaka na uwezo wa kunena Neno Lake kinyume nao. Mungu alimwambia Yoshua, “Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali tafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawa sawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; mana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana” (Yoshua 1:8).

***Nia moja ya kufanya hii ni:***

Soma vitabu vya Zaburi na Mithali kila siku. Soma kwa SAUTI Zaburi tano kila asubuhi. Tumia mpango wa kalenda. Kwa mfano, tarehe tatu ya mwezi soma Zaburi 3, 33, 63, 93 na 123). Pia soma Mithali 3. Ukifuata mpangilio huu atasoma zaburi na mithali yote kwa muda wa mwezi mmoja. Mpangilio huu unafanya upya akili zetu na kunena neno kwa shetani na kukusaidia kushiriki katika mateso ya mwandishi wa Zaburi. Unaweza kupata mambo mazuri katika siku hizi za mwezi katika Zaburi 119.

Pia kuwa makini kusikiliza Roho Mtakatifu ambaye atakupa neno la kupigana vita kwawa wakati fulani.

**5. Tafakari:** Kutafakari Neno la Mungu ni jambo muhimu sana na la maana. Nilidondoa kutoka Yoshua 1:8 ambayo inatuambia tutafakari maneno yake mchana na usiku. Zaburi 1:1-3 inasema, “Heri mtu yule asiye kwenda katika shauri la wasio haki; wala hakusimama katika njia ya wakosaji; wala hakuketi barazani pa wenye mizaha. Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, na sheria yake huitafakari machana na usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, Uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halinyauki, na kila allitendalo liltafanikiwa.”

Kutafakari Neno huondoa mawazo yako ya kimwili ambalo ni tendo gumu. Pia hukubali Neno liingie ndani ya moyo wako. Neno kutafakari linauhusiano na ng’ombe anayecheua. Anatafuna na kumeza na kurudisha mdomoni tena na tena. Hii itaruhusu Neno liingie kilindini cha moyo wako na inapatia Roho Mtakatifu nafasi ya kunena jambo fulani maishani mwako kutokana na Neno.

**6. Kufunga:** Kufunga ni nidhamu ya maana. Kunazo aina nyingi za kufunga na sitaongea kuhusu somo hili hapa. Umuhimu wa kufunga ni ya kwamba, hukataa ile tamaa kuu ya mwili ya kupenda kula. Kufanya hivyo kunawezesha mtu kumsikia Roho Mtakatifu vizuri. Kumbuka mwili una tamaa mbaya kinyume na Roho na tamaa za Roho ni kinyume na tamaa za mwili, Wagalatia 5:17. Nimesoma,

yakwamba, wakati mtu anaona jaa, hata kusikia kwake kwa kawaida ni kuzuri.

**7. Tii Mungu:** Mwambie Mungu akupatie jambo rahisi kila siku ili uweze kumtii. Linaweza kuwa ni kukiri dhambi zako kwake au ni kuteka mawazo yako nyara, ama kumsamehe mtu, ama pengine kupeana zawadi iliyo na gharama.

***Hii ni jambo kumbwa!*** Yohana 14:21-23 inasema, tunapotii Neno Lake, atajifunua kwetu zaidi na zaidi. Mara “utakapomuona” Yesu, uhusiano wako na Yeye hautakuwa nidhamu tena, bali utakuwa shauku ya kufuata.

# Sura ya 4
# Majeraha Kutoka Kwa Watu Wengine

Sura za kwanza chache za kitabu hiki zilitarajiwa kukusaidia kuelewa juu ya majeraha, matokeo yake, na tiba yake kwa njia ya kwaida. Tungetaka kukutia moyo ya kwamba, Mungu anatamani sana kukuponya kupitia uhusiano wako wa karibu na Yeye. Sasa tutakuonyesha mambo kadhaa ambayo yanasababisha majeraha haya, na ni naomba utapata ufunuo wa Roho Mtakatifu na utambue majeraha yalio ndani yako.

Sijihesabu kuwa shupavu katika mafundisho haya ya majeraha ya ndani, dhuluma, na uponyanji wa ndani. Lakini nimejifunza mambo mengi kuhusu hoja hizi kutokana na yale nimepitia na ukombozi, kutoka kwa Neno la Mungu, kutoka kwa kitabu cha uponyaji wa ndani[6] na kutoka kwa Wahariri wenzangu Michael na Karen. Kitabu hiki hakitarajiwi kiwe kilinki kamili ya uponyanji wa ndani, bali kinatarajiwa kiwe chanzo cha majeraha hayo na njia za asili za kuyaponya. Tunasadiki ya kwamba, Mungu atatumia ufahamu wetu wa kimsingi na hali yetu ya kawaida ya uandishi kukutia moyo, pengine muumini wa kawaida, aweze kuzingatia ukamilifu.

**Neno la kukutia moyo.**

Ningependa kukupa neno la kukutia moyo ikiwa pengine ulidhulumiwa, ulikataliwa, au ulijeruhiwa kwa njia moja au nyingine na mtu mwingine au na maisha yenyewe. Ni na kutia moyo ikiwa unang'ang'ana na tabia fulani, kutawalia na kitu Fulani, au hali ya maisha isiyo ya uungu. Unapoendelea katika sura zinazofuata, utapewa suluhisho la shida zako. Haijalishi vile unajihisi, uko kwenye utumwa Fulani, ama ni muda gani umekuwa pale. Hustahili kuishi na hisia ambazo hazitoshereshi maisha yako. Watu wengi waliokataliwa hujihishi kama daima wameshindwa. Wanahisi jambo lolote watakalofanya ama gusa halitafaulu, hata katika uhusiano wao na

[6] Inner Healing – Dunklin Memorial Ministries – nimetumia kwa idhini.

Mungu wa muda mrefu. Wanajihisi kuwa duni miongoni mwa waaminio wengine na hushangaa kwa nini hawana ushusiano wa karibu na Mungu kama watu wengine walivyo.

***Mungu alikuwa wapi?***

Mungu mwenyewe ni Mwenye Enzi. Anatawala ulimwengu kwa ujuzi usiotoshana, vile vile, havunji kusudi lake la asili kwa mwandamu kwake. Anatamani uhusiano wa upendo na mwanadamu. Hata hivyo, ilituweze kufurahia uhusiano wa upendo wetu na Mungu, ni lazimatuwe na nguvu za kupinga mambo yaliyo kinyume na mapenzi ya Mungu, ambayo hupinga ukuu Wake wa kutawala pamoja na upendo Wake. Bila kuwa na uhuru wa hiari, hauwezi kuwa na upendo wa kweli. Kwa hivyo, watu waovu hutenda mambo maovu. Hii ndiyo sababu mambo mengi hutendeka maishani mwetu na hatuwezi kuyaelezea. Unaweza kujiuliza, "Mungu alikuwa wapi wakati babangu alinikataa?" Au, "Mungu alikuwa wapi wakati mtu wa jamii yangu alininajisi nilipokuwa mchanga?" "Sikuwa na uwezo wa kuchagua wakati huo." Mtu mwingine anaweza kuuliza kwa nini Mungu aliruhusu Ayubu, "aliyekuwa mwaminifu kwa Mungu" apitie yale aliyoyapitita. Tuna kijitabu kuhusu hoja hii kinachojulikana kama Job's Journey[7] (Safari ya Ayubu).

Hakuna anayeweza kukupa jibu kamili kuhusu maswali haya ya "kwanini" ila tu, tunaishi ulimwengu uliojawa na dhambi. Hata hivyo nina amini Neno la Mungu hutupatia majibu mengine, ambayo hutupatia amani, usalama, karibu, na kusudi. Kazi ya Yesu msalabani na kufufuka Kwake, pamoja na kuzaliwa upya kwako kunapatia nguvu kupitia neema. Kubadilisha kila hatari ambayo umepitia na kuwa Baraka. Nina amini ukubwa wa hatari umepitia ni ukubwa wa nguvu za utajiri. Zingelikuwa nikifanya kazi ya Mungu katika ufalme wake isipokuwa ni hatari ambazo nilipitia hapo awali. Ninajua Michael na Karen wanatumiwa sana na Mungu kuleta uponyaji wa ndani kwa watu wengi katika mataifa mengi kwa sababu ya hatari ambazo wao walipitia hapo awali. Badala ya kutharao hali ulizopitia,

---

[7] http:www.isob-bible.org/lc-upload/job/job.pdf

ruhusu Mungu azibadilshe “takataka” zako hadi “vitu vya dhamani” kama vile imefafanuliwa katika kitabu chetu Junk to Jewels[8] (Takataka hadi Vito).

Pamoja na hayo,  ni nafikiri ni muhimu kuweka umuhimu wa kwanza na makusudi ya Mungu katika mawazo yako. Siamini ni makusudi ya Mungu kutupatia maisha rahisi, akihakikisha hatukutani na mambo mazito. Hata kama hataondoa uchungu, hii ni njia anayotumia kutenda kazi yake ya kawaida na kusudi hilo likiwa kushindwa kwa shetani pamoja na wafuasi wake. Yale Ayubu alipitia yaliweza kumshinda shetani na nguvu zake katika eneo la utawala wa Ayubu. Ni nina amini huu ndio msingi wa kitabu cha Ayubu. Paulo “Aliyetumwa kutoka kwa shetani”  “mwiimba ndani ya mwili wake” (2 Wakorintho 12) ulishindwa katika maisha ya Paulo. Kushinda majeraha na hali zinazoleta kuteseka ni jambo kubwa kuliko kupata uhuru. Pia inahusu kushinda mambo ya kishetani na laana zilizo katika eneo letu la utawala.

“Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu; tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake” (Wokolosai 1:24*).*

**Utafiti ya akili huonyesha kukataliwa ni jambo linaloumiza sana.**

Kutoka: New Scientific - tarehe 9 oktoba 2003.

> *Moyo wa upweke umetumia millennia ukijaribu kupata uchungu wa kukataliwa ndani ya kuchora mashairi na nyimbo. Sasa wasomi wakisayansi wameiona ikiyumbayumba kiajabu katika picha za akili kutoka kwa mwanafunzi wa chuo anayeugua kukataliwa.*
>
> *Picha za akili zinaonyesha mambo mawili ya akili ambayo yanafanyishwa kazi na uchungu wa kiwiliwili na pia infanyishwa kazi kwa sababu ya hali ya kutengwa na wengine.*

[8] http://www.isob-bible.org/biblepick.html

Nilimhoji dada mmoja ambaye amekuwa akifanya kazi katika hospitali ndogoya binafsi na amehitimu katika utafiti wa magonjwa ya “Alzheimer’s na dementia”. Alinimbia wakati mtu ana tukio la kumshtua, adrenalini ipitia kipimo huingia akilini. Matokeo ni kwamba ‘alama ya kemikali’ hujirekodi akilini. Alama hii inanguvu ya kurudia tukio la kustua mara kwa mara. Dada huyu ni Mkristo.Nilimuuliza kama anafikiria uponyaji wa ndani na msamaha kupitia damu ya yesu unaweza kuponya hali hii. Alisema itaweza bila shaka. Nikapitiza ya kwamba alama hii hubadirika kutoka kigaga hadi kovu. Tutazungumzia haya katika sura zinazofuata. Watu waliokobolewa kutoka hali ya kutawaliwa na mambo Fulani katika maisha hutuambia walikuwa wamekabiliana na “hali ya kufurahia”mara kwa mara kutokana na alama hizi, ambazo wakati mwingine zilizababishwa na muziki ambao walisikiliza, madawa, ponografia, au matukio mengine yakusisimua. Mashujaa wa vita mara kwa mara husumbuliwa na kiwewe ambacho walishuhudia vitani.

***Mojawapo ya matokeo ya kukataliwa ni moyo uliopondeka.*** Mithali:15:13 inasema, “Moyo wa furaha huchangamsha uso; Bali kwa huzuni ya moyo roho hupondeka.

***Moyo uliopondeka, ambao husababishwa na hali ya kukataliwa unaweza “kukauka” ama kupoteza hamu ya maisha.***

Mithali:17:22 inasema, “Moyo uliochangamka ni dawa nzuri; Bali roho iliyopondeka huikausha mifupa.

***Ikiwa hamu ya maisha imeisha, hakuna nafasi ya uponyaji kutendeka.***

Mithali: 18:14 inasema, “roho ya mtu itastahimili udhaifu wake; Bali roho illiyovunjika nani awezaye kuistahimili.”

**Nguvu hasi katika ulimwengu wote ni upendo wa Mungu**

Mungu ni Upendo; kwa hivyo, upendo ni nguvu za Mungu za kipekee. Sisi tuliumbwa ili tuwe na uhusiano wa ndani na Mungu. Zaburi 139:13-16 inasema, “Maana wewe ndiwe uliyeniumba mtima wangu, uliniunga tumboni mwa mama yangu. Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu ya kutisha. Matendo yako ni ya ajabu, na nafsi yangu yajua sana. Mifupa yangu haikusitirika kwako,

nilipoumbwa kwa siri, nilipoungwa kwa ustadi pande za chini za nchi. Macho yako yaliona kabla sijakamilika; chuoni mwako ziliandikwa zote pia, siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado.

Waefeso 1:4-5 inasema, “Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuweka misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo. Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na Uradhi wa mapenzi yake.”

Pia tuliumbwa na kuunganishwa na mzazi wetu. Hizi daraja zilinjengwa kwa upendo, kukubalika, na kwa sababu ya kuhitimu kusafiri kati ya hawa watatu, Mungu, mama, na mtoto. Hii ni hitaji ya kihisia na pia ya kimwili. Tunahitaji upendo na kukubalika kama vile tunavyohitaji maji na chakula. Mungu alituumba tukiwa na haya mahitaji kwa sababu yeye ako na vyote na ana uwezo wa kutimiza yote kupitia uhusiano wetu na yeye

1 Yohana 4:8,16 inasema, “Yeye asiyependa, hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni upendo. Nasi tumelifahamu pendo alilonalo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. Mungu ni upendo, naaye akaaye katika pendo hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake.”

Ikiwa upendo ndio nguvu hasi katika uumbaji, kwa hivyo, tunaweza kusema, kutokuwa na upendo ndio nguvukatika uumbaji. Kukataliwa ni kukataa upendo na kukubalika maishani mwetu. Uhusiano unavujika wakati umekosa hali ya kugusa, maongeo ya moja kwa moja, na hisia za usalama. Kugusa kunaleta watu pamoja. Kugusa kwa kwaida ni ya muhimu na huu ni mwanzo wa kujenga uhusiano. Mhariri wangu wa kuchangia, Michael, alipokuwa akisafiri Afrika, alitambua jinsi watoto wanabebwa na mama wao wakiwa wamefunganishwa kwa usalama begani. Alishuhudia vile jambo hili huonyesha usalama wa mtoto kwa mama. Hakuona mtoto hata mmoja akiwa amekosa amani. Kwa upande mwingine, bila kuguswa kuna upotevu mkuu sana unaoendelea. Michael alizaliwa kama wakati wake haujafika. Na mara tu alipoachana na mamake aliwekwa katika kiangulio. Badaaye, alipokuwa akipitia hali ya kuponywa ndani na Mungu, aliweza kumwonyesha vile alivyokuwa katika kiangulio, vile alivyokuwa akishangaa na uwoga na hasira zikamwingia. Mara nyingi

daraja zetu zimeharibiwa maishani kupitia kukataliwa. Kukataliwa ni jambo linaloumiza sana. Ni jeraha la kawaida la kutokana na mateso yanayotukumba katika maisha. Uhusiano uliovunjika na mambo ya kukataliwa huja kwa njia zote na viwango vyote na kutoka mahali popote. Tutaangalia baadaye katika kitabu hiki majeraha yanayo sababishwa na ndoa, hata kanisani, familia ya kanisa, ama serikali ya kanisa.

Aina zingine za kukataliwa ni kutokubali, kukataa, utupu, chuki, kujitenga, kudharao, kutojua, kuachilia, kuepuka na kutokubali. Kukataliwa sio jambo la kawaida kila mara.

***Kukataliwa kunaweza kusababisha uwoga wa kukataliwa na kujikataa mwenyewe.***

Baadhi ya mambo mengine ambayo husababishwa na uwoga wa kukataliwa kulingana na kitabu cha uponyo wa ndani ambacho tumekuwa tukitumia ni hasira, uchungu, dini za ushushi na vikundi visivyo halali, kujikataa, uchungu wwa moyo, kujihurumia, kupoteza tumaini, mfadhaiko, kujitenga na hisia za kujiua. Katika kitabu cha uponyaji wa ndani tunatumia mambo haya katika vikundi vine. Mambo haya yote yametokana na matunda ya kukataiwa.

**Matunda ya kukataliwa na sababu za kukataliwa.**

Kukataliwa ni kama mti wenye mizizi kali. Unaweza kutoa matunda kali. Hali ya kukua na matunda kutalingana na kiwango cha kukataliwa. Hapa chini kuna baadhi ya matunda ya kukataliwa:

- Kutokuwa na uwezo wa kupokea upendo - tunaamini, sisi so wamaana.
- Kutokuwa na upendo wa kupenda wengine – tunakaa mbali, bila kuamini
- Kutokuwa na usalama – tunangojea kukataliwa
- Kujiepusha – tunafikiki tukosalama tunapojitenga
- Kushuku – Kila mtu anataka kututumia vibaya
- Duni – Kwa sababu tunahisi sisi sio wa maana
- Kuona haya - kila mtu ni bora zaidi kutuliko
- Uoga wa kutofaulu – Hudhibitisha kuamini kwangu mimi ni dhaifu

- Kumuogopa binadamu – “Kama wangelijua mimi nilikuwa nani….?
- Kuogopa kukataliwa – Hutuzuia kuwa sisi halisi
- Kujikataa – tunaamini uongo ni ukweli
- Ndoto – tunafikiri mambo yetu wenyewe.

***Sababu za kukataliwa***
***Kukataliwa kabla ya kuzaliwa:***

1. Kupata mimba haraka sana unapoolewa.
2. Kupata mimba karibu na mtoto uliyepata hivi karibuni
3. Kusumbuka kifedha ama kijamii.
4. Kuogopa kutofaulu.
5. Vita baina ya wazazi watarajiwa.
6. Kutoa miimba kuliopangwa ama kujaribiwa
7. Wazazi kutofurahia mtoto yule wamepata.

***Sababu zingine.***
***Shida za mwili.***
***Waathiriwa wa kudhulumiwa kwa matusi, kupigwa, na kunajisiwa.***
***Kuathiriwa na hali ya mazingira .***

Kwa mfano, mtoto asiyenauhusiano wa uzazi na mamake, awe ni motto alyeasiliwa, wazazi waliovunja ndoa yao, shida zilizoletwa na walimu ama wale mliosoma nao.

Mungu alituumba tuwe na uhusiano Naye kama Baba, na chanzo cha mambo haya ni kukataliwa kutokana na uhusiano wa kidunia. Hii imesababisha majeraha mengi ambayo imetudhuru. Suluhisho ni rahisi ikisikika, lakini si rahisi kumruhusu Roho Mtakatifu kutuongoza katika nidhamu ya kugundua mizizi ya ndani iliyo na uwezo maishani mwetu. Kwanza ni kusamehe. Kusamehewa na kufuatilia na moyo wako wote uhusiano wako na Mungu. Waebrania 12:15 inasema, “ona ya kwamba hakuna mtu yeyote atakaye kosa neema ya Mungu na hakuna mizizi chungu itakapokuwa na kuleta shida na kuchafua wengi.”

Kukataliwa huku kulio na mizizi ya ndani kunaenezwa katika utoto wetu na tumbo la mama. Kukataliwa huku kunajenga imani yetu. Kwa mfano, wazazi wanapata mimba kwa haraka wanapooana na mara moja tu uoga unawaingia. Baba mtarajia anajihisi si kama yeye kwa sababu hakuwa anatarajia mtoto wakati huu. Kwa sababu hii' baba anatumia wakati wake nje akinywa pombe na kusherehekea na marafiki wake kama njia ya kuepuka ukweli usiotakikana kwa wakati huu. Naye mama anakaa na uoga na kutoamini kwamba hii miimba imesababisha akataliwe na bwanake. Hata anaanza kujiuliza kwanini akaolewa na huyo mume. Hata anaendelea kuwaza kuhusu kutoa mimba kwa sababu hakuwa amepanga kupata mimba. Haya yote, uoga, kukataliwa na vita inapelekewa mtoto aliyetumboni mwa mama. Kukataliwa huku kunaweza kuwa mwanzo wa kujikataa na pia kumkataa motto huyu. Mtoto anaweza kuzaliwa baada ya wakati wake kwa sababu ya mafikira mengi ambayo mama inapitia akiwa mja mzito. Juu ya kutozaliwa wakati unaofaa mtoto hataweza kushikana vizuri na mamake siku za kwanza ama miezi ya kwanza maishani kwa sababu aliwekwa kwenye kiangulio. Kukataliwa huku husababisha shida nyingi. Huu unweza kuwa mwanzo wa kuwa na hasira na Mungu, hata mwazo wa kuwa na mawazo ya kujiua kwa sababu yakuona yeye ni "hatia" na hahitajiki. Kuna uchungu mwingi sana kuangalia nyuma na kuona majeraha ya miaka yetu ya hapo awali. Kama wanadamu, tunataka kuchukuwa njia ambayo haina usumbufu. Tukiruhusu Mungu aturejeshe katika sehemu za majerajha yetu na atuponye, tutaweza tutembea pamoja na yesu tukiwa na uhuru ambao Yesu alituletea. Atatuwezesha kushinda majaribu ya kukataliwa na uchungu katika maisha yetu tukiwa watu wazima.

Kama tulivyoona hapo awali, Yesu alifanya miujiza kama vile imeandikwa katika Marko sura ya 2. Hadithi hii ya kupooza inatuonyesha msamahawa dhambi ya kukataliwa kutoka kwa Yesu. Msamaha huu unaleta uponyo wa ndani ambao unasababisha kuzaliwa kwa matunda na kujidhihirisha kutoka kwa kukataliwa. Hatimaye majeraha ya kukataliwa yanaisha.

**Labda haujapooza mwili, lakini umepooza roho ama katika mienendo yako**

Kunauwezekano umepooza kutokana na kutawaliwa na madawa ya kulevya na umeshindwa kuyaacha, ama unatawaliwa hali ya ulafi. Ili kuponya utupu wa uhusiano wako, unafanya mambo fulani yanayokudhuru mwili wako kama kujikata ama mambo mengine machungu. Labda umeshindwa kuacha hali ya kutawaliwa na madawa, kuona picha za ponografia, hasira, ama mafadhaiko. Labda unafanya mambo bila kipimo ama unajisifu ukijaribu kufunika uchungu fulani. Baadhi ya watu wanatumia misisimuko, kujipeana katika michezo na kazi za shetani na mengineo. Kupooza kwako kuna tiba ya ndani ambayo, Yesu aliweza kulipia deni yote. Pengine weww haujapokea "maisha haya tele."

**Aina zingine za majeraha, kukatalilwa na wengine. Imedodolewa kutoka kwa Dunklin.[9]**

*Watu wengi hutoka kwa familia hazifanyi sawa. Hiyo haimanishi kuwa madawa ya kulevya na ulevi uko huko. Pombe na kulewa inakuwa tu mambo ya kuonyesha kutofanya kwa familia lakini kwa njia ya urahisi familia yeyote ile Yesusi kichwa haifanyi sawa iko na ulemavu.*

*Kudhulumiwa kwa matusi, kimawazo, kimapenzi, ama wazazi wanaotarajia makuu kunaweza kusababisha ulemavu katika familia. Wazazi ambao hutarajia ukamilifiu wa hali ya juu husababisha hali ya utendakazi fulani kwa familia. Mtoto anabidika kutenda jambo Fulani ili aweze kupokea upendo na utumishi. Hii ni hali isiyofaa katika familia.*

***Kudhulumiwa kwa matusi**.*

*Kudhulumiwa kwa matusi kwa mtoto kunasababisha hofu na kuchanganyikiwa. Katika mawazo yake, anahisi amekataliwa. Hisia za hasira na shauku la kutoka ndani ya udhalimu huu na kuadhibiwa, inaanza kujengeka kwa sababu mtoto ametumiwa vibaya na mtu*

[9] Inner Healing Haki ya Kumiliki 1992 na Dunklin Memorial Church - imetumiwa kwa idhini ya ISOB.
Tovuti: http://www.isob-bible.org/openless.htm#heal

*ambaye anastahili kumtegemea. Kunauwekano mkubwa hata yeye aatakuwa mtu wa kudhulumu wengine vibaya.*

***Kudhulumiwa kimapenzi***

*Mtoto aliyetumiwa vibaya kimapenzi anaweza kutokuwa na uwezo wa kufungwa moyo wake kwa watu wale wengine. Yeye huonyesha kuwa muathiriwa kimawazo na hana uwezo wa kuamini mtu yeyote yule, hasa walio na mamlaka.*

*Majeraha ambayo hutokana na kudhulumiwa kimapenzi huumiza sana. Yamefanya watu wengi waishi maisha ya uharibifu mwingi. Husababisha kukosa matumaini na kukata tamaa. Nimeshuhudia watu wakikombolewa kimiujiza na wana anza kutumiwa kwa hali ya juu sana na Mungu katika kuwaponya wengine.*

***Kupata mtoto wa jinsia usiotarajia.***

*Mtoto anaweza kuwa anatarajiwa kwa hamu hadi siku ya kuzaliwa. Jinsia ya mtoto ni muhimu sana kwa wazazi wengine. Hata kama hakuna uzito katika chaguo la jinsia, kupata mtoto wa jinsia isiotarajiwa kunaweza kusababisha uharibifu kwa sababu ya mtoto kukataliwa na wazazi. Kwa sababu ya jambo lile mtoto hana uwezo wa kutawala. Jinsia ya mtoto ni uamuzi wa Mungu ambao unapaswa kukubaliwa na wazazi.*

*Wazazi wengi wamechukizwa sana na jinsia ya mtoto wao. Labda sababu ya kukataliwa kwa mtoto hasikuwa kumdhuru, lakini kulitendeka bila kujua athari za matokeo yake.*

*Majeraha haya yanapotokea, shetani huchukuwa nafasi hii haraka sana. Mtoto kukataliwa na wazazi kwa sababu ya jinsia wakati mwingi hufanya vijana kuwa kama wasichana na wasichana kuwa kama vijana.*

*Mtoto aliyekataliwa kwa sababu ya jinsia yake atajua akiwa na umri mdogo sana. Mara nyingi wao hujaribu kuwa kama wale aliotarajiwa kuwa ili waweze kukubarika na wazazi wao. Kuna uwezekano wa mtoto huyu kukua akiwa amejichukia na kujikataa. Jambo hili humfanya awe msenge.*

*Kwa sababu "ametumika" kwa njia isiyo ya kawaida, anahisi uchungu wakukataliwa.*

Inaonyesha, kulingana na yale tumesoma hapo juu kuhusu hali ya mtoto, kukataliwa baada ya kuzaliwa kunaweza kudhuru zaidi kuliko ya yule mtoto ambae hajazaliwa. Hata kama mtoto alizaliwa katika hali ambaye hakuchagua, anaweza kumwambia Mungu amubadilishe na amukomboe. Mimi mwenyewe nimeona haya yakitendeka kwa mtoto mchanga.

Bila kujali chanzo cha majeraha haya, Yesu ni Mkuu na anauwezo wa kuponya na kulainisha mambo. Nimesikia shuhuda za watu waliokombolewa na kuwekwa huru kutokana na mikasa kama hii. Ikiwa unamjua mtu mmoja anayeishi katika haya maisha ya ngono, tafadhali usimhukumu. Badala yake, tenda jambo ambalo litaleta tumaini maishani mwake. Nimesikia majeraha ya aina hii huleta nguvu za kishetani zilizo na nguvu sana katika ulimwengu wa kiroho na ni ngumu sana kuzivunja. Ukombozi unategemea moyo na shauku mwathiriwa. Ikiwa atataka kusaidiwa kabisa, Yesu atakuja amponye na amkomboe.

**Majeraha ya ndani kutokana na ndoa iliyovunjika**

Wakati majeraha tunayopata katika ujana wetu yanaweza kuwa baya sana, majeraha tunayopata katika ndoa isiyo kamilika, kwetu sisi na kwa watoto wetu, yanaweza kutudhuru sana na tuwe watu ambao wanahitaji uponyo wa ndani. Huduma ya Roho Mtakatifu ni kuleta msamaha, toba, kurekebishwa, na matokeo yake ni uponyo.

Ndoa ni agano la damu. Kama agano zingine za damu, kifo cha wahusika wote wawili kinahitajika ili kutumikia moja na mwingine. Bila jambo hili kutendeka majeraha ambayo yanahitaji uponyo wa wote wawili kwa ndoa na kwa watoto pia hutokea. Yeremia 34:18-20 inaelezea ya kwamba, wale wanaovunja agano watapeanwa kwa adui. Na tunajua ya kwamba, msamaha na toba zitaondoa adui maishani mwetu.

Kuaminika katika ndoa sio kunena tu ‘sitawahi taka talaka.” Kusema maneno haya kasha utumie wakati wako mwingi na rafiki zako kuliko mpenzi wako kutafanya ndoa yako iwe talaka iliyo hai. Kuwajibika ni kwako wewe. Yale utafanya siyo mengi kuliko yale hutafanya.

Baada ya kusema haya yote, Mungu anataka kutuosha kutokana na kila hukumu ya ndoa iliyovunjika. Na ikiwa wewe ulihusika na utumbu, utasamehewa dhambi zako na sitaondolewe kabisa. Ikiwa mchumba wako wa kale au wa sasa amekukosea, ni lazima umusamehe ili wewe uwe huru.

Mafundisho mengine yanasema taraka kuwa dhambi ambayo haiwezi kusamehewa, lakini hiyo sio kweli. Mungu hakupanga hivyo katika Neno lake. Tuko na orodha kadhaa zinaitwa "uponyo kutoka majeraha vya ndoa". Zinapatikana katika tovuti yetu http:/www.isob-bible.org/marriage/tocmar.htm. Kitabu kingine muhimu kimeandikwa na Daktari M.G. Mcluhan, Marriage and Divorce[10] (Ndoa na Taraka.)

**Mungu alituumba na hitaji la baba.**

Kutokana na yale nimesoma, vunjiko lote na "baba" wetu ni funguo na kuhisi kukataliwa na majeraha vya ndani kama ilivyosemwa hapo awali, inaweza kuwa ama isikuwe moja kwa moja kuvunjika kwa huo uhusiano wa baba inaweza kuwa dhambi ya kizazi inayotoka kwa uzazi wa baba zetu. Inaweza kuwa ni kuvunjika kutoka wakati wa adamu na Mungu.

***Daudi alinena kwa urahisi (Zaburi 27)***

Daudi aliweza kujua kutoka kwa Mungu kwamba wazazi wa ndugu na familia yake wanaweza kuwa mbali na ukamilifu lakini tamaa moja yake ilikuwa awe mwana wake Mungu na tena awe na ushirika wa kuendelea na baba wa mbinguni

Zaburi 27:10 inasema: Baba yangu na mama yangu wameniacha, Bali Bwana atanikaribisha kwake.

Zaburi 27:4 inasema: Neno moja nimelitaka kwa Bwana, nalo ndilo nitakalolitafuta, nikae nyumbani mwa bwana siku zote za maisha yangu, Niutazame uzuri wa Bwana na kutafakari hekaluni mwake.

---

[10] Mcluhan M.G.,, Marriage and Divorce. Tyndale House Publishers. Wheaton Il. 1991

Yesuakutulipia deni ya msamaha na uponyo ndio tukaweze kuendelwa na maisha yetu ya kale la! Alilipa deni hiyo ya gharama ya juu ndio sisi, kama Daudi, tuwe na ushirika na baba yetu.

**Katika kitabu chake[11] "God A Good Father" Mwandishi Michael Philips ametoa maneno ya maana sana kuhusu ubaba wa Mungu ambayo yamejifungilia kwa nafsi yangu.**

*Ukweli uliyo wa maana sana katika ulimwengu wote unweza nenwa kwa maneno manne: Mungu ni baba wetu, kadri tuna vyoelewa ubaba wa Mungu ndivyo maisha yetu. Itaingiana itakamilika na kuwa na ukamilifu katika uhusiano wetu na muumba aliyetufanya tuishi katika mazingira aliyotuweka.*

*Tunaposoma katika vitabu vya injili kwa macho yetu yaliyo elimishwa upya, tunaanza kuona kwamba baba wa Mungu ndio ukweli wa pekee ambao Yesu alikuwa anaeleza ndio ulikuwa wa msimamo ama ujumbe wake hapa duniani katika ujumbe.*

*Walakini Yesu aliunda msimamo mpya, kando na matokeo machache pote pote katika Agano la Kale, Mungu hakuwa ameeleweka kama baba hakukuwa mafundisho ya dini iliyieleza juu ya utatu mtakatifu hivyo ni kusema hakuna wazo la baba, wala ujuzi wa mwana kutambua Roho Mtakatifu. Yahwe alikuwa mmoja neno Baba halingetumika kwa vyovyote vile kueleza Mungu*

*Pia dini ya Kiyahudi katika siku za Yesu ya kibnafsi. Walimatazama Mungu kama anayepeana amri na hakimu. Musa na Daudi walienenda katika urafiki wa karibu na Mungu, lakini haikuwa hivo kwa watu wengine, amri lazima zingetiiwa na hakimu mwenye nguvu aliyeitwa yahwe alisimama tayari kutoa hukumu amri ikivunjwa.*

*Hakuna mahali popote katika theology ama ulimwengu wa philosophia katika wakati wa Yesu tabia ya kiungu ilitoshanishwa na ubaba.*

---

[11] God A Good Father. Michael Phillips, Destiny Image Publishers, Inc, Shippensburg, PA., 2001, ukurasa 43-49

*Akina baba wa dunia wameondoa utukufu wa Mungu hata usiweze kutambulika ubaba wa Mungu ndio akili ya asili kwa binadamu ambayo ni ya maana, shauku nii ambayo imeumbwa kutazama juu na kumwangalia baba yetu*.

**Yesu alikuja kuponya na kukomboa wanadamu kutokana na uhusiano wa baba uliovunjika.**

Nimeona katika Agano la Kale kwamba Mungu mara mingi aliongoza watu kwa kuacha nyumba za babazao na kumfuata. Kuna ushahidi mwingi wakutosha wa ubaya wa ubaba wa watu wengi kotekote katika Agano la Kale, akina baba ambao hawa kutimiza kazi zao kama baba za nidhamu, upendo kuhusika kudhibitisha, uadalifu,uaminifu na kadhalika. Somo liletumepata katika Yohana nane, linaonyesha, moyo wake Yesukuhusu haya mambo wakati Wayahudi, walisema Abrahamu ndiye baba yao, Yesualiwachanga moto na wakasema hata Mungu ni baba yao, lakini kwa haraka Yesuakawaambia ilibilisi ndiye baba yao. Aliwajuliza dhambi zileziko juu ya maisha yao lazima kwanza zishuguiliwe, kwanza, ndio Mungu awe baba kwao. Maneno ya mwisho ya Yesukwa mwanfunzi wake imerekodiwa katika (Yohana 14-17) na hii ni lazima ikuwe ya kuunganisha tena sisi na baba. Aliongea kuhusu Roho Mtakatifu atakuja iliatuunganishe na baba Mungu. Yesundiye njia, kumanisha kutayarisha mambo na kurejeshea neno, lakini roho matkatifu mtu anaye fanya kuunganisha kwa uhalisi wakati wake.

***Yesu ndiye njia ya Baba:***

Tuna hitaji mtu yule atachukuwa dhambi zetu ili tuwe na umoja naye baba Mungu. Yesu akatenda haya. Tafadhali kila wakati weka hii ndani yako. Kwamba kusamehe kwa dahmbi ni Jambo linahusu watu wote wawili si yale tu tumetenda na kujipatia Yesu lakini hata yale yamefanywa kinyume chetu. Ndio tukaweze kuwa na uhusiano na ushirika wa karibu naye Mungu baba na tena huo umoja tunahitaji Yesu. Neno ni Yesusasa neno ndio njia kwake baba (1 Yohana 14:6) inasema: Yesu akamwmbia, mimi ndimi njia na kweli, na uzima; mtu haji kwa baba, ila kwa njia ya mimi.

***Yesu alituonyesha wepesi wa baba.***

(Yohana 14:9) inasema: Yesu akamwambia mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, filipo? Aliyeniona mimi amemwona Baba; (Wagalatia 4:6) inasema: Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana [huios[12]], Mungu alimtuma Roho wa mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba.

Yohana 16:27 inasema, "maana yeye mwenyewe anawapenda ninyi, kwa sababu ninyi mmenipenda mimi na mmeamini kwamba nimetoka kwa Mungu."

***Tunakuwa na uhusiano wa karibu na umoja na Yesu na Baba***
"Wote wawe na umoja; kama wewe, baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyeituma" Yohana 17:21.

***Baba huyu hatakukuwacha***.

(Waebrania 13:5b) inasema: Msiwe tabia ya kupenda fedha; mweradhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa.Wewe hutakuwa na hofu tena. Mrenendo yakosi kamilifu utatenda dhambi mara kwa mara. Hata hivyo baba yako hatakuacha na kukuachilia. Yeye atakuwa hapo kukugeukiana na kukurejesha. Yeye ako na shauku kukuhusu.  Weka picha katika mawazo yako na moyo kuhusu upendo wa Mungu kwako na vile dhabihu yake Yesumslabani ilinunua uzima wako.

---

[12] Tafsiri ya Huios kulingana na Kamusi ya maneno muhimu ya Biblia ya strongs

Wale wana mcha Mungu kama baba yao, wale kwa tabia na maisha yao yanakaa yake Mungu, wale wanongozwa na Roho wa Mungu, wana upole na furaha ya kumwamini Mungu kama vile watoto wanafanya kwa wazazi wao ( Warumi 8:14, Wagalatia 3:26), baadaye katika baraka na utukufu wa maisha ya milele watavalishwa heshima za wana wa Mungu. Jina ambalo limetumiwa kumuelezea Yesu Kristo, kama yule ambaye anafurahia pendo la Mungu, aliyeskikamana Naye katika upendo wa karibu, anayetii mapenzi ya Baba katika matendo yake yote.

**Fikiria picha ya Yesu akiwa amesimama katikati yako na yule mtu alikuhukumu, hakika akiichukua hiyo dhuluma kwa ajili yako.**

Tazama hizo dhuluma hazingeweza kukudhuru kwa sababu zilichukuliwa naye Yesu. Hapa ndipo Yesu ukweli alikuwa wakati ulikataliwa na kushutumiwa alikuwa, akichukuwa na kuvumilia zile dhambi kwa niaba yako. Na hata yale yote na dhambi zote zimetendwa kinyume na wewe na wengine hata hii weka kwa mawazo ukiisha ruhusu Yesu akaweze kunyonya dhambi kwa kusamehe yule mtu aliyekutendea maovu utakuwa umewekwa huru. Ikiwa hutakubali huu ukweli na uchague kutosamehe, utaendelea, kukuwa mwaadhiriwa na utabaki kuwa mtu aliyegwaruzwa (Isaya 3:4-5) inasema: nami nitawapa watoto kuwamiliki, na watoto wachanga kuwa tawala. Nao watu wataonewa, kila mtu na mwenziwe, na kila mtu na jirani yake, mtoto atajivuna mbele yam zee, na mtu mnyonge mbele ya mtu mwenye heshima.

**Tunaweza kuwa na ujasiri wa kuwa na baba anaye tujali sisi, na mahitaji yetu yote.**

" Tena siku ile hamtaniuiza neno lolote. Amin, amin, nawaambia, mkimwomba baba neno lo lote atawapa kwa jina langu." (Yohana16:23)

Ninaweza elezea haya "hiyo siku, nitakapo kuwa nimefufuka na wewe uwe naye Roho Mtakatifu, utaenda kwake baba kama vile mimi huenda kwake kwa sababu utakuwa "Jina" sawa ama tabia ile ninayo. Yeye atakutenda vile tu yeye hunitenda hata shughulikia hitaji lote lako (hata ile nidhamu unahitaji liwe kwa jina langu.

**Suluhisho.**

Ikiwas majeraha vyetu vingo huja kutokanan na kukataliwa na kukataliwa kule kubaya ama kuvunjika kwa uhusiano kuko nakule yake baba, tena ile uhusiano wa sili unaponya na uko na baba Mungu. Kukataliwa ndio nguvu kubwa ina uwezo kinyume halafu upendo ndio nguvu iliyo na uwezo zaidi kwa uzuri.

***Kwa hivyo uponyo wa ndani uko na hatua mbili za kimsingi:***

1. KuonaYesu kama yeye ndiye antuvumilia kwa dhambi zetu kuwa yeye anaweza kusamehe, wale wamekataa sisi na kutumbu zile dhambi zinatokanan na kukataliwa kwetu. Hii ndio mlango wa hatua illiyo mbele.

*2.* Kuwa na ushirika na baba wetu kupitia kuendelea na uwazi wetu na kupitia Yesundiye neno na kujenga huo uhusiano naye kwa kutii na mapatani ya kubadili

Warumi12:2 inasema: wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu.

**Yesu alikataliwa na kujeruhiwa kwa ajili yangu.**

Naomba Roho Mtakatifu atayafanya haya maandiko halisi kwako wewe (Marko 15:34) inasema: Na saa tisa Yesuakapaza sauti yake kwa nguvu, Eloi, Eloi lama sabakthani? Maana yake, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? (Isaya 53:3) inasema: Alidharauriwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitika; na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauiwa wala hatukumhesabu kuwa kitu.

**Mazoezi ya kukataliwa**

Omba kwanza na uulize Mungu aweze kukudhihirishia kwako wewe kukataliwa tano uliyopitia kabla ufikie miaka kumi. Tena uliza yeye akuonyeshe ile mizizi chungu ukonayo kwa sababu ya kukataliwa, kwa sababu kila uchungu wote uliyo upitia na matunda gain umekuwa nayo kwa sababu yah ii mizizi. Kuomba akipitia haya mambo yote weza kumwuliza Mungu yeye alikuwa wapi wakati huku kukataliwa kulikuwa. Kaulize Mungu akuonyeshe hasira na chuki uliyokuwa. nayo kwake yeye na tena wale wengine na kwa babu ya haya mambo ya kukataliwa na kutubu.

# Sura ya 5
# Majeraha Kutokana na Laana za Kizazi

Niliposoma kuhusu utamaduni , wa watu ulimwenguni , ilikuwa wazi , utamaduni mwingine umeweza kulegeza dini na mara mingi kuiita kuuisha. Kutokana na kueleza kwa mambo haya ni kuabudu kwa maroho wa ukoo, ama babu zetu wqaliwame pita kufa . Nimeona bakuri za chakula zikiwa na mashimo yaliyotengenezwa ili isiweze kutumiwa na wanadamu , na isichukuliwe na mtu , ndio isiweze kutumiwa na wanadamu , na isichukuliwe na mtu, ili roho ziweze kukula kutokana kwake, nazo zinawekwa juu kaburi.

Huku kuabudu mara mingi huonyesha kabisa ni utamaduni usio na ufahamu. Wao hufanya haya mambo ya kuabudu na wanahisi ya kwamba kunao babu zao na wanastahili kuwabariki maishani mwao, ama kuna baraka zingine, ni lazima zitoke kwa hao babu zao. Mara mingi kwa utamaduni ulio na ufahamu, naamini huu unyama, sana sana hujadhihirika vizuri na sio ya kumaanisha. Ina kuwa imezalishwa vizuri kwa tofauti zilizokupatia , njia hizo nguvu za laana za kizazi kuweza kupita. Mara mingi , lakini si kwa hali zote, kuunganishwa kwa familia inaweza tumiwa kama chombo kikuu kwa mapepo kutumia. Sherehe kwa utamaduni ni kama hizi, uungamano wa familia. Wanasherehekea huo mwaka unopita na kuapa ya kwamba watahifadhi kuabudu kwa mapepo ya familia na inaendelea mwaka mwingine. Tumeshapata kuona haya Haiti. Na ninaamini kuwa Mardi: Gras in New Orlians Luvisiana ni 'mtoto' wa huu utamaduni wa Haiti na kwa maoni yangu, hizi sherehe zinafananishwa na sherehe za Mungu , na kwamba hizo zilimaanisha kupitisha baraka zake.

Ilihali inaweza kukuzwa, hiyo ni kuabudu sanaamu. Na kuabudu sanamu ni kuabudu mapepo nahii iko na nguvu sana katika ulimwengu wa kiroho.

***(I Wakorintho 10:19-21) inasema:***

"Basi niseme nini? Ya kwamba kile kilichotolewa sadaka kwa sanamu ni kitu? Au ya kwamba sanamu ni kitu? 20 sivyo, lakini vitu vile waviitavyo sadaka wavitoa kwa mashetani, wala si kwa Mungu;

nami sipendi ninyi kushirikiana na mashetani. Hamwezi kushirikiana katika eza ya bwana na katika meza ya mashetani."

Sanamu nyingi tukirudi kwa historia ya siku za Agano la Kale ziliweza kupotosha kwa hali ya kimapenzi. Maarifa ya vita vyake shetani kwa hii hali ni ya ujanja sana. Anajua mtu kwa urahisi, anaweza kufungwa na kuwa mwombezi wa saanamu na utawaliwa wa kishetani kupitia kupotoshwa kimapenzi.

**Nani familia yako?**

Mara mingi Yesuamenena kuhusu 'kuchukia' familia yako kwa kupendelea Mungu. Dhahiri hakutumia jina chuki. Kama vile mara mingi huielezea. Alimaanisha hatufai kuweka familia ya kawaida mbele ama kuipa nafasi ya kwanza, lakini tuweze kutafsiriwa kwa hii familia mpya ya ufalme wake Mungu. Alijua ya kwamba utawala wa familia unaweza zuia wewe kutoajibika aslimia mia moja kwake Mungu (Mathayo 12:50) inasema: Kwa maana ye yote atakaye yafanya mapenzi ya baba yangu aliye mbinguni, huyu ndiye ndugu yangu na umbu langu na mama yangu.

Watu wengi hutumia wakati mwingi na pesa nyingi wakijaribu kutafuta jamaa zao za ukoo na familia. Hilo si jambo mbaya na hakuna kosa kwa haya na inaweza kuwa ya usaidizi na maana sana. Ninawajua watu wengi sana walio katika uzao wa nne na tano, na niwahuduma waliojazwa nguvu za Roho Mtakatifu , na wamepata uridhi huu wa maana na wameachiwa kama baraka na babu zao. Ilihali kutafuta kule bora, kwa jamii ni kule kunaangazia matokeo ya kuzaliwa mara ya pili, sio kuzaliwa mara ya kwanza.

Wakati utakapoamua kuajibika na kufanya Yesukuwa Mungu juu ya kila eneo la maisha yako, yeye atadhihirisha kwako eti wewe ndiye kiumbe kipya na mmoja wa ukoo wake Yesualiye uanzisha wakati alipofufuliwa kutokana na kifo. Yeye akawa kifungua mimba na wewe uko kwa huo msatari. Ninaseme tena, utakapo una kweli kweli wewe ni nani utaanza kufananisha maisha yako ya inje na vile kuko ndani. Wakati umeimsha wa kutoa makosa maisha yako, kudharau tabia na kutofaulu kwako na uweze aanza kuona huu ukweli , wewe utakuwa huru kuwa wewe.

**Adamu**

Adamu, yule mwanadamu wa kwanza, aliumbwa kwa kawaida. Hii inamaanisha alikuwa awe na roho wake Mungu akikaa naye. Aliweza kuelezewa akae kama ameunganishwa naye Mungu kupitia neno, mti wa uzima na kutoamini akili zake za kujitegemea .Alipokuwa hakika akaanza kuamini na kujitegemea, kutoka kwa neno lake Mungu, alijipata akiwa mfungwa wa shetani, na watoto wake wa ukoo wakapitia hii shida ya kuwa wametengana na Mungu.

Kama tunavyosoma , sisi zote tulizaliwa na huku kutenganishwa , na sasa sisi tuko huru, kuweza kuchagua ukombozi wetu mpya na kuzaliwa mara ya pili. Tunapoenda kuamua hii chaguo ilhali sisi hujipata na mafikira ya kale kuhusu tunavyojiona, ama uhalisi wetu. Biblia inatueleza hivi, tunastahili mawazo yetu kufanywa upya ili tukaweze kuona huo upya wa kweli kile kilitendeka kwa kuzaliwa upya kwetu. Ni kweli ilikuwa ya maajabu sana na tunakuwa na, wakati mwingine mgumu wa kuamini. Ugumu mwingi, ni lazima uwe umetokana na uongo wake shetani, udanganyifu wa kitamaduni, mipango ya kidunia , na mawazo yetu iliyo oza' .

**Baraka na laana.**

Mungu alianzisha ulimwengu na akabariki mwanadamu. Maneno ya kwanza aliyoengea kwa Adamu yalikuwa kuhusu baraka. Mwanzo 1:27-28 inasema: "Mungu akaumba mtu kwa mafano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba."

Walakini, mara yote kumekuwa ni lazima kuwe na nguvu za kinyume kwa jambo lote. Ikiwa kuna upendo ni lazima nguvu za huki kinyume ziwe. Ikiwa kumekuwa na jambo la kutii, ni lazima kuwe na nguvu za kinyume za kutotii, ama dhambi. Kwa hivyo, ikiwa kutakuwa na baraka ni lazima kuwe na uweza wa laana. Na hii inaitwa " taji lisiweza kufanya."

***Baraka za kutii, Laana za kutotii.***

Laana ni kinyume cha baraka, baraka ni aina ya ufanisi ule huleta matunda mazuri na maneno mema ama matendo laana. Ni aina ya kutofaulu inayosababishwa au kuzalishwa kwa ubovu kwa maneno ya

kinyume ama matendo. Katika (Kumbukumbu la Torati 28 na 29) Musa aliweza kuandika baraka za yule mtu atakayetii amri zake Mungu na laana za yule hatatii amri zake Mungu.

Naamini somo kuu kwa Biblia linabadili laana kuwa baraka . Laana zile ziliweza kunenwa katika kitabu cha mwanzo na laana kuweza kumalizika katika kitabu cha ufunuo. Hata mimi ninaamini ya kwamba hii njia ya kutoa ama kumaliza laana ni ya " ushindi "

***(Kutoka 34:5-8) yasema kwamba laana zinapitishwa kuendelea kwa ukoo utakao kuja.***

"Mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu n makosa na dhambi; wala si mwenye kuhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; mwenye kuwaptiliza watoto uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne" (Kutoka 34:7)

Kusudi lile halisi lake Mungu ni tuweze kuwa na baraka zitakazo ufikia uzazi wetu, na hii ni lazima itokane na mwanadamu kuwa huru na uhusiano mwema na Mungu. Hata kama haki ni lazima, iitishe, kwamba, ikiwa baraka zitateremushwa  njia katika uzazi hata laana ni hivyo hivyo. Kuncho kitendawili kinaonenekana dhahiri, ni yale Mungu aliweza kumwambia Musa katika Kutoka 34: 5-8 . Alisema kwamba yeye ataweza kusamehe, na tena atapitisha dhambi ama makosa kwa uzazi ujao.

***Kwa nini atende yote mawili? Swali njema .*** Mungu ni mwenye haki, na hawezi akapuuza makosa na dhambi. Kwa hivyo ataipitisha kwa ukoo ujao na mwishowe iliweza kumfikia Yesu, kondoo aliye na ukamilifu, mwenye akiweza kuzivumilia dhambi zetu sisi wote. Akawa laana kwetu sisi,(Wagatia 3: 13)

***Laana  na baraka ziko chini ya sheria ya kupanda na kuvuna.*** Ikiwa babu yako aliweza kupanda dhambi ya hasira na gadhabu, wewe ama watoto wako wanaweza kuwa na hasira kuu , kuliko ile iliweza kutendwa na babu yako. Aliweza kupanda mbegu na ujue matunda yanakua kwa wingi kuliko mbegu. Ikiwa wewe hunywa pombe kidogo , usishituke ikiwa watoto wako ama uzao wako utapata balaa ya kuwa hunywa pombe bila kipimo. Tumeshinda udhaifu wa kiasili ambao babu zetu walikumbana nao . Ingawa hatujui chanzo

cha udhaifu huu, tunajua ya kwamba ulisukumiwa kwetu. Ilhali, kwa sababu ya kushinda kwetu, watoto wetu, na wajukuu wetu, hawatateswa na mambo haya. Kizazi hicho kimekwisha pita (Mathayo23:34) wakati Yesualisema (Mathayo 23:34), ninaamini yakuwa hakuwa anaongea tu juu ya mwisho wa dunia lakini alikuwa pia anagusia laana ya kizazi katika maisha yako binafsi. Katika (mathayo 24). Alikuwa anaogea kuhusu aina zote za mikasa ile imefanyika kama tangulizo ya laana zilizoshindwa . Hii ndiyo njia ya kushinda.

**Kukata tamaa na kukosa tumaini.**

***Katika kitabu chake " Blessing or Curse[13]", Derek Prince ameeleza matokeo mengine ya laana.***

> *Wewe pia inawezekana umeonja ufanisi , ni kweli unajua utamu wake lakini haukai ,gahfla pasipo na sababu yote unapoelezea unajikuta hujatosheka. Majonzi yanakushukia kama wingu, kazi yako yote inakuwa bure. Unatazama wengine wanaonekana kutosheka katika hali zile zile, Na unajiuliza " ni nini kilichoenda mrama na mimi?' kwa nini sipokei kule kutosheka halisi?*

***Kupigana na vivuli ni semi moja inatumika sana na Derek Prince.***

Maishani mwangu ninapokumbana na matokeo ya laana kama ni kutokana na matunda ya matendo yangu au kitu ambacho kilisukumiliwa chini kupitia vizazi kiwango cha kujistahi kwangu, kilikuwa nunge. Nilifanya kuhisi kana kwamba kulikuwa na jambo mbaya na mimi na na kashikwa na kukata tama na kukosa matumaini. Huu ulikuwa wakati ambao uhusiano wangu na Mungu ulikuwa wa karibu sana. Watu wanaweza kupokea mambo haya kwa njia tofauti. Wengine watazama chini ya uzito wa kukata tama na kufa moyo . Wengine wanajitahidi katika kazi zao na kutafuta kujenga kiburi chao kulingana na kazi zao. Sikukata tama lakini nilipokea pumziko katika

[13] Prince Derek Blessing or Curse Grand Rapinds, MI:vitabu vilivyo chaguliwa, 1990.

kushiriki na Bwana katika neno lake kila siku. Nakumbuka Bwana akinifunza wakati ule juu ya laana na baraka na juu yangu mwenyewe kasha Mungu akanipa kiburi changu ambacho kimejengwa katika kujiitanisha na yeye. Nikitazama nyuma naona kwamba uponyaji wa ndani , niliupata kabla ya laana, kushindwa na kabla ya hali zangu kuangazwa. Ningekuomba uwe mwadilifu na Mungu, uwache ukajue kama kuna hali kama hizi maishani mwako. Itakuwa ni mwanzo wa ukombozi wako. Ukweli utakuweka huru wakati wote.

**Yesu alikumbana na watu wengi waliokuwa wamefungwa na udhaifu ama mapepo ambayo yakionekana asili yake ni kutokana na vizazi.**

Katika (Marko 9:17-29) Yesuakakemea pepo kutoka kwa kijana ambaye alikuwa amepagawa na pepo kutoka utotoni. Wanafunzi hawangeweza kumukemea huyu pepo na baada ya Yesukufanya kazi hii, wakamuuliza kuhusu jambo hili.(Marko 9:29) *inasema:"Akawaambia, namna hii haiwezi kutoka kwa neno lolote, isipokuwa kwa kuomba."* Ni wazi kulikuwa na mambo yaliyo hitaji kushugulikia kando na hilo pepo kuwapo. Ni vyema kuona moyo wa Yesukatika kushughulikia vifungu vya kiroho. Vinavyo tokana na vizazi . Kwanza anataka tuwe huru kisha yeye ni mwenye enzi na wakati mwingi, yeye ndiye huanza. Pia yeye hutuponya bila kutuhukumu. Sisemi kuwa hatutakosa starehe ama Mungu hatatuletea mambo mazito na nidhanu ya hali ya juu, lakini yeye hatuhukumu, Roho Mtakatifu hudhibitisha kosa, na inastahili tumekomaa na uadilifu kutosha kumwachilia yeye afanye hivyo. Katika Yohana 9. Yesualipokuwa akitembea na wanafunzi wake akapatana na mmja alipokuwa kipofu kutoka kuzaliwa. Jee alijuaje yule alikuwa kipofu kutoka kuzaliwa? Nani anajua? Pengine lilikuwa neon la uzazi, labda Mungu alikuwa amemunenea kwa maombi usiku kucha. Huyu hakuwa anatafuta kupona, Yesualimtafuta kutoka kwa kikundi . '

( Yohana 9:2) *inasema: wanafunzi wake wakamuliza wakisema, rabi, ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu?* walidhania kuwa udhaifu huletwa na dhambi, pengine

dhambi za wazazi, pengine ya ndani ya kizazi kama vile Musa alitambua. Yesuakajibu lile swali kwa njia ambayo naamini " the Amplified Version inasema yasema vyema (John 9:3) *inasema: "Yesuakajibu, huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake bali kazi za Mungu zidhibitishwe ndani yake."* Ni wazi, wote wametenda dhambi hata huyu mtu na wazazi wake pia, jambo ni kwamba Yesualiona kusudi la juu katika udhaifu ule, na kuelewa kuwa kulenga na yule aliyesababisha, jambo hili kupitia dhambi zake halitaleta rehema hata ukombozi. Naamini Yesu alikuwa anafunza kuwa "taka yetu" ikiangaliwa na mtazamo a Mungu ilikuwa tu kama kitu ambacho kinaweza tengenezwa kuwa dhahabu. Hivyo ndivyo ilivyo na laana zetu za kizazi ninamini Yesu anafunga na kuomba na huja kwetu kwa nguvu zake, na anabadilisha laana zetu kuwa baraka.

Kile ninataka kushirikisha hapa kwanza ni uzazi wa mambo haya na pili jinsi ya kushirikiana na bidii ya Mungu ya kutukomboa.

**Lengo lako maishani huenda lisitimilike ikiwa laana hazitashughulikiwa.**

Miaka mingi iliyopita, nilikuwa katika matembezi na Bwana, Katika hisia zangu, ningependa kujipeena kabisa kwake na nikasema " Bwana andika kusudi lako katika moyo wangu kwa kalamu iliyotumbukizwa katika wino wa Roho Mtakatifu" . Nilitaka tu kile tu Mungu alitaka kwa maisha yangu, sio zaidi ya hiyo. Niliweza kuona kijikaratasi cha aina fulani ndani yangu naye Bwana akiandika mpango wake juu ya maisha yanyu (Mithali 7:2-3) *inasema: "Uzishike amri zangu ukaishi, na sheria yangu kama mboni ya jicho lako. 3 Zifunge katika vidole vyako, ziandike juu ya kibao cha moyo wako."*

Bwana akajibu "si lazima niandike" mpango wa maisha yako baada ya kuumbwa kwa dunia. Hiyo nguo mzito imeibiwa na mfano wake na imeandikwa kusudi lake juu, ina akafunika kusudi langu. Kile kinahitaji ni kuondoa huo mfano "Mungu alijua kwamba nimekutana na mchoraji, siku moja mwenye ataiba rangi maridadi kutoka kwa nyumba ya sanaamu, na sii kwa urmbo wa michoro, lakini ni kwa dhamana ya hiyo nguo mzito. Yeye angepaka rangi juu

ya hiyo halisi na hii ndiyo picha niliyoona. Ninaamini kwamba Mungu yuko na kusudi maridadi kwako wewe, hapa ulimwenguni, moja yenye itakutosheleza wewe, kuliko ndoto zako kuu, ndoto hujawahi ota, lakini zimefungiwa ndani yako wewe, (Waefeso 3:20)

Ninaamini pia mifano mingi imepakwa rangi, ina dhambi za hapo awali na sana sana laana za ukoo. Na ikichangia yale mambo ilifanyika kwako ukiwa mchanga, Na mambo yale yalitendeka kwa babu zako kabla yako wewe kuzaliwa. Naweza kukuambia mambo mawili yaliyotendeka maishani mwangu, kwanza Mungu amekuwa akinipeleka kwa kusudi langu , na bado anaendelea kuifanyia kazi. Pili, haijakuwa rahisi vile imechukuwa “ kushinda” kila hatua ya njia yoyote lakini hakuna kitu rahisi katika hii maisha , kwa hivyo kwa nini tusiende kupata “dhahabu”

***Tendo la kutupa ndilo linahitajika.***

Tendo la kutupa na inaaminika na kutumainika. Hii ni imani, na inavuta, kusudi la Mungu sana . Ikiwa wewe huishi maisha ya kujiachilia kabisa kwake Mungu, inaweza kuwa wewe utaishi maisha ya kujuta wakati utamuona Yesuuso kwa uso . Wakati utajiachilia wewe kwa imani yake Yesu, unamuweka yeye huru kuimarisha kusudi yake ndani ya maisha yake. Ni lazima uweze kutengenezea yeye nafasi ama atakosa kutenda. Na ninaamini kuwa Mungu anapoona ku changia kwako, ataanzxa safari yako juu ya maisha yako, kugeuza laana na kuwa baraka .

**Hapa kunayo maneno ya kweli kuhusu laana za kizazi zinazo tolewa katoka kwa kitabu “ Blessing or Curse”[14]**

(i)Adhabu ya dhambi ni laana. Nayo laana ya utengano wa milele ni chanzo cha laana ya utengano wa milele ni chanzo laana. Ikiwa hiyo imeshughulikiwa, kwa nini hizo ndogo dogo zisishughulikiwe? Ikiwa alifuta kifo, lazima afute laana yangu.

---

[14] Prince Derek Blessing or Curse Grand Rapinds, MI: Vitabu vilivyo chaguliwa, 1990.

(2)Laana ama baraka ni nguvu zisizo za kawaida kwa wema ama kwa ubaya. Kumbukumbu la Torati 28:21 inasema walijishikilia, mstari 29 unasema hakuna anayeokoa.

(3)Laana na baraka zaweza kupitishwa kupitia kizazi. Inaweza kuwa kwa familia, nchi, ukoo ama eneo Fulani.

(4)Laana zinaweza zalishwa kwa maneno ya kuongea, kuandika ama ndani ama na vitu.

(5)Laana ni kama mkono mrefu kutoka ya jao kupigana na kivuli.

(6)Msingi wa laana unasababishwa na kutosikia na kutii Mungu kumbukumbu la torati 28.

***Ishara zingine za laana.***

Siamini ya kwamba haya mambo yote kila mara ni lazima yawe yametokana na laana,lakini, wanatengeza kijikaratasi cha kwangalia. Tafadhali usiangalie haya yote mambo kama suluhisho la mwisho, ya kuonyesha ya kwamba kunayo laana inafanya kazi maishani mwako. Nimeona mambo mengi yakiwa ya kipekee. Na haya yote yametolewa kutoka kwa kitabu cha 'Blessing or Curse' na Derek Prince,kama imeelezewa hapa juu.

(1) Akili ama kuvunjika kwa sikitiko.
(2) Magonjwa ya kujirudia sana, sana ikiwa imeridhiwa.
(3) Utasa na laana kutoka kwa mama au shida zingine za akina mama.
(4)Kuvunjika kwa ndoa na kutengana mbali kwa familia.
(5)Shida ya kukosa pesa ambayo haiishi.
(6) Kuwa wazi kwa ajali za barabarani.
(7) Historia ya kujiua na vifo visivyokuwa vya kawaida.
(8) Uhalifu.
(9) Mambo ya kishetani.
(10)Kutofanikiwa na kushindwa kufaulu.
(11) Mambo ya mapenzi yasio kuwa na kipimo ama kiasi.
(12) Kutumia vitu vibaya kama pombe na madawa ya kulevya.
(13) Tabia za kula zisizo na kipimo.
(14) Na tabia zingine zinazofanywa kupita kiasi.

Ikiwa una hisi haya mambo ni kama yako na wewe, usione kana kwamba umehukumiwa, kuwa wa kushawishika tosha. Mimi nimeshakombolewa kutokana na laana nyinginezo. Shida zingine ni

eti watu wengi,hawataki kukubaliana na Mungu kuhusu hali zao, na kwa hivyo kukombolewa kwao kunakuwa ngumu zaidi karuhusu Yesuachukue laana zako na dhambi zako. Amefanya haya yote, sasa wewe weza kuyakubali. Kuwa muadilifu na yeye. Inaweza kuwa ni chungu, kuzuia huu ukweli, lakini utaishi kwenye kifungo.

***Mahali laana zinakotoka.***

Kumbukumbu la Torati 27:17 *inasema " na alaaniwe aondoaye mpaka wa jirani yake".* Kwa hivyo Mungu aliweza kutupa mipaka na wakati tunaondoa tunalaaniwa.

1. Miungu ya uongo Kutoka 20: 3-5
2. Kuabudu miungu mingine(Kumbukumbu la Torati 28: 27)
3. Kutotii wazazi –(Mithali 30:17)
4. Kusaliti – jirani (Mithali 17:13)
5. Kutokuwa na haki na wanyonge na maskini. (Mithali 28:27)
6. Mapenzi yasiyo ya kawaida zinaa ya maharimu (Mambo ya Walawii)
7. Kuto-tumika (Mwanzo 12)
8. Kutegea mwili sanan (yeremia 17;5-7)
9. Kuiba (Zech 5:1-4)
10. Kutopeana (Mal 3:8-10)
11. Kugeuza injili kamili (wagalitia 1:8-9)
12. Kuishi kwa sheria nasineema (wagaatia 13:10)
13. Kunena mambo ya kinyume (Mwanzo 27:11-13) (Mathayo 27:24-25)
14. Watumishi wa shetani, wengine wakikulaani kama Balamu ama Goliath (Hesabu 22:6,23: 11-13) (1 Sam 17:43)
15. (Deut 28:15) Ilhali Mungu antuamlisha "tuache hofu" Hofu ile imezaliwa kutokana na kutojua kwa upendo mkuu wake Mungu kwetu sisi,inaweza leta laana. Hofu inaweza kuwa Jambo la kuunganisha sisi na laana.

***Kupatana na kanuni za kuvunja laana*** (Mithali 26:2) *inasema: "kama shomoro katika kutanga-tanga kwake, na kama mbayuwayu katika kuruka kwake; kadhalika laana isiyo na sababu haimpigi mtu."*

Njia ya kufanya kila laana isiwe na tendo maishani mwako ni kushirikisha na kuipeleka kwake Yesu, ambaye alizivumilia laana zetu na kusikia na kulitii neno lake Mungu. Tunapo kosa hii, tunatubu dhambi zetu na tunakuja tena kwa kikao kioja na kutii ( 1Yohana 1:9).

***Kuondolewa kwa laana kulikuwa ahadi kwa wana wa Israeli***. Sisi kama kanisa tunvuna faida ya Agano Jipya mbele ya wakati waisreali wakawaida watawaopia wataingia kwa Agano Jipya kama ilivyo elezewa Yeremiah. Yeremiah akaelezea ahadi, ilhali mstari 29-30 unapeana picha kubwa ynye inakuuliza uweze kuiweka kwa akili na roho (Yeremia 31:29,30) *inasema:" siku zile hawatasema tena, baba za watu wamekula zabibu kali, na meno ya watoto wao yametiwa ganzi. 30 Bali kila mtu atakufa kwa sababu ya ouvu wake mwenyewe; kila mtu alaye zabibu kali, meno yake yatatiwa ganzi".*

Yesu ndiye alikuwa wakutimiiza hii ahadi (Wagalatia 3:13) *inasema: "Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana ameandikwa, Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti."*

**Yesu alichukua laana za Baraba na zako pia.**

Katika Mathayo 27:16 tunaambiwa kwamba Baraba alikuwa mfungwa mashuhuri. Kulikuwa na misalaba mitatu Golgotha. Ile misalaba miwili, kila upande, ilitengenezwa kwa ajili ya wahalifu. Na je, msalaba wa katikati ulitengenezwa kwa ajili ya nani? Kwa ajili ya Yesu?Hapana. Kwa ajili ya Baraba. Yesu alichukua nafasi ya Baraba. Isaya 53inatuambia ya kwamba Yesu alichukua nafasi Yetu.



Katika Isaya 53:4-6 tunaona kwamba Yesu alichukua yale tuliyopaswa kuyapata. Imeandikwa hivi: "Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu; lakini tulimdhania ya kuwa

amepigwa, amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote."

**Hatua za kuwa huru kutokana na laana;**

1. Kiri imani yako kwa kazi iliyo malizika hapo msalabani, kwamba Yesu aliweza kuchukuwa kila laana ile ingekuja kwako. Nauinue Yesu, kama vie wana wa Israeli walipoinua nyoka ya shaba. Jiweke sawa kuvuna matokeo yote ya dhambi, pengine yale ya babu zako, ama yako wewe mwenyewe pale msalabani.

2. Kiri kwa imani yako,kwamba yseu ndiye mwana wake Mungu, nay eye pekee ndiye njia yak wake Mungu, na kwamba alikufa msalabani na amefufuka tena

3. Kutubu ni jambo lilio na nguvu zaidi ya kushughulikia laana kutubu kutokana na uasi wowote na dhambi na kunyenyekea kwake Yesukama Mungu. Hii inaambatana na kutubu kwako wewe, binafsi na kushirikiana kwa kutubu kwa anjili ya familia yako ama mwenye amehusika kwa hii laana. Kwa watoto wetu, nilazima tutubu kwa anjili yao na kwa babu zao, wale wanaweza kuwa wamepitishwa hizi laana kwetu sisi.

***Tazama nyuma iliuone dhambi za babu zako na uweze kuwasamehe. Hatimaye weka matunda ya dhambi hizo pale msalabani wa Yesu aliyechukua matunda hayo.*** kaangalie wewe mwenyewe na uulize Mungu akusamehe wewe. Tena angalia mbele na uulize Mungu aweze kukusamehe watoto wenu na uombe kwa kuweka hizi laana za kizazi kwake Yesubadala ya hao. Kutubu kwa njia nii kuna nguvu zaidi. Bibi yangu ni mimi tunaweza shuhudia haya. Tumeweza kuona baraka zisizo za kawaida kupitia njia hii.

4. Weza kuuliza msamaha wa dhambi zako zote, na sana, sana dhambi zile ziliweza kukuweka wazi kwa laana. Uliza Mungu aweze kukufungua kutokana na matokeo ya dhambi za babu zako.

5. Wasamehe wote wale wamekukosea, ama kukutenda mambo mabaya.

6. Tangaza uhusiano wote kwa mambo ya kishetani mpaka vitu vile vina ziwakilisha

7. Weza kuweka tena kwa ile nafasi imebaki ; neno la Mungu. Mwuuliza Mungu akupe wewe neno lile litakuwa pale ndio likaweze kutangaza huru kutokana na hiyo laana. Tena tafakari kuhusu hilo neno, sema tena na tena na uendelee kuikili.

**Kushinda laana huja mara moja ama huchukuwa muda.**

Mara mingi huchukuwa muda, ndio ukaweze kuwa huru kabisa, na kwanza kufunguliwa kutokana na madhara ya laana. Kwa wengine huwa mara koja tu, lakini kwa wengine kama mimi iliweza kuchukuwa muda mrefu. Sikuweka na weka Mungu kwa chupa ndio aweze kuwa na formula, yeyey anaweza fanya kazi yake jinsi apendavyo. Najaribu tu kukueleza vile ama yale mimi niliweza kupitia na vile imekuwa sababu neno lake Mungu. Tumeona ushindi na uwezo wa kushinda wakati tunapoishi na mtindo wa kuweza kushinda kama nilivyo eleza (Ufunuo wa Yohana 12:11) inasema: Nao wakamshinda kwa damu ya mwana-kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao, ambao hawakupenda maisha yao hata kufa. Tumeweza kuona dhihirisho za haraka kwa hii njia ya uponyo na ukombozi na wakati tunapotambua shida na kuweza kukiri dhambi zetu na kuweza kuzitibu. Kazi yetu kubwani kuweza kuwa waadalifu na kutubu. Mungu akona mipango, ile ilyo kamili na sawa kwa maisha yetu.

Mara kwa mara maishani mwetu, tumetumia miezi na hata miaka tukiwa na uwezo wa kushida laana, tukiamini neno lake Mungu, hata ingawa hisia zetu zilikuwa na mapigo makali sana, kwetu sisi. Tumegundua ya kwamba mara mingi, tukiweza kushinda mashetani yameweza kuzalishwa na laana, na kuzituma kwenye kushindwa kwa milele. Hata hivyo hatukuwahi, kata tamaa! Mungu alijua ni yapi alikuwa anatenda.

***Vuta Nyororo iliyouzunguka mti.***

Nilisimsikia mtu mmoja kutoka huduma ya Derek Prince akieleza jinsi aliweza kusimama hii hali kimaajabu sana. Alitumia usawa wa tabia ya ‘giant Red wood Tree’. Wakati mwingine ukweli ni kuwa

hawangeweza kuona chini badala yake wangejifunga na nyororo kwa mzunguko wa huo mti mkubwa na kukaza kwa mtambo wa kuvutia kamba ya nanga. Kial mara wanakuja na kukaza kamaba kadhaa. Mti umeshakufa wakati hay yanayotendeka, na bado huwa na majani mengi sana. Kila mara mingi wafanyikazi huja na kukaza hiyo nyororo tena na tena mpaka dhihirisho ya kifo kinakuwa wazi wakati tunapokutana na hali zilizotajwa hapo juu, laana yetu inakuwa imeshakufa, lakini kamba kwa kuishi mtindo wa maisha ya ushindi.

Hivo ndivyo tutakuwa tukifanya atunapo jiweka sisi kuwa huru kutokana na laana ndani ya maisha yetu. Sasa tumefungwa ukanda chini ya nyororo. Na sasa kwa urahisi tunaweza kaza kamba kwa kuishi mtindo wa maisha ya ushindi. Kumbuka kuweka shamba lako safi ama Kama maneno mengine (Waefeso 4:1) kaa kando na mng'ang'ano na uishi maisha ya upendo na kusamehe.

**Maombi lililopendekezwa.**

***Kutoka kwa neno;*** Bwana YesuKristo, naamini kwamba pale msalabani. Ulichukuwa kila laana, ile ingekuja kwanGu! Imani kwa Kristo: wewe ni mwana wake Mungu, njia iliyo ya pekee kwake Baba Mungu ulikufa msalabani na kafufuka.

***Kutubu:*** Nakupa uasi wangu wote na dhambi nakupatia yote kama Mungu na mtawala.

***Omba msamaha:*** Ninatubu dhambi zangu zote na kuuliza msamaha kutoka kwako, sanasana kwa dhambi zilizo nifunua kwa laana na kunipatia mimi kutokana na matokeo ya dhambi za babu zangu

***Samehe:*** kukata kauli ya hali yangu na wasamehe wale wote walionitenda vibaya na kutia uchungu kwangu kama vile ningetaka Mungu asamehe mimi.

***Kataa:*** Na kataa shirikisho na kitu chochote cha kishetani.

Ikiwa nilijihusisha na chombo. Najipeana mimi kuziharibu zote. Nakosa maneno yote ya kishetani. Kinyume na mimi (tazama ukurasa 68-71) ya <u>Blessing of curse: You can Choose,</u> orodha ya dini za ushushi/ mafundisho ya siri. Pia tazama alama tano za siri katia

kurasa 121-124 za kitabu They Shall Expel Demons[15] kwa"Mtawafukuza mapepo ya Ishara za dini)

***Achilia:*** nauliza wewe uweze kuniaachilia mimi kutokana na kila laana juu ya maisha yangu. Katika jina la Yesuna jiachilia mimi mwenyewe.

**Sasa Pokea Kubadilisha.**

| **Baraka** | **Laana** |
|---|---|
| Kuinuliwa | Aibu |
| Kuza | Utasa |
| Afya | Magojwa ya kila aina |
| Ufanisi | Umaskini na kutofaulu |
| Ushindi | Kushindwa |
| Utawala (Kichwa) | Kushindwa (Mkia) |
| Kuwa Juu (Uwezo) | Kuwa Chini (udhaifu) |

**Hapa kuna jambo la kumbuka. Suluhisho la Mungu kwetu ni kuona na kuamini.**

kuna ukweli wa kiroho na ulimwengu usio onekana umetuzunguka lakini sisi hatuwezi kuona na macho yetu ya kawaida. Ni kuimarisha kila kitu kile tunaweza ona kwa haya macho yetu. Paulo akoamba katika kanisa la waefeso kuwa watu wangepata macho iliwaweze kuona ulimwengu wa kiroho. Waefeso 1:17-18 inasema: "Mungu wa bwana wetu YesuKristo, baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yeye 18 Macho ya mioyo yenu yatiwe nuru mjue tumaini la mwito wake jinsi ulivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo." Wakati tutakapoona ukweli ulio katika ulimwengu wa kiroho tutajua ukweli nao ukweli utatuweka huru.Yohana sura ya 8.

Ombi la Paulo lilikuwa watu waweze, kuona utajiri wa utukufu na ndio uridhi wetu. Utukufu ni nini? (Wakolosai 1:27) Utukufu, baraka

[15] Prince, Derek. They Sahh Overcome Demons. Grand Rapinds, MI:: Vitabu vilivyochaguliwa 1998

ni Kristo aliye ndani wewe mtu wa kale ako chini ya laana, amesulubishwa naye Kristo Wagalatia 2:20 inasema:” Nimesulubiwa pamoja na krist; lakini ni hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake ajili yangu.”Ilhali yule mtu ambaye, sasa Kristo aliye ndani anaishi najua hivi Kristo akiwa ndani yako hawezi kuwa chini ya laana.

***Ni lazima tuone mema na baya.***

Kwanza ni kuona vizuri, kwamba wewe ulizaliwa na Kristo aliyefufuka, yule sasa anaishi ndani yako, na yeye hawezi kuwa chini ya laana. Kristo yeye si mfano to wa kuishi, yeye si mtu tu aliye mbinguni anakusaidia wewe, lakini yeye amesha kuwa badilisho, yako. Yeye akiishi maisha yake ndani yako, badala yako wewe kusihi maisha yako ya kale.

Mungu katika rehema zake atakusaidia kujiona wewe mwenyewe. Utakapo kaa karibu na kutumia wakati mwingi naye kwa maombi na neno na Roho Mtakatifu ata dhibitisha kwake ngome tabia na hali yako, yale si yake Kristo. Tumia hizi sababu ikiwa Yesu(Kristo) anaishi ndani yangu, tena ni nini hii iko ndani yangu ambayo haifanani na Kristo? Hii dhibitisho ni zawadi ya kutubu kwake Mungu unapojihisi na kusikia uchungu, hasira, wivu, uovu hayo yote, mara tu ilete kwake kama dhambi: uliza Mungu awae kukuonyesha wapi haya yalitokea/ Fungua milango yote ya roho yako na uweze kumwambia Mungu aingie katika hizo milango zilikuwa zimefungwa maishani mwako. Ni yeye tu anaweza kuziponya Danieli hakuweza kudhulumiwa na simba, alipotupwa katika tundu la samba, kwa sababu, kama vile maandiko yanasema, huku wanahatia mbele zake Mungu,na kwa Kihibriania neno Innocent linamaanisha kuwa wazi-Daniel 6:21.

Kwa miaka iliyopita, baada ya mimi kujua kuhusu laana na baraka, Mungu alikuwa ananifunga kutokana na laana kupitia urahisi uadilifu na uwazi ulikuwa ndani yangu nilikuwa na soma neno kama kioo. Kuacha na nina ruhusu iweze kusoma mimi. Tena ningekiri mambo yote iliyo ndani yangu, yale haya kuwa yanakaa kama Yesu. Hii ndio tunafaa kufanya ndio tuwe huru.

***Ukweli kwamba laana zinajaribu kukushinda zimejengwa juu ya uongo!***

Ikiwa Yesu anaishi ndani yangu sasa hii jambo la laana kukudhuru wewe iliyo suluhishwa kisheria. Ilhali ni lazima wewe uweze. Kupokea ukweli kwa kuona nini kinatendeka katika ulimwengu wa kiroho na kudhibitisha ukweli wa yale unayo yaona. Hii ndio njia pekee ya kuweza kufaulu, kwa sababu laana zingine hazitoki siku inayofuata. Ng'ombe zingine za mapepo haziwezi kuenda kama mbwa aliyenauoga ni lazima ichukue uvumilivu na muda mwingi kudhibitisha na kushuhudia ukweli na msalaba. Na wakati huo tu ni lazima uwe unaishi maisha matakatifu, kwa maneno mengine uadalifu wa maisha, ndio ushuhuda wako uwe umekamilika na Mungu na shetani pia anaweza chukua muda kwa mawazo yako kufanywa upya ama tabia zako kuwa zimebadilika lakini unapoendelea kuona na hata kuamini wewe unapata ushindi.

Kuona ni uridhi uliopewa wewe na Mungu kama mtoto wake 1 wakorintho 2:9,10 inasema:" Mungu ni mwaminifu ambaye mliitwa na ye mwingie katika ushirika wa mwanawe, YesuKristo bwana wetu. 10 Basi ndugu, nawasihi, kwa jina la bwana wetu YesuKristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja."

**Kumbuka mambo ambayo tumetaja hapo awali kuhusu laana.**

nafasi ya kutueneza. Ukihukumu kwa haki sheria ya kupanda na kuvuna ita lete hukumu ya haki kwako kama dhawabu.

***Rafiki yangu aliniiambia hadithi ya mavuno mabaya ya hukumu aliyeshuhudia.***

Kulikuwa na mvulana aliyekuwa na mazoea ya kucheka na kudhihaki watu waliokuwa wanene zaidi alliwapa wakati mgumu sana.  Akapatwa na shida ya kikoromeo na kunenepa sana akawa kitumbo bila hata kujaribu.

Nimeshuhudia mimi mwenyewe wau kanisani wakihukumu na kulaani watu wenye wametalakiwa.  Hawa kuwa na habari kana kwamba ilie taraka ilikuwa kuli ngana na maandiko au la ama jambo lolote ilivyo tokea, waliuchukua msimamo wakifarisayo. Tumeshuhudia wengi wa hawa wakipata talaka maisha yao ama maishani ya wana wao.

**Nadhiri**

Nadhiri sana sana huwa zinafanywa na hukumu, tunavyofanya kinyume na wengine. Nadhiri tunavyofanya huwa zinafuatwa na hukumu.  Hukumu huwa ina bomoa lakini na kuzusha chini wengine lakini nadhiri huwa inanijenga. Hukumu husema angalia wao, na nadhiri nayo na mimi je? Tuna weka nadhiri ilituweze kujisikia vizuri, kuhusu sisi wenyewe. Nadhiri ni ya kudumu kwa kawaida na kwa hivyo haiku kwa utawala wetu, wakati tunapomaliza kuweka nadhiri kwa mfano, unapo hukumu baba yako kuwa mwepesi  kutoa makosa, unaweza toa nadhiri wewe hutawaki kuwa hivyo. Lakini kwa sababu tunavuna yale tumepanda mwishowe tunajipata tukiwa hivyo kama baba.  Wakati mwingine inachukua muda, kama miaka ilikuweza kudhirika yenyewe ndani ya maisha yetu, lakini mwishowe huja kuwa ngome iliyo na nguvu. Mpaka tuivunje ile hukumu na kuikanusha nadhiri katika Jina lake Yesu. Hali mbay a yetu ya mambo mingi huwa inatokana na zile nadhiri tulitoa wakati tulikuwa tukihukumu watu wale wengine.

Tutakapo wacha kuhukumu watu wengine haimanishi yale watu wengine wamefanya ni mazuri lakini hii huwa inatakaweka huru kutokana na kamba zile zimetufunga sisi, kwa sababu ya hukumu zetu

na nadhiri za ndani. Hukumu na nadhiri iliyo haribifu sana na inayotoa ni ile iko kinyume na wazazi wetu.

(Kumbukumbu la Torati 5:16) inasema: "waheshimu baba yako na mama yako; kama bwana, Mungu wako alivyokuamuru, siku zako zipate kuzidi, nawe upate kufanikiwa katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako." Kuheshimu inamaanisha kutii, kufanya bidii ili kuweza kupeana heshima, inaamanisha kupenda, kudhamini na hata kusamehe. Wakati mwingine wazazi wametukosea sana. Lakini Mungu anasema tuitoe kwa moyo. Tunapo hukumu wazazi wetu na moyo uko na uchungu, hatuwapei heshima hata kidogo. Sheria ya Mungu kuhusu nadhiri italeta matokeo na maisha haitakwenda vyema na sisi. Tunaweza kuwa kabis kinyume cha yale yote tunayo hukumu kwa kushikilia kila kiwango tumeweza kueneza na kutosheresha kila nadhiri tuwewahi weka na kwa matokeo tunajikuta tumekuwa kabisa wenye haki. Wakujitegemea na tumefungwa kutenda jambo. Ama tunakuwa kabisa kama lile tuliweza kuhukumu lakini tukiweza haribu kila kiwango tumeweza kueneza na kuvunja kila nadhiri tumefanya na kwa matukio tunakuwa watu wakujihukumu na kufungwa na aibu.

(Mathayo 5:33-37) inasema:"Tena mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, Usiape uongo, ila mtimizie bwana nyapo zako. 34 lakini mimi nawaambia, Usiape kabisa; hata kwa mbingu, kwa maana ndicho kiti cha enzi cha Mungu 35 Wala usiape kwa kichwa chako, maana ndio mji wa mfalme mkuu. 36 wala usiape kwa kichwa chako, maana huwezi kufanya unywele mmoja kuwa mweupe au mweusi.37 bali maneno yenu yawe ndiyo, ndiyo; siyo, siyo kwa kuwa yazidi hayo yatoka kwa yule mwovu."

Wakati mtu anapotoa nadhiri, wanakuwa wanategemea nguvu zao hao wenyewe ili kuweza kuitimiza. Hii inaleta laana (Yeremia 17:5) *inasema*: "Bwana asema hivi, amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake na moyoni mwake amemwacha Bwana."

Unapotoa nadhiri kwake Mungu unweza kuwa unajaribu kulipa neema yake Mungu na huwezi kulipa neema yake Mungu. Ukiweka nadhiri kwa kusema nitawahi, hutawahi tenda jambo fulani. Ama useme, nitakuwa kila wakati nikifanya jambo fulani. Utakuwa

umefungwa na hiyo nadhiri kwa sababu ya matukio yaliyo katika nadhiri ni hukumu na iko chini ya sheria ya kupanda na kuvuna.

**(Wakolosai 2:20-23)**: *Kimsingi nilishughulikia kazi za kidini na mwili, hii hutupa sisi mfano vile ni bure kuamini mwili wako na nadhiri (colosians 2:20-23) inasema: "Basi ikiwa mlikufa pamoja na Kristo mkayaacha yale mafundisho ya awali ya ulimwengu, kwa nini kujitia chini ya amri,kama wenye kuishi duniani. 21 Msishike, msionje, msiguse 22(mambo hayo yote huharibika wakati wa kutukiwa); hali mkifuata maagizo na mafundisho ya wanadamu?23 Mambo hayo yanaonekana kana kwamba yaana hekima, katika namna ya ibada mliyojitungia wenyewe, na katika kunyenyekea, na katika kuutawala mwili kwa ukali; lakini hayafai kitu kwa kuzizuia tama za mwili."*

**Unawezaje kuajibika bila hii nadhiri?"**

Nadhiri za ndoa na nadhiri zingine zimekubaliwa naye Mungu ni njia za uzima lakina hata kama nilazima tuziweke,zinategemea neema yake Mungu na nguvu zake nasi kwa uweza au nguvu zetu.

***Suluhisho kwa dhambi za hukumu na nadhiri.***

Kaa kabisa ukiwa mwepesi kwa Roho Mtakatifu na uweze kuuliza yeye akudhuhirishie kila hukumu za kinyume unaweza kuwa nazo ama umeweza kujaribiwa nazo uliza msamaha na utumbu kutokana nazo fanya kama hivyo kwa nadhiri zingine umetoa hapo awali kaweze kufuatilia sana kwa akili zako na hisia zako kwa zile hukumu zinaweza kuwa zikikujia.

**Nukuu kutoka <u>'Inner Healing' na Dunklin</u>.**[i]

*Ile hukumu tumepanda kinyume na mwingine tunapokea kutoka kwa wengine. Tukijua hii ni lazima tutamani kuwa tunapanda upendo na huruama popote sisi tuendapo tukijua ya kwamba tutavuna upendo na huruma kwetu sisi. Chochote tunapo atamia ndani ya nafsi zetu huumbika kwa hali zetu. Chochote tunaweza andika kutoka kwa nafsi zetu kw awengine, inapokelewa na nafsi zao na tena intumwa kwetu sii kwa hii sababu, tunastahili kuweka nafsi zetu zikiwa ndani ya upendo wa kiungu (*

*warumi 8:33) inasema: Ni nani atakayewashitaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye kuwahesabia haki.*

**Ndondoo kutoka <u>“The Cross of Christ,”</u> June 22.**

*Sheria isiyo badili ya hukumu (mathayo 7:2) inasema: “Kwa maana mwanamke aliye na mume amefungwa na sheria kwa yule mume wakati anapo kuwa yu hai; bali akifa yule mume, amefunguliwa ile sheria ya mume.” Huu usemi ama maandiko si ya kibahati lakini ni sheria ya Mungu ya milele. Hukumu yeyote utakayo toa itakuwa kabisa kile uta hukumiwa nayo. Kuna tofauti kubwa sana kutokana na kulipisha kisasi na adhabu Yesualisema. Junsi ya maisha ni adhabu “kwa kile kiwango unatupia wengine, itatumia pia kwako wewe”. Ikiwa umekuwa mwenye busara kutafuta makosa yaw engine, kumbuka hiyo tu itatumiwa kwako wewe. Vile unalipa ndiyo njia ya vile unavyoishi na utalipa tena. Hii sheria yake Mungu infanya kazi kwa ufalme wake na hata kwetu sisi (Zaburi 18:25-26) (Warumu 2:1) inaeleza vyema sana kwa kusema yule anaye mchambua mwingine ana hatia la jambo lilo hilo. Mungu haangali jambo hilI tu,lakini hata kwa uwezo wa kutenda hilo jambo lile anaona akisha angalia ndani ya moyo.*

La muhimu kuanza njia ya kuvunja hukumu na nadhiri na mizizi ya hukumu tumetoa kinyume na wazazi wetu. Hii imeweza kudhuru maisha yetu kuliko hukumu tumewahi toa. Ombo na uweze kuuliza Roho Mtakatifu akuonyeshe hukumu, na nadhiri amabazo umekutia kinyume na wazazi wako. Tena weza kurudia haya maombi na kuvunja nguvu zilizoko maishani mwetu.

**Ombi la kuvunja hukumu:**

**Na hukumu kwa _______________. Ninavunja hiyo hukumu katika jina la Yesu.**

**Niliweka nadhiri kwamba ___________. Naivunja hiyo nadhiri katika jina la Yesu.**

# Sura ya 8
# Vifungo Vya Nafsi

Njia nyingine ya kukaa ndani Utumwa.

Vifungo vya nafsi[16] hufanyika wakati wawili ama zaidi kuliko wawili wanakuwa wameshikana pamoja. Vifungo vya nafsi vinaweza kuwa nzuri ama baya,pengine takatifu ama imenajisiwa. Mungu ameweka idhini vifungo vya nafsi kupitia kwa kufunganishwa kwa watoto na wazazi, bibi na bwana marafiki na marafiki waKristo na waKristo . Vifungo vya nafsi vimekubalika na Mungu ilivitoe mfano wa fungo ya watu pamoja na fungo la upendo wake Mungu (agape). Vifungo vya nafsi vilimaanisha kuleta daraja ya upendo wa agape. Ile Mungu alikusudia kwa mema, iligeuzwa kuwa baya. Vifungo vibaya vya nafsi ni daraja ya kuleta mabaya maishani mwako. Kuna viwango tofauti katika vifungo vya nafsi. Ile ina nguvu sana kama kimapenzi, ndoa na familia. Vifungo hivi hufanya wahusika wawe wazi kwa laana na baraka kwa yule mwingine. Kwa mfano kijana wa miaka kumi na sita akifanya mapenzi na Malaya, yeye huyo kijana ameshawekwa wazi kwa laana za huyo kahaba, basi kahaba huyo pekee yake lakini kwa wale wazee wote huyo kahaba amelala nao, ama wamefanya mapenzi na Kahaba na huyu kijana, wanakuwa na vifungo vya nafsi na watu maelfu ama mamilioni na tena kuwa wazi kwa laana zao zote. Tena kunazo vifungo vya nafsi ambazo hazina nguvu sana kama vifungo vya kiurafiki natutaelezea katika somo hili.Vifungo vizuri vya nafsi vinamaanisha kueneza kupitia uhusiano kati ya wazazi na watoto. Kama mtoto aliye na uzima hukua, anaweza anzisha, vifungo vya nafsi ya uzima na watu wachache walio wa karibu. Baadaye anakuwa tayari kuanzisha kifungo cha nafsi cha karibu sana kupitia ndoa baada ya ndoa sasa wawili wanaweza anzinsha vifungo vya nafsi na wa Kristo wengine.

## Kifungo cha nafsi ya ndoa

[16] Mambo mengi katika sura hii yametolewa katika kitabu Inner Healings, Session Eight Judgements and Soula Ties, ambayo imetumiwa kwa idhini. Haki miliki * 1992 na Dunklin Memoral Church – kwa idhini ya ISOB.

Waefeso 5:31 inasema, “Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili moja”. Bibi na bwana wanafungwa pamoja kwa upendo.

“Hata wamekuwa si wawili tena ,bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwadamu asiwatenganishe.” (Mathayo 19:6) ubora wa ndoa ni yule Mungu amefunganishwa bwana na bibi. Ikiwa Mungu ame unganisha mume na mke, na sasa sana masikitiko, na huzuni ina patikana, ikileta matokeo ya majeraha vya ndani. Hata kwa ndoa ile Mungu hakuanzisha wawili huwa na vifungo vya nafsi na nilazima zivunjwe, majeraha vya kukaatiliwa na kujidharao ni dhahiri.

**Vifungo vya mzazi na mtoto**

Wakati kifungo cha nafsi hakijaanzishwa kati ya mzazi na mtoto, mtoto sana sana yeye huishi kwa maisha yake yote akijaribu kufunganisha kile kifungo kimekosekana. Kupitia kutafuta, mtoto huwa wazi kwa kupata vifungo vya nafsi zingine na sana sana huwa mbaya.

Familia ya akina Yusufu walikuja Misri kutafuta chakula kwa kukosa chakula pale walimoishi. Huu ndio wakati Yusufu alikuwa kiongozi huko misiri. Aliweza kusalimia ndugu zake akiwa ameficha kujulikana kwake. Mipango yake ilikuwa kufanya ujanja kwa ndugu zao ili aweze kuweka kikombo cha dhamana kwa kifurushi cha Benjamin na ili amshike kwa kuiba, ndio aweze kuleta Benjamin kurudi Misri na ndio babayao aweze kuja hata yeye. Kile kilitendeka Juda aliomba Yusufu yule alikuwa fumbo kwao, aweze kuruhusu Benjamin arudi. Juda alimwelezea shida yake akitaja babake Yakobo alikuwa na kifungo cha nafsi na Benjamin na tukivunja hii tunaweza sababisha kifo cha babake Benjamin.

Mwanzo 44:30-31 inasema, “Basi nikienda kwa mtumwa wako, baba yangu, na huyu kijana hayupo pamoja nasi, iwapo roho yake imeshikana na roho ya kijana, itakuwa atakopoona ya kwamba huyu kijana hayuko, atakufa; na watumwa wako watashusha mvi za mtumwa wako, baba yetu, kwa huzuni kaburini ”

Wakati mtoto anapozaliwa, akiwa mchanga ni ya muhimu aweze kufunganishwa wazazi wake kifungo cha nafsi kilicho na uzima ni vizuri kiweze kuwa kwa kuhudumu ya upendo na usalama,kwa huyo mtoto maisha yake yote. Hizi vifungo vya nafsi hutumika kama kuweza kudhibitisha kuhusu huyo mtoto ama ubinafsi wa huo mtoto. Ilhali kunayo mambo mengine pale mzazi hataki kuachilia hizo vifungo mtoto akisha otewa, na ni ya muhimu mtoto aingie kwa ndoa na sasa hicho kifungo kinafaa kuachiliwa. Nimeona wazee wakongwe sana na bado wanatawaliwa na mama zao na hii inaleta kutokomaa kwa ndoa, ndani ya uhusiano wa kiungu.

**Vifungo vya nafsi vya urafiki**

Vifungo vya nafsi vya urafiki vinaweza kuwa baraka ikiwa kati ya wawili ni wa kiungu. Hata kama hii haina nguvu, kwa vifungo vya nafsi zote siza kiroho zingine na haina mfereji wa laana.

***Yonathani Na Daudi***

1 sam18:1 inasema, “Ikawa Daudi alipokwisha kusema na Sauli, roho ya Yothani, ikaambatana na roho ya Daudi, Yonathani akampenda kama roho yake mwenyewe.”

Hii aina nyingine ya vifungo vya nafsi, na ni sawa na imejengwa juu a upendo. “Ajifanyiaye rafiki wengi ni kwa uangamivu wake mwenyewe; Lakini yuko rafiki ambatanaye na mtu kuliko ndugu.” (Mithali 18:24). Huu ni upendo wa kipekee unaofanyika kwa marafiki wawili wamejitoa.

**Vifungo vya nafsi vya Wakristo**

Waefeso 4:16 inasema, “..... katika yeye mwili wote ukiunganishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo.” Uhusiano baina ya waKristo unalingaishwa na uhusiano kati ya viuongo mbali mbali vya mwili. Vifungo vya nafsi huwezesha mwili wa Kristo kukomaa na kutekeleza mwito wake.

Vifungo vya nafsi vya urafiki na waKristo hazina matukio mabaya juu ya mmoja kama hizi zingine. Ilhali maandiko yanatuonya

kuhusu kuwa na uhusiano wa karibu na watu wako na mienendo isiyo mizuri, inaweza kuharibu mitindo yetu ama mienendo yetu.

**Vifungo vya nafsi vya uhusiano mbaya**

1 Wakorintho 15:33 inasema, "Msidanganyike; Mazungumzo mabaya huharibu tabia njema" Mithali 22:24-25 inasema, "Usifanye urafiki na mtu mwenye hasira nyingi; Wala usiende na mtu wa ghadhabu nyingi."

Vifungo vya nafsi vya uhusiano mbaya itatega mtu, yule amekuwa ametatanisha kwa nguvu za uovu. Marafiki wetu hututawala sisi, na sasa ni ya muhimu kuchagua marafiki wema.

**Vifungo vya nafsi vya mapepo.**

"Au hamjui ya kuwa yeye aliyeungwa na kahaba ni mwili mmoja naye? Maana asema, Wale wawili watakuwa mwili mmoja." (1Wakorintho 6:16)

Vifungo vya nafsi vya pepo hufuatishwa umbo la vifungo vya nafsi vya meme na matakatifu yale yamepatikana katika upendo. Vifungo vya nafsi njema vinapatikana kutokana na upendo. Vifungo vya nafsi vya pepo vinapatikana na kutoka kwa tamaa nyingi. Kwa mfano, uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa, huleta vifungo vya pepo kupitia kuzini, usherati, kifungo kibaya kinaumbika ndani ya tamaa za mwili. Hivi vifungo vya nafsi huharibu uhusiano mtakatifu uliojengwa kwa upendo na uaminifu. Warumi 1:26-27 inasema, "Hivyo Mungu aliwaacha wafuate tamaa zao za aibu hata wanawake wakabadili matumizi ya asili,Wanaume nao vivyo hivyo waliyaacha matumizi ya mke ya asili, wakawakiana tamaa, wanaume wakiyatenda yasiyopasa, wakapata nafsini mwao malipo ya upotevu wao yaliyo haki yao."

Vifungo vya ukaidi vina umbika kati ya wawili wa hali ya maumbile moja. Kufanya mapenzi na mtu wa jinsia moja. Mambo ya ngono inaitwa moto na tama za mwili, ile wanaweza ita hao wapenzi. Tena kifungo cha ukaidi hueneza hao wenyewe, kwa lile umbo la kati ya mtu na mnyama. Maelezo ya huu ukaidi wa kinyama kulala wazi wazi na wanyama. Vifungo vingine na wanyama huwa ni kuu kuliko kinyama. Inapewa tabia isiyo na kipimo na wanyama.

**Vifungo vya familia vya kupotosha:**
Yesu mara mingi ameongea kuhusu hatari za kujifunganisha na familia yako. Kidunia, vifungo vya familia ni ya faida na tena sana na baraka Ihali ukijaribu kuishi maisha yako na Yesuna familia yako sio, wanaweza kuwa na adhari juu maisha yako ama juu ya uungu wako, hata kukufanya wewe uweze kurudi nyuma na kukataa Mungu.

Luka 14:26 inasema, “kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake na mke wake, na mwanawe, na ndugu zake waume wa wake; naam na hata nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.”

Kifungo cha uhusiano baina ya mzazi na mwanaye ni cha uzima na faida, isipokuwa wakati anaendelea kuingia mtu mzima. Wakati mtoto wa kiume ama kike anafikia umri wa kuolewa, kifungo cha mzazi ni lazima kiondolewe ndio kifungo cha ndoa kiweze kuumbika.

Wakati baba anapopatiana bintiye aolewe, yeye hutenga kifungo cha nafsi kulingana na aina ya mume wa bintiye. Wakati hicho kifungo hakijatengwa kati ya mzazi na mtoto wakati unaofaa, ile iliyokuwa njema na ya muhimu huwa baya kupitia kutawaliwa na kujishikilia. Ukaidi wa kimapenzi ndani ya uhusiano na kifamilia, huja wakati kuna zinaa ya maharimu baina ya baba na bintiye, mama na mwana wa kiume, dada/kaka baba mkwe/bibi mtoto wake mamamkwe/mme wa bintiye ama wengine wakaribu katika familia. Wakati uunganishi wa muhimu unakosekana baina ya mtoto na mzazi huyo, mtoto akiwa hana pumziko na kutafuta maishani mwake. Shetani anaweza kwa urahisi chukuwa huyo mtu na kumuingiza kwa vifungo vya ukaidi.

“Wakaja mpaka sakafu ya Atadi, iliyo ng’ambo ya Yordani. Wakaomboleza huko maombolezo makuu, mazito sana. Akafanya matanaga ya babaye siku kumi.” (Mwanzo 50:10)

Kumbukumbu la Torati 34:8, “Wana wa Israeli wakamwombolezea Musa katika uwanda wa Moabu siku thelathini; basi siku za maombolezo ya matanga ya Musa zikaisha.”

Wakati mtu mmoja wa familia ama rafiki wa karibu hufa, vifungo vya nafsi vilivyoweza kuumbika kwa huyu mtu ni lazima vife, ama vitoweke wakati ama kipindi cha kuhuzunika kufuatia kifo cha

mpendwa. Ni moja ya yale yanatokea kwa sababu ya kukazwa kwa vifungo vya nafsi Wakati vinavyoisha. Hii inaitwa roho ya huzuni, masikitiko, upweke na nyingine kuingia.

**Kuvunja vifungo vya nafsi vya mapepo:**

Kama vifungo vya nafsi mbaya vinatambuliwa, nguvu zao ni lazima ziwe zimegeuzwa kukubali kwetu, kuwa waaminifu kunategemea uponyo ule tutapokea

*2 Wakorintho 6:17 inasema, "Kwa hiyo, Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha."*

*2 Wakorintho 6:18 inasema, "Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike. Asema Bwana Mwenyezi."*

Mathayo 16:19 inasema, "Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lolote utakalolifungu a duniani litakuwa limefunguliwa mbinguni."

Haijalishi kiwango gani cha dhambi, sisi tumejiunganisha kupitia damu yake YesuKristo kuweza kukataa kutubu na kufungua hizi nguvu mbaya kutokana na nafsi zetu,ndio tuweze kuwa huru na kujazwa na Roho Mtakatifu.

**Dokeza la maombi**

1. Kuwa unaongozwa na Roho Mtakatifu kupitia maombi kwamba Mungu atakusadia wewe kukumbuka wote wale umekuwa nao katika uhusiano wa kimapenzi nao. Uliza Mungu kama kunayo nafasi nyingine uliweza kuwa na mapenzi siku zako za utotoni, kwamba ulikuwa mdogo sana kuweza kukumbuka.
2. Hii ni vita kali ya kiroho na kwa hivyo hatuhitaji kufanya jambo hili peke yetu. Tunastahili kutafuta MKristo aliye komaa yule tunaye mwamini kutuongoza kupitia haya maombi. Hii huwa inajenga kifungo cha nafsi cha uzima.

3. Tubu kwa dhambi uliyofanya kinyume na Mungu ni muhimu. Amri zake Mungu zile zimevunjwa. Tamaa za mwili zimetuchukua mbali na mipaka ya usafi ule Mungu ameshatuwekea. Hata kama dhambi imetendwa kwa kutojua inastahili msamaha. Uliza Mungu akusamehe kwa kila kifungo cha ukaidi kimeumbika ndani yako.

4. Haribu nyumba ya shetani kwa kuchukua yale yote ameweza kupata kinyume na wewe. Kiri mbele zake Mungu. Shetani hana mamlaka kisheria kukuweza. Tangaza kila kifungo cha mapepo, na kile umetambua weza kuivunja katika jina la YesuKristo

5. Amuru roho mbaya zile zinahusika na vifungo vya nafsi kukuacha katika jina lake Yesu Kristo mwana wake Mungu.

Tazama: tofautisha, uwezavyo, wakati unavunja vifungo vya nafsi, vifungo vya nafsi vinaumbika kwa kila mtu mmekuwa na uhusiaono wa kimapenzi naye. Nje ya ndoa. Taja kila mtu na uweze kuvunja hizo vifungo vya nafsi. Kuna vifungo na wanyama? Kuna vifungo si za kawaida na watu wa familia? Kiroho umeweza kuwa na ukaidi wa vifungo vya nafsi vimeumbika kupitia ngono na mtu wa hali moja, kuomba miungu mingine, ama kujipata kwa kutabiri yale yatakuja, ama nguvu za kumtia mtu hali ya usingizi ili atende jambo fulani, ESP, maagano ya damu, nadhiri isiyo takatifu na maaguzi kwa nyota. Umewahi toa mimba ama baba wa huuyo mtoto umevunja vifungo vya nafsi na yeye na tena baina yake na mtoto.

**Maombi ya kuvunja vifungo vya nafsi:**

Vufungo vya nafsi baina ya namna ya watu fulani sasa kuvunja kwa vifungo vya nafsi ni lazima iwe kwa hao watu fulani. Ni sawa wakati tunapo uliza msamaha kwa kumhukumu mtu Fulani. Ikiwa majina hayawezi kuletwa kwa akili, elezea ndio uweze kumtambua huyo mtu ama unaweza tumia hali vile tu, tunaweza kuwa tukitofautisha ndio tutaweza kutubu kwa kifungo ama hukumu.

Vifungo vya nafsi ni kama pande mbili za mbao zimepakwa kitu cha kushikanisha pamoja. Wakati hizi mbao zinatenganishwa baadhi ya kila kipande huwachwa kwa kila kipande.

Nime kataa kifungo cha nafsi na

________________________________________

________________________________________

Na vunja kifungo katika jina lake Yesuna kuzikataa. Naulilza Yesumsamaha kwa matendo yangu yale yameleta vifungo na nina samehe wale wamefunga vifungo hivi nami. Narejesha lolote ndani ya nafsi yangu lile linaweza kuwa limebaki ndani yangu, nawachilia jambo lolote la kila nafsi ambalo linaweza kuwa limeshikana nami.

**Ninatubu dhambi za** _________________________________
Katika jina la Yesu. (Andika hizo dhambi kwa huo mstari.)

Na vunja kifungo cha nafsi na ___________________________
Ninachukuwa sasa mambo yangu na nina warejeshea yao katika Jina la Yesu (Jina la huyo mtu andika kwa huo mstari)

Natubu kwa kila hasira ama chukizo kuelekea watu wale wengine ama wewe Mungu kwa kuruhusu hii itendeke. Nisamehe kwa chukizo na hasira ninayo kwangu mimi kwa kujiunga na hizi dhambi: Najisamehe.

Natubu kwa hasira na chukizo kuelekea huyo mtu mwingine aliyejiunga na hii dhambi na ninamsamehe. Nina amuru pepo mbaya katika hii dhambi kuniacha katika Jina la Yesu, sasa niko chini ya damu Bwana, nijaze mimi na Roho Mtakatifu katika nafsi nii yangu. Nakushukuru na kukusifu, Yesuapata utukufu wote, Amina.

# Sura ya 9
# Kusononeka
## Hatua ya Kupokea Uponyo

Kuhuzunisha ni hisia ya kiasili ya mwanadamu inayotokana na hasara ya aina yoyote ile. Tofauti katika maisha yetu huja, kulingana na vile tunavyofanya wakati tunahuzunika, tunaweza jificha na kufanya kana kwamba haipo ama tunaweza endelea kuhuzunika maisha yetu yote na kuishi kwa hali ya kujihurumia. Hisia hizi mbili zitatuweka katika kifungo. Ilhali kuna njia njema ya kushughulikia huzuni ambayo itapatia Mungu nafasi ya kutupa uhuru ambao anatamani kutupa. Yesualikufa kwa ajili ya hasara zetu, alichukua nafsi zetu na sasa tunastahili tujifunze jinsi y kujitwalia uponyanji wake.

Unsatahili kuwa kweli na Mungu kuhusu hasara ambazo umepata maishani mwako. Yaweza kuwa majuto kutokana na ujana wako, ama pengine watu ambao wameaga kama vile mmeo, ama mke wako, mtoto, talaka ama maasi nakadhalika. Watu huhuzunika juu ya kupotelewa na ndoto zao, maono na mipango ya maisha yao.

Wakati mwingi wanadamu humlaumu Mungu kuhusu hasara zao. Watu wengi hawatambui uchungu wao kama hasara na hivyo mambo haya yanakaa yamezikwa ndani ya nafsi zao, kama kidonda ambacho kinaambukiza maisha yao yote.

**Kulia ni kusononeka.**

Mathayo 5:2-4 inasema, “Akafumbua kinywa chake, akafundisha, akisema, Heri walio maskini wa roho ; Maana ufalme wa mbinguni ni wao. Heri wenye huzuni. Maana wao watafarijika.”

Machozi hutoka kilindini cha moyo na siyo kutokana na matendo ya dhambi, lakini ni kutokana na kujua kuwa wewe ni maskini waroho, kutubu kutokana na kujaribu kufaulu kivyako na kuona upendo na neema yake ikija kukusudia.

Niliona senema ambayo asili yake ilikuwa hadithi ya kweli katika shule ya kiamerika, ambayo iligusa vijana kutokana na vichochoro mbalimbali vya ndani wa mji. Idadi ya watu katika vichochoro hivi

ilikuwa ni kusanyiko ya watu wa tamaduni mbali mbali ambayo walikuja pamoja katika shule ya upili. Watoto hawa na umri wa miaka kumi na tano walikuwa wanachama wa magenge wanaotumia madawa ya kulevya, wasiyo na nidhamu hata kidogo na ambao hawana haja kamwe na masomo. Fujo na kuuana ilikuwa ni kawaida. Tamduni hizi tofauti, weusi walatino, wahindi, walichukiana wenyewe kwa wenyewe. Katika hali ile kukaja mwalimu kijana mzungu aliyekuwa na roho ya kubadilisha mambo alinganga na kwa muda na watoto wafidhuli ambao walimchukia lakini hakufa moyo. Mwalimi huyu akaweka jaribio ambalo naeleza vyema dhamani ya kuhuzunuka na njia inayofaa. Alimpa kila mwanafunzi kijitabu na akawauliza kila mmoja wao kuweka matukio ya kila siku. Wangeandika chochote kile walicho panda na hawa kuhitajika kumwonyesha kijitabu kile. Walakini wale wanfunzi wote walipeana vile vijitabu bila kushurutisha na walitaka mwalimu avisome wakaandika kuihusu utoto wao ambao ulikuwa wakuogofya, mateso yao katika vichochoro ambavyo vilijaa magenge, dhuluma kutoka kwa wazazi na mengine kama yale watoto hawa walikuwa wanahuzunika. Walipata sikio la huruma na wakamwaga roho zao. Hadithi hii ilikuwa ya ajabu, wale wanafunzi wakampenda na kumheshimu mwalimu wao wakaanza kusoma vitabu kuhusu mateso ya wengine hata “the nazi hola Caust” nazile tamaduni tofauti zikanza kushikana na kupenda wenyewe kwa wenyewe. Ni nini ilifanyika? Walitoa huzuni yao na waka pokea uponyaji. kutembea pamoja na Mungu katika hasara zako kuna nguvu.

**Yafuatayo ni dondoo kutoka kwa kitabu “The Inner Healing[17]” ambacho tumekuwa tukitumia.**

Jambo moja la maana tunalostahili kujua ni jinsi ya kuhuzunika. Kuhuzunika ni ule uwezo wa kutambua na kusononeka kwa sababu ya hasara ambazo tumezipata. Mungu ametupatia uwezo wa

[17] Inner Healing Haki ya Kumiliki 1992 na Dunklin Memorial Church - imetumiwa kwa idhini ya ISOB.

kuhuzunika. Ikiwa mmoja wetu amepoteza mmoja katika familia kupitia kifo, tunaweza kuhuzunika hasara ile.

Shida zinazo chipuka ndani yetu wakati tunapitia hasara maishani mwetu lakini hatuhuzuniki hizo hasara. Badala ya kuhuzunika, tunaruhusu sisi wenyewe kuwa wagumu ndani. Kwa matukio, sisi tunatenda Jambo kwa mambo mengine kwa njia isiyo halali. Sisi tunakuwa kama tumechukizwa na tumeudhiwa nao. Ni kana kwamba hatutambui, ile uchunu mngwaruzo na hasara na haturuhusu Mungu aweze kutuhudumua sisi katika hali hizo.

Watu wa jamii wametwambia sisi uongo nasi twakubali kuwa ukweli. Tulielezwa ya kwamba wanaume hawawezi kulia, kwahivyo vijana wadogo walio na ushujaa hawafai kulia ikiwa wanataka kuwa wanaume. Mwanaume hafai kuonyesha uchungu ama sikitiko, ama uchungu. Lakini huo ni uongo.

Hii huwa shida kuu nasi wakati hatu ruhusu sisi wenyewe kuweza kueleza huzuni ile tunahisi ndani yetu. Hatutambui ya kwamba wakati tunakuwa wazi kwake Mungu na waaminifu, atatuponya kwa hizo hali ndani ya maisha yetu. Tutakapo leta haya mambo kwa mwangaza wake Kristo yeye anaweza kutuhudumia uponyo wake kwetu sisi. Mambo mengi yale yanatudhuru sisi, maishani mwetu yamejaa ndani mahali pa ndani ya mafikira yetu, tukitumai eti yatasahaulika. Lile hatujui ni eti haya mambo yote yataendelea kutudhulumu katika matendo yetu na watu tunaokutana nao kila uchao. Ni lazima tujifunze jinsi ya kuwa waaminifu, kwa wale watu tunao kutana nao, tena vile tunaonyesha masikitiko na vile tunahuzunika kuhusu hao. Tukisha waruhusu kuonekana, Mungu anaanza njia ndani yetu inayo tupa sisi ufahamu na ujuzi kuwahusu. Uponye sasa unaweza kufanyika.

Kizuizi kimoja cha uponyo wetu ni kwamba wakati tuko na masikitiko tuna uwezo wa kuona upande mmoja wa halifulani. Hii ni kumanisha hatuwezi kuona picha yote, tutaona tu pande mmoja kuna hatari.

Hatari moja katika kuhuzunika ni kuwa, tunajipata tumeingia ndani yake. Tuna jipata sisi wenyewe tumejazwa na kujihurumia na

kujihukumu. Kuna wakati halali wa kuhuzunika lakini kuna tena wakati halisi wakuendelea.

Sifikiri kama kwamba kuna mmoja anaye nena mabaya kumuhusu yeye aweze kuleta ndani ya maisha yao ni kusudi halisi, imekuwa nayo.

Tunaweza aje kushirikiana naye Mungu, ni yapi yanapswa kuwekwa ndani ya huu uungano? Ni naamini kuna kadhaa. Ilhali kwa hii somo tutaweza kugusia lile ninalo amini kuwa ya kwanza, na ya muhimu sana, na lile moja bila yake hatuwezi kabisa elewa mapenzi yake Mungu ndani ya maisha yetu na hii ni kuwa halisi naye Mungu.

**Hilo ni jambo la ukweli:**

***Kuna mambo mawili ya msingi ya ukweli***

Katika Zaburi 85 inasema wakati ukweli wetu una inuka juu kutoka kwa dunia kwamba sisi hupokea haki kutoka mbinguni kwa maneno mengine Yesundiye ukweli, yeye yuko pale, lakini ili tuweze kuwasiliana, ni lazima "tutume" ukweli wetu kwake.

"Fadhili na kweli zimekutana, haki na amani zimehusiana. Kweli imechipuka katika nchi, Haki imechungulia kutoka mbinguni.Naam, BWANA atatoa kilicho chema, Na nchi yetu itatoa mazao yake. Haki itakwenda mbele zake, Nayo itazifanya hatua zake kuwa njia."(Zab 85:10-13)

***Hali ya kwanza ya ukweli nikuwa halisi kwako wewe na Mungu***

***1 Yohana husema ukweli wetu unatuongoza kwa kuoshwa.***

("Na hii ndiyo habari tuliyoisikia kwake, na kuihubiri kwenu, ya kwamba Mungu ni nuru wala giza lo lote hamna ndani yake. Tukisema ya kwamba tunashirikiana naye, tena tukienda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli. Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote. Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe wala kweli haimo mwetu. Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. Tukisema kwamba hatutendi dhambi, twamfanya Yeye kuwa mwongo wala lake halimo mwetu." (1 Yohana 1:5-10)

Hatuwezi kataa ama kuzika hisia zetu ya yale mambo tumeyapitia na masakitiko yetu bila kuigaramia kwa bei mbaya. Wakati hatukufaa kuishi kwa hisia zisizo za Mungu ama sisi tuwe tukiongozwa na masikitiko yetu, tunakuwa na "kuwapa" wao kwa Mungu kama kitu kinachoendelea, amahakija kufa.

Hatukatai eti hisia na masikitiko huwa, lakini tunakataa, ukweli wao kututawala maishani mwetu. Tunayakili kwake Mungu na anchukua zile sehemu, zisizo zake, na dhambi, na anasamehe na kuyaondoa.

**Ndondoo zifuataazo zilitolewa kutoka kwa kitabu "Be real with God."[18]**

> *Muundo halisi wa Mungu katika maisha yako, ni kwamba uwe na uhusiano naye ulio hai. Kusudi ya hiki kitabu ni kusaidia wewe kupata huu uhusiano na kutembea ndani yake. Sikuongeza sehemu za kazi ile tunafanya maishani na hasa, kazi za kidini na michezo ya kidini, naomba hiki kitabu kitakupa nguvu ili uweze kuwa wazi kwake Mungu, muumba wako na kupitia kuwa wazi utaweza kuuhisi upendo wa ajabu wake Mungu na neema ile ita kufanya wewe kuwa lile umbo halisi maishani mwako.*

***Kila mmoja wetu huanza na kutojua yeye ni nani hasa. Kisha tunakua kwa nia halisi kuhusu sisi ni akina nani.***

> *Wale "wanataka kuwa" huwa wanakuwa kazi zile tunazofanya, kila mara na haya mawazo yanafanywa kama yasiodhibitika vizuri. Hizi kazi zote hujenga fujo kama za kitunguu maishani mwetu. Ni kusudi lake Mungu kuturudisha kwa yule halisi kwa wewe "uliye" hakika. Huyo ndiye "wewe" mwenye Mungu anapenda kwa uhakika na ni wewe pekee, yule Mungu anaweza fanya kazi naye kukufanya wewe mzima na maisha yanayo tosheresha.*

***Tunaogopa kugundua sisi kweli ni nani***

[18] Dondoo kutoka kitabu Uwe Halisi Kwa Mungu – na Larry Chkoreff

*Kwa miaka mingi tumeweza kutengeneza kuta za kujidanganya juu ya sisi wenyewe kama kujo za kitunguu. Tuko nanjia mingi sana, za kuficha yale watu wengine ama sisi tumeweza kutengeneza. Hizi kazi niza kujichanganya na tumekuwa wapotovu sana nyuma ya kujo nyingi ya kwamba tumendanganywa na tunatosheka na yale jeremiah alisema, "Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua." (Yeremia 17:9)*

*Kutoshereka kwa ukweli katika haya maisha ni kujua wewe kwa uhakika umekubalika. Ni kujua ya kwamba hujui kuwa mkamilifu hakika kwa tukio moja lakini unapoenda maishani Mungu ataruhusu hizo kuto ziweze kutoka moja kwa moja jinsi tunavyoweza stahimili na kuikubali. Una gundua kwamba Mungu anakukubali, jinsi tu uvyo. Ilhali yeye anataka kuondoa hizi kujo ili kupata "wewe" halisi. Utapata kujua Mungu ni mpole katika huu mwenendo wote. Utagundua kuwa mara mingi hata upole unaweza kuwa chungu.*

*Kunaweza kuwa na sehemu maishani mwako zimejificha na kana kwamba hutaki mtu, na sana sana Mungu, kufichua na kuziweka wazi unajua ina weza kuwa na uchungu mwingi lakini Mungu husema endelea mbele na uamini mimi ndiye niwezaye kuguza huo uchungu mara moja tu. Naweza leta uchungu mwingi, maishani mwako kwa kuiguza lakini ni kwa hayo uponyo utakao kuja ni wa dhamana." Ni kama daktari anauliza," si afadhali uchungu wa kisu changu kama yamaanisha kutoa huo ugojwa?"*

*Kuna sheria katika sayari ya dunia ambayo hufanya kazi kila mara; inatwa kupanda na kuvuna.*

*(Wagalatia 6:7-8) Mtu atavuna yale yote amepanda. Hii sheria inatumika hata katika ukweli. Ikiwa unapanda kwa kweli utavuna kwa ukweli. Ikiwa una unapanda uovu na auongo,utavuna giza tupu na ukweli hautang'aa maishani mwako. "Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu." (Yohana 18:37b)*

*Mafale Daudi aliweza kusema maneno haya baada ya kujaribu kuficha dhambi zake mbaya kutoka kwake Mungu. Daudi hangeweza kuishi na yeye, lakini aligundua kwamba Mungu anaheshimu ukweli na ukweli utatuweka huru.*

*"Heri BWANA asiyemhesabia upotevu, Ambaye rohoni mwake hamna hila. Niliponyamaza mifupa yangu ilichaa kwa kuugua kwangu mchana kutwa."(Zaburi 32:2-3). Soma Zaburi 32 yote.*

*Kuna ile gharama utalipa kabisa. Mithali 23:23 inasema, "Inunue kweli, wala usiizue; Naam, hekima, na mafundisho, na ufahamu." Moja ya gharama utakayo ilipa ni unyenyekevu. Naamini kwamba uovu ulikuja kwa ulimwengu wetu na kuendelea kuwa kupitia kutoaminika kwa mwandamu. Hizo picha ziko hapo chini zinaonyesha hivi. Kiwango kile cha kuonyesha wewe sio halisi kiwango cha nguvu mbaya ama za giza mashani mwako. Jinsi pengo liko kubwa, ndio ukubwa wa nguvu za mapepo.*




***Kuwa halisi au hakika ni jambo la kwanza la ukweli, na hali ya pili ya ukweli ni Yesu.***

*Neno lake ni ukweli wa mwisho hata kama neno lake halita dhihirika, kwa wale hawafanyi zoezi la ukweli kwanza, nani huharibu uaminifu wao mbele zake Mungu*

***Yesu akajiita yeye mwenyewe "ukweli".***

*"Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi."(Yohana 14:6)*

*Kuwa huru kuna tabia zingine na moja wazo ni ukweli wakati hizi jinsi mbili za ukweli zimewekwa hapo juu zikiguza moja wapo Mungu anaweza kwenda kazini.Hali zingine zimeandikwa katika sura ya nane na hukaa ndani ya neno lake, kuwa mwanfunzi wa Yesu, kumtii yeye*

*na si kudai haki yako maishani. Tena utajua ukweli, na ndio kuwa na uhusuiano naye. Ukweli ulio wa kiwiliwili*

*"Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itakuwaweka huru. Wakamjibu, sisi tu uzao wake Ibrahimi, wala hatujawa watumwa wa mtu wakati wo wote; nawe wasemaje, mtawekwa huru? Yesuakajibu, Amin amin, nawaambia, kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi. Wala mtumwa hakai nyumbani sikuzote. Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli."* (John 8:31-36)

*Ni lazima uwe na uhakika kuhusu masikitiko yako, hisia na uchungu ndio umwezeshe Mungu kukuweka huru.*

**Kuhuzunika kwa kiungu**

Mungu ametuwekea njia ya kuhuzunika. Ilhali ikiwa sisi hatujapata onyo, ama tukikosa kuwa waangalifu tunaweza jipata ndani ya kuhuzunika kusiko kwake Mungu. Kuna vifungu sita za kuhuzunika ambazo zina jionyesha zenyewe katika huu mfuatano, ilhali ni zakawaida kutembea nyuma na mbele kati ya hizi hatua tunavyo endelea.

1. ***Kukana.*** Kuhini; kwa urahisi hatutaki kukubali msiba.
2. ***Kupigana na Mungu:*** Ikiwa Mungu atarejesha ama tengeneza tena ama kujaza tena lile linatufanya tuhuzunike, tutafanya chochote atakalo.
3. ***Hasira:*** sisi kabisa hatufai kwa yale yametendeka na tuna hisi ya kwamba, hatujatumika vizuri: Hii inaleta haki kwa hasira zetu

4 ***Kukubali:*** Tunakubali kwamba ilitendeka natuna kiri ya kwamba hakuna jambo tunaloweza fanya katika jambo hili.

5 ***Kuhuzunika kwa hasara:*** Tunakuwa waaminifu kwa ajili ya hisia zetu tunashiriki hizo hisia na wale wengine na kuruhusu sisi wenyewe kuponywa.

6 ***Azimio:*** Tukusudie kuchukua hizo vipande, na kuweza kuendelea na maisha.

**Kiwango kingine ya ukweli**

Tena tunatakiwa kuwa waadilifu kuhusu matendo yetu ya dhambi ya kwamba yametendeka kwetu. Kunayo mambo tatu yawezekana tumetenda kwa matendo yetu kwa wengine ama yale maisha yametupatia sisi.

1. Hukumu: Teumeambiwa kutiak maandiko, hatufai kuhukuu isiwe hata sisi tuta hukumiwa.
2. Kuheshimu baba na mama: Ikiwa hatuta waheshimu maisha yetu hayataenda vyema kwetu sisi.
3. Kupanda na Kuvuna: Wakati tunapanda mbegu, ni lazima tutarajie mavuno.

**Habari njema!**

***Yesu alichukua huzuni zetu.***

katika Isaya 53:4, "Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa."

Wakati tunapowaachilia ukweli wa huzuni, tunaweza vuna ukweli wa uponyo wake. Aliweza kuchukuwa nafasi yetu. Yesuakachukua uzito na huzuni za kila mmoja aliyekuwa hai wakati alikufa pale msalabani. Alichukuwa kwa ajili yako ndiposa uwe huru.

**Huduma yake Yesunikutufanya sisi kuwa huru. Kuponywa ndani na kutuweka huru kutokana na dhambi zile zimeingia kwetu kinyume na hasara.**

Tazama kwanza mabadiliko yale Yesualikuja kutupa sisi, tena tazama ahadi za wale walikubali dhawabu yake. Ni ya faida kujua kuendelea kwa maandiko ya Isaya 61:1-11,

*Roho ya BWANA MUNGU i juu yangu; kwa sababu BWANA amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; amenituma ili kuwanganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao,na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao.*

*Kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa na siku ya kisasi cha Mungu wetu; kuwafariji wote waliao.*

*Kuwaagizia hao waliao katika Sayuni, wapewe taji ya maua badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito; wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na BWANA, ili atukuzwe.*

*Nao watajenga mahali pa kale palipoharibiwa, watapainua mahali palipokuwa ukiwa zamani, watatengeneza miji iliyoharibiwa, mahali palipoachwa kizazi baada ya kizazi.*

*Na wageni watasimama na kulisha makundi yenu, na watu wa kabila nyingine watakuwa wakulima wenu, na watunzaji wa mizabibu yenu.*

*Bali ninyi mtaitwa makuhani wa BWANA; watu watawaiteni wahudumu wa Mungu wetu; mtakula utajiri wa mataifa, na kujisifia utukufu wao.*

*Badala ya aibu yenu mtapata maradufu, na badala ya fedheha wataifurahia sehemu yao; basi katika nchi yao watamiliki maradufu; furaha yao itakuwa ya milele.*

*Maana mimi, BWANA, naipenda hukumu ya haki, nauchukia wivi na uovu; naminitawalipa malipo katika kweli,nitaagana nao agano la milele.*

*Na kizazi chao kitajulikana katika mataifa, na uzao wao katika kabila za watu; wote wawaonao watakiri ya kuwa wao ni kizazi kilichobarikiwa na BWANA.*

*Nitafurahi sana katika BWANA, nafsi yangu itashangilia katika Mungu wangu; maana itoavyo amenivika mavazi ya wokovu, amenifunika vazi la haki, kama bwana arusi ajipambavyo kwa kilemba cha maua, na kama bibi arusi ajipambavyo kwa vyombo vya dhahabu.*

*Maana kama nchi itoavyo machipuko yake, na kama bustani ioteshavyo vitu vilivyopandwa ndani yake; ndivyo BWANA MUNGU atakavyootesha haki na sifa mbele ya mataifa yote.*

***Inayakupendeza kuzingatia kuendelea kwa Mlango huu wa Isaya 61.***

1. Yesualikuja kusaidia watu waliokuwa wamepoteza maishani mwao, maskini waliovunjika moyo waliotekwa nyara, wafungwa wale wamefungwa kwa minyororo ndani yao.
2. Tena anaweka huru nakulipizia hao kizazi kwa wale waanzilishi, wa dhambi kinyume na waadhiriwa, huyo akiwa shetani na jeshi lake.
3. Baada ya haya fariji hao watu. Jina fariji hapa linamaanisha kuhurumia mpaka inamfanya mwenye kuhurumuwa atubu. Hii inamaanisha kwamba wale watu wamefungwa, wanauona upendo wa Mungu, ukiwaelewa na kuwaongoza katika maisha mpya.
4. Tena anatuliza wale wanaomboleza huka Sayuni, Sayuni inawakilisha ufalme wa Mungu. Neno kutuliza linamaanisha kuamuru, agiza, funza na ugeuze/badilisha. Mungu anataka kututuliza baada ya kuingia Sayuni ufalme wa Mungu. Hii ndiyo njia yake, kwa kutoa watu wale wamepoteza na kuomboleza.
5. Tena angalia 61:4-11 uone zile ahadi Mungu atafanya nasi nakupitia sisi.

**Ushuhuda**

Miezi michache baada ya Yesukuniokoe,katika 1979 nilikuwa ni "kiomboleza" kuhusu kupoteza miaka mingi maishani mwangu kabla ya kumpata Yesu. Nilikuwa na mwambia Mungu jinsi nihisi, nilikuwa na tamani kuanza tena. Lakini furaha yangu ikawa eti nimeokoka, lakini huzuni ni kuhusu hiyo miaka niliyopoteza.

Nilikuwa na njaa la neno lake Mungu na nilikuwa nafuata wahubiri wa kipentakoste, kwa sababu ujumbe wao ulionekana kunitosheresha mimi zaidi. Nilikuwa na pata kanda ya kusikiliza kutoka kanisa la The Way huko Carlifonia. Mhubiri Jack Hayford alikuwa anahuburi katika ibada ya Jumapili na akanena ujumbe wa unabii ule ilinihusu mimi pekee. Nilishangaa tangu awali ilikuwa kwa kanda ya kusikiza na nilikuwa naisikiliza kwa pahali pale nilikuwa nafanyia biashara. Lakini Mungu alikuwa anaongea akinielenga mimi.

Mhubiri Hayford akasema kwa ujumbe wa unabii "maisha yako ni kama hati ya kuviringisha, na kwamba yuko na kusudi la maisha

yako iliyoandikwa pale, lakini hiyo hati ya kuvitinishwa imechomwa mwisho, mwisho, mwisho wa kiviringisho chako cha maisha kimechomeka na kuwa Jivu na kuanguka chini. Huwezi kuzirudisha tena kwa kivurungisho chako ndio maisha na kusudi lako liwe nzima tena. Lakini kwa hivyo mimi Mungu……(Joel 2:25-27).

Wakati nilikuwa naandika hiki kitabu baada ya miaka 29, naweza sema kwa ukweli hayo yametendeka, kwa ukuu mwingi kuliko hata matarajio yangu makuu Alinipatia mimi urembo kwa jivu, mafuta ya furaha kwa maombolezi:

**Ikiwa hutahuzunikia hisia yako hutakuwa na "uzima baada ya kifo" ama miujiza ya ufufuo kwa hii maisha yako.**

Tazama katika isaya 61 tumeweza kuahidiwa chochote, mambo yote mazuri, yanaletwa kwa umbo la kubadili. Urembo kwa jivu, mafuta ya furaha kwa kuomboleza na kadhalika. Huku kubadili ni kununuliwa kwa msalaba, ama kwa maneno mengine, damu ya maagano na Mungu, chochote tunacho huenda kwake Mungu, na chochote anacho chatukujia sisi.

***Hii Ndiyo Alipata:***

"Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu. Hakika ameyacukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa." (Isaiah 53:3,4)

***Hii ndiyo matunda ya yale aliweza kupata***:

Kumwaga huzuni yako yote na kumpa Mungu hasara maishani mwako, itawezesha yeye kukumwagia kupitia ufufuo usio wa kawaida "dhamani" haingezaliwa isipokuwa tu kupitia hasara ya "kufa" na "kufufuka" kwako. (Isaiah 53:11)

**Dondoo kutoka kwa evelyn akin:**

> *Kabla hatujaendelea na uponyo wa ndani inaonekana kwangu ni lazima kwanza "jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi.."(Romans 6:11) ile inahusisha kufa kibinafsi (sana sana ile sehemu kwetu sisi ina weka uchungu ule unahitaji uponyo wa ndani) Watchman Nee alielezea kwamba sisi*

*tushajua tayari Yesualikufa lakini ni lazima tusadiki hivyo. Hii inamaanisha kukuja kwa mahali hatuta patiana haki zetu kwetu binafsi ( haki zetu za maisha yale tunaishi kutamani na kutawala hisia zetu vizuri) Lakini tunapoenda kilindini na kufungua "haki" zetu kwa uchungu na yote yametendeka kwetu ile mpaka sasa imekuwa sisi ni nani na tumejua sisi tunakuwa, nataka kufikiri ya kwamba mara mingi sisi huwa vile uchungu wetu ulivyo, kujulikana kwa njia kuu sana. Hii ina maanisha, tuachilie haki zetu, tutende kwa kujihurumia, hasira, chukizo na kupata kile na kadhalika. Hiki ni kifo cha kweli kwa ubinafsi. Nina amini. Ni ya kupenda kwa kusema, nimepitia na inaweza tendeka na kamwe haitaletwa tena, kama haijawahi tendeka – wacha iweze kizikwa na Kristo, kama vile dhambi zangu zimezikwa na yeye. Tunafurahia kwamba dhambi zetu zimechukuliwa na yeye,lakini hatuelewi jambo hilo lingine ni kufa kwa kibnafsi ile huleta uzima ndani ya roha lakini inahitaji tukufe kwa haki zetu na kwa uchungu wetu.*

# Sura 10
# Msamaha
## Mafuta ya Uponyaji wa ndani

Tumejadiliana mambo mengi kuhusu uponyaji wa ndani na uzima katika masomo ya hapo awali. Ilhali hili somo la msamaha ndilo jambo kuu la uponyo wa ndani. Hili ndilo Jambo la muhimu

Msamaha ndio ulikuwa vita vya kifo ule uliweza kumshinda shetani. Kutosamehe hupatia shetani mamlaka ya kutawala maisha yako. Mtume Paulo akatuonya sisi kwa 2 Wakorintho 2:10-11 kuhusu shetani kuchukua mamlaka dhidi yetu hupitia kutosamehe 2corin 2:10-11 inasema, “lakini mkimsamehe mtu neno lo lote, nimemsamehe kwa ajili yenu mbele za Kristo. Shetani asije akapata kutushinda; kwa maana hatukosi kuzijua fikira zake.”

**Huduma ya Yesu imeelezewa katika Isaya 61 na anaongea katika Luka 4 kutuweka sisi huru kupitia msamaha kwa yale mambo yanayo tufunga sisi.**

“Akapewa chuo cha nabii Isaya , akakifungua chua, akatafuta mahali palipoandikwa,

Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena. Kuwaacha huru walioteswa, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa. Akakifunga chuo, akamrudishia mtumishi, akaketi; na watu wote waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho. Akaanza kuwaambia, Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu.” Luka 4:17-21)

Ilhali hatuwahi jisikia ama pata mawazo iliyofanywa kuwa upya kwa neno lake Mungu mpaka wewe upatie Mungu ukweli kuhusu wewe mwenyewe. Ni lazima ufungue “vyumba” vyote ndani ya roho yako utaweza haya yote ikiwa tu utaweza kuongea na Mungu kama rafiki yako wakaribu mweleze vile wewe unahisi, dhambi, mashaka kutosamehe na yote yale yakujiona wewe duni sifiche chochote! Hawezi kukuonyesha wewe ni nani ndani yake mpaka umwonyeshe wewe ni nani bila yeye kukosa kutenda haya utaishi kuwa mfungwa

***Tunahitaji kupata ukweli wa utambulisho wetu kutoka kwa mungu kupitia neno lake.***

Na kusihi uweze kusoma hadithi iliyo (hesabu 13 a 14) kuhusu wana wa Israeli na wale watu kumi na mbili waliotumwa kuichunguza nchi ya Ahadi. Mungu aliwaahidi hao nchi ya ahadi. Ni wawili pekee kwa wale wote kumi na mbili. Joshua na Caleb walikuwa na imani tosha ndani ya neno lake Mungu kuona hao wenyewe wakishinda adui zao wale wengine kumi wakasema, “Kisha huko tuliwaona Wanefili, wana wa Anaki, waliotoka kwa hao Wanefili; tukajiona nafsi zetu kuwa kama mapanzi; nao ndivyo walivyotuona.”(Hesabu 13:33)

***Shetani hupanda mbegu ya kutoa mfano ama picha mbaya ndani yetu***

Katika mathayo 13:1-23 Yesuakawaambia wanfunzi wake kuhusu fumbo, neno lake Mungu kuwa limepandwa ndani ya mioyo yao kama mbegu. Akaelezea vile inafanya kazi na vile shetani tu atajaribu kuiba neno ndani ya mioyo yetu. Lakini hata hivyo (shetani) ni yeye alikuwa mpanzi wa mbegu.

“Akawatolea mfano mwingine, akasema, ufalme wa mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika konde lake; lakini watu walipolala, akaja adui yake akapanda magugu katikati ya ngano akaenda zake.” (Mathayo 13:24-25)

**Ukweli katika neno la mungu unaopaswa kuutafakari.**

Haya mambo hakika ni mbegu njema, zile zitazaa matunda mema maishani mwako.

***1. Ulikuwa umepotea na bila tumaini***

Hii inamaanisha kwamba kuna mtu aliyepaswa akutafute wewe (Ephesians 2:12)

***2. Ulikuwa umekufa ktika dhambi***

Hakuna njia nyingine ya mwanadamu aliyekufa ni ile tu kupokea uhai. Waefeso 2:1 a na b) inasema, "kwamba zamani zile mlikuwa hamna Kristo........mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani."

Hamna njia nyingine kwa mfu, ila kupokea uzima. Waefeso 2:1 inasema, "Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu ;"

Damu ya Yesuiliyomwagika pale msalabani ilifanya mengi kuliko kukusamehe dhambi zako. Tazama haya mandiko kwamba sisi tuna msamaha na ukombozi "NDANI YAKE" (Wakolosai 1:14) inasema, "ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani msamaha wa dhambi." Waefeso 1:7 inasema, "Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu,msamaha wa dhambi, sawa sawa na wingi wa neema yake."

***3. "Msamaha" wetu wa mwanzo hauleweki***

Wengi huhisi ni kama tu hakuna mabadiliko, lakini ukweli ni kwamba Yesuameshawaondolea 'kuwaruhusu" ama kuwasamehe dhambi zao.

Vibaya! Ulisulubishwa naye YesuKristo. Jambo la kwanza Mungu alikutendea ni "kukuweka" katika hali yake Kristo kufa kama yeye. Ile hali yako ya kale ya Adamu "mwanzo wako" haikuwa na tumaini la kuwa inaweza oshwa ulikuwa ufe. Malipo ya dhambi ni kifo. Habari njema ni kwamba ulikufa wewe. Ulikuwa tayari "ndani ya Kristo" wakati aliposulubishwa, wewe ulihitaji kuigundua na kuamini na kuikubali.

***4. Wewe ulikuwa tayari "ndani ya kristo" wakati haya yote yalikuwa yanafanyika***

(Wagalatia 2:20) "NimesuMbuliwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu."

***5. Ulikufa naye Kristo***

(Warumi 6:5) "kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake. "

***6. Ulizikwa naye Kristo***

"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kususdi kama Kristo alivyofufuka katika wafu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima." (Warumi 6:4). "Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo; na katika huo mkafufuliwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu."(Wakolosai 2:12).

Ikiwa uko na wakati mgumu kwa kujitaua nafikiri unaweza jifunza kwa moyo wa Warumi sita. Kufanya hii imekuwa ya maana sana ndani ya maisha yangu

***7. Uliwekwa uhai pamoja naye kristo***

Wakolosai 2:3 inasema, " na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehe makosa yetu." Waefeso 2:5 inasema, "Hata wakati tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema."

***8. Ulinunuliwa naye kristo ukaketishwa naye kristo***

(Waefeso 2:5-6) "Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu"

Huu ndio msimamo ulio kubalika naye Mungu siku ya leo na msingi wa haki uliokubalika. Kama vile ulimwengu wa kiroho unahusika, mahali pako pako naye Kristo juu mbinguni wewe umeketi kwa kiti cha utawala. Shetani na haa akili zako wewe mwenyewe zitakueleza ya kwamba wewe hujaketi na Kristo huko juu mbinguni lakini huo ni uongo! Unahitaji kujua ya kwamba Mungu alisha kuketisha hata kabla ya kuokoka!

***9. Wewe ni kiumbe kipya***

2 Wakorintho 5:17 inasema, "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya. "

***Unaweza uliza "haya yaweza fanyika aje?***

Swali njema Mungu alituweka ndani ya Kristo, 1 wakorintho 1:30 inasema, "Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki na utukufu, na ukombozi."

Kuwa katika Yesuni kama kuwa ndani ya kile kijidude hutia mamba na yai ya mama na baba. Uliridhi historia yao katika kizazi chako. Wewe fikiri kuwa ni wewe adhiri ndani ya kitabu wakati kitabu kinacho ondoka adhiri huwa ndani yake. Wakati kitabu kinawekwa katika kabati hata adhiri inawekwa. Kikichomwa hata nayo inachomwa. Ikiwa kimiujiza kitabu kinarejeshwa na kuwekwa kwenye kabati hata adhiri pia. Historia yako na wewe ni nani ndani ya Kristo, ni matokeo ya agano ya Adamu na Mungu kupitia kifo chake YesuKristo pale msalabani na ufufuo wake.

***10. Wewe ni mwenye haki***

Kuwa mwenye haki humanisha ya kwamba 'kusimama na haki naye Mungu. Mwana wa kiume (ama binti) ni wa haki kwa kuzalilwa na babake. Yeye yuko ndani ya familia na yeye yuko na msimamo wa haki ule mtu mwingine ama jirani hana. Sisi ni wenye haki kwa kuzaliwa kwetu si kwa jambo tuliyo ifanya. "Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu,ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye." (2 Wakorintho 5:21). Sisi ni wenye haki kwa sababu Mungu ameweka uhai ndani yetu si kwa sababu ya vile tunavyoishi ama tenda.

***11. Utawala wa shetani dhidi yako umevunjwa***

Shetani alikuwa na utawala wa hali yako ya kale,lakini hali yako jipya ni roho wake Kristo pekee, umeweza kushinda shetani. "Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye; tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufka katika wafu hafi tena, wala mauti haimtawali tena."(Warumi 6:8-10) .Ikiwa roho wa dunia imekuweka. Kusihi na hofu Mungu atakuweka huru sasa. Kwa sababu ya yule uliye wewe ndani ya Kristo "mambo maovu" hayana nguvu juu yako. Badala yake, wewe una nguvu juu ya hiyo yote na kuweza kubadili yawe baraka. Wakolosai 1:20 inasema, "Na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake kufanya amani kwa damu

ya msalaba wake; kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni."

***Kwa nini siwezi kuhisi vile haya maandiko yanasema?***

Ninafuraha kwa kuwa umeuliza haya. Hili ni swali la maana sana. Ilikuchukuwa miaka ili wewe uweze kupata ulimwengu na "miungu mingine" kulingana na wewe umeweza kuelimisha kwa hatia dhambi, hofu na kuelewa kwa laana na tena itachukuwa muda ilikuweza kufanya akili zako upya kwa ukweli. Kutokana na jinsi Shetani anavyoona anajaribu kuiba mbegu ya neno lake Mungu kutoka kwa moyo wako. Ikiwa anaweza weka mshurutisho wa kutosha ndani yako na hali yako na hatia utaweza kukosa kuaimini.

**Tunapokea dhawabu aje?**

***1. Fanya yesuna neno lake mtawala na mungu***

Ni lazima uamue kuamini neno badala ya hisia zako mitindo ya kimwili ya kale. Ni lazima uamue kutii neno kutii ni ukamilifu wa sehemu ya kuamini. Warumi 10:9-10 inasema, kwa sababu, ukimkiri Yesukwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokaka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.

***2. Kuwa mwaminifu naye mungu kuhusu hali yako***

Mambo yote itasafishwa katika mwangaza, mambo yote itawekwa chini ya kifungo cha giza. Ni lazima ulete hali yako chini ya mwangaza, kwa Yesukatika uaminifu. Ikiwa unaweza kubali na mtu mwingine hiyo inaweza kuwa ya nguvu sana. Ilhali tumia onyo kali kwa ujasiri na wengine.

***3. Samehe wengine na upokee msamaha wako***

***4. Jikubali jinsi ulivyo n kile Mungu alikuumba uwe*.**

Jua Mungu alikufanya wake "kazi ya mikono yake" ile inaweza tafsiriwa kuwa "poiema" ama uhalisi mmoja wa aina ya kipekee shairi, (Waefeso 2:4

**Vile tunafanya wengi ni jambo kuu**

Mithali 14:35, "Upendeleo wa mfalme humwelekea mtumwa atendaye kwa busara; bali ghadhabu yake itakuwa juu yake aletaye

aibu." sisi sote tunapaswa tuwe waangalifu jinsi tunafanya wengine kwa njia ile Mungu angetaka tuwafanyie. Tunastahili kutenda wengine na haki lakini si kwa hukumu na hatia. Ikiwa tutatumia hatia, aibu na hukumu kwa watu, hata kama ni kwa nia nzuri tutakuwa tukifanya kazi ya adui na pengine kukata maisha yake munug kwa watu wale tunajaribu kusaidia. Kuna wakati atasababisha wewe utumie upendo wa kudhibitisha kusaidia watu wengine kwa wema. Nimeweza kupitia hiyo hali lakini ni lazima tuwe waangalifu zaidi kujua kwamba huyo ni Mungu anaye niongoza kwa uwezo huu, ama tuweze kuanguka katika makosa mbaya na kugwaruza mtu vibaya

**Mkururo wa 'Canari'**

Katika kitabu cha John Steinbeck kuna somo kuu kuhusu hatia na aibu. Doc kama mchezaji mchanga kwa mchezao wa mpira wa chimbuko, aliweza kurusha sarafu ile imepasha uharibifu wa kuishi kwa akili zake kwa kugonga , gonga(Nimesahau jina late lakini tutamwita Joe). Joe alishtuka kuwa pweeza kama kitu kinachogonga ama hofu maisha yake yote. Kuchagua moto na hatia. Doc angeenda kumtafutia,kumlisha na tena kumjali yeye. Doc alikuwa anajenga nyumba ya kuhifadhia baharini na alikuwa karibu kumalizia. Wakati mmoja Doc hakuwa mjini mlevi akatumia ile nyumba kwa karamu ya ulevi na akavunja lile tangi la maji na kuharibu ndoto ya Doc. Wakati Doc aligundua ya kwamba huyu mlevi amefanya huo uharibifu, papo hapo akamsamehe akijua ya kwamba kuweka mtu kwa hatia mama aibu ilikuwa chungu vibaya sana, hata chungu kabisa kuliko kupoteza ndoto yako ya maisha. Ni la kushangaza kuona uhalisi wa kutotaka kupata hatia na aibu kwa mwingine. Ikiwa wewe umeshakuwa kombolewa kutokana na hatia na aibu naye Yesunawe utakuwa wa makini kuzuia wengie kutoka kwa matokeo haya mbaya na ya kuogofya.

**Ombi:** Aibu huelekeza kwa kujichukia. Pahali kuna kujichukia ni lazima kwanza tu uungame na tutubu "Mungu, nina ungama dhambi za kujichukia. Naomba msamaha wa kila chukizo ninao ibeba ndani ya mwili wangu, nafsi ama roho. Tafadhali nisamehe na unioshe

kutokana na kujichukia, nalete njia zangu zote za kale za kufikiria kuamini, kuhisi na hata kutenda kwa msalaba na ulize aweze kuleta utu wa zam kivuli chako pahali pake. Nipatie njia zako za kufikiri,kuamini, kuhisi na hata kutenda. Fanya upya nia yangu na ubadilishe nafsi yangu. “Yesuwewe ni Mungu wangu, nina ungana hatia yangu na aibu. Naleta kwako yale nimetendewa na wengine na yale nimetendea wengine na yale nilitenda ambayo ilikuwa dhambi kwako na mbele zako. Asante Bwana kwa damu yako iliyo mwagika pale msalabani, Nina ndiyo haya yote matendo iweze kusamehewa na kuondelewa. Asante kwa kuvumila aibu na hatia yangu hata kama ungana hukustahili. Asante Mungu kwa kuvumilia aibu na hatia yangu hata kama hustahili. Asante kwa kuitwa mwenye hatia na kwa kuwa na aibu na kufanywa mabaya, vile hukuwa na makosa na nilikuwa mwenye hatia kabisa, sasa kwa urahisi ninaamini neno lako lile lina sema mimi sihukumiwa na kwamba dhamiri yangu imeoshwa.

“Ni nani atakayepanda katika mlima wa BWANA? Ni nani atakayesimama katika patakatifu pake? Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe, asiyeiinua nafsi yake kwa ubatili, Wala hakuapa kwa hila. ”(Zaburi 24:3-4)

# Sura ya 13
# Vita Vya Akili Zako
# Hatua Kuelekea Kuponywa

Warumi 12:1-2 “Basi, ndugu zangu,nawasihi,kwa huruma zake Mungu,itoeni mili yenu iwe dhabihu iliyo hai,takatifu, ya kumpendeza Mungu,ndiyo ibada yenu yenye maana.”

Biblia iliyopanuliwa (Amplified Bible) inasoma “kwa maoni ya wote rehema zake Mungu.” Ninaamini hiki kielelezo kwa rehema zake Mungu ambayo Paulo ameandika kuhusu katika Warumi 1-8 tena 9, 10, 11 ni maneno yaliyoingizwa katikati na wazo la Paulo akaliendeleza tena katika kifungu cha 12. Paulo anasema kwamba wakati unaangalia nyuma na kuwekeza kuona rehema zake Mungu zote kukuelekeza wewe lile jibu sawa ama lilokubalika ni kuweza kupeana mwili wako kama dhabihu iliyo hai, na sana sana akili zako. Kwa maneno mengine hilo ndilo ndogo sana unaloweza kufanya. Katika tafsiri iliyopanuliwa inaitwa “akili zako za busara huduma na kuabudu kwa kiroho. Tazama tena kwamba ahadi za kuwa na akili yako imebadilishwa ili uweze kujua ama kuhakikisha mapenzi kamili yake Mungu.

Neno kuhakikisha katika Warumi 12:2 ni neno sawa limetumiwa katika kusafisha dhahabu na fedha kwa hivyo tunajua hii njia ni lazima iwe na uchungu. Unataka mapenzi yaliyokamilika yake Mungu maishani mwako? Peana akili zako, jinsi unavyofikiri, kwa hii njia ya kubadilisha.

Neno badili ni la kusisimua katika kamusi ya ‘Strong’s’, inaelezea kama kugeuka: badili badili hasa kwa uzuri. Kubadilisha kuwa umbo lingine, mfano wake Kristo uliweza kubadilishwa na ukawa umeng’aa na nuru ya kiungu katika mlima wa ugeuzi.

**Tunahitaji mabadiliko kamili katika kuwaza kwetu.**

Hata baada ya kuokoka ama kuzaliwa mara ya pili, watoto wa Mungu, kuwaza kwetu nilazima kugeuzwe ili tuweze kuona ni nini hasa Mungu ametuumba tuwe. Hataki sisi tuwe bila usalama au duni. Anataka tujue kuwa sisi ni vyumbe wapya ndani ya Kristo, sehemu ya

jamii mpya ya watu. Yesusasa anaishi ndani yetu na ametusababisha sisi tuweze kuzaliwa tena, katika jamaa mpya tukiwa na utawala juu ya shetani. Sisi tuko na Roho aliyefufuka wake Kristo, jambo Adamu na Hawa hawakupata kufurahia.

***Kwa nini tunahitaji mabadiliko katika kuwaza kwetu?***

Tunahitaji mabadiliko katika kuwaza kwetu, kutoka kwa uongo kuingia ukweli. Ukweli ndio chombo kilicho na nguvu zaidi hapa ulimwenguni. Ni cha dhamana sana kiasi cha kwamba kimezungukwa na askari wa uongo. Tunavyofikiri kunadhuru usemi wetu, na jinsi tunavyo nena kutadhuru maisha yetu.(Luka 6:45) (James 3:4-6)

"Tena angalieni merikebu; ingawa ni kubwa kama nini, na kuchukuliwa na pepo kali, zageuzwa na usakani mdogo sana, kokote anakoazimia kwenda nahodha. Vivyo hivyo ulimi nao ni kiungo kidogo, nao hujivuna majivuno makuu.  Angalieni jinsi moto mdogo uwashavyo moto mkubwa sana."

**Silaha zetu nizakuzuia maisha ya mafikira yetu na haki za agano yetu kwa kumjua yeye**

2 Wakorintho 10:3-5 "Maana ingawa tunaenda katika mwili; (maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zinauwezo katika Mungu hata kuangusha ngome) tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka dhidi ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo."

kwa vile njia unayofikiri, inaweza kukutawala katika maisha yako yote. Ndio sababu haya maandiko huongea kuhusu vita kali za kiroho kinyume kinyume na vizuizi katika mwenendo wetu na Mungu hayo yakiwa mafikira yanayoinuka.

***Kuna vita katika maisha ya mawazo yetu.***

Mungu ametufanya sisi wafalme na makuhani. Wafalme kuweza kupigana na makuhani kuweza kuwakilisha binadamu kwake Mungu na Mungu kwa binadamu.,ama kwa maneno mengine, huduma . Hatuwezi kuwa na uzima maishani mwetu ama huduma kwa wale wengine bila kujiunga katika vita vita tukilenga mafikira yetu na kufikiria maisha ya kufikiria.

## Kumjua Mungu ni chochote

***Agano agano la damu ni kuhusu kumjua yeye.***

Kujua ni neno linalodokeza mawasiliano ya kibinafsi ya karibu sana zaidi ya ufahamu wa kiakili. Ni kujua kwa njia ya kibinafsi na kwa karibu sana. Hata kama tuko katika vita kwa ajili hii. Vita vyako ndani na katika mafikira yetu. Kazi iliyongumu kwetu ni kuweka mafikira kwenye kifungo cha zile silaha Mungu ametupa. Yesualishamshinda shetani pale msalabani. Tayari ametupatia agano la damu lililokamilika. Vita vyetu hasa si vya kumshinda shetani lakini ni kuweza kulinda urithi wetu wa haki. Na kwa mengi, Yesundiye mpatanishi wa agano la damu. Yeye yuko hapo kuona kweli tumeweza kupokea mambo mazuri ya agano la damu. Lakini kumbuka jina lake ni Neno.

Wakati unapojua Yesuanawakilisha wakati, unamwona akiwa hapa duniani, mipango ya shetani yaweza kupotoshwa .ihali shetani tu akiweza kupata mafikira yako na kuweza kuyapata mafikira yako na kuweza kuyatawala hutamjua Yesuna mipango ya shetani yeweza kufaulu. Kumbuka Yesualiwaambia wengine katika Mathayo 7:23 “sikuwajua ninyi kamwe”.

***kuondolewa kwa dhambi ndio huturuhusu sisi kuweza kumjua yeye.***

Yeremia akatabiri, Yeremia 24:7 na 31:34 “ Nami nitawapa moyo, wanijue ya kuwa mimi ni Bwana; nao watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao; kwa maana watanirudia kwa moyo wao wote” “wala hawatamfundisha kila mtu jirani yake, na kila mtu ndugu yake, wakisema, mjue BWANA; kwa maana watanijua wote, tangu mtu aliye mdogo miongoni mwao hata aliye mkubwa miongoni mwao, asema BWANA; maana nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena.”

*Ikiwa wewe umetenganishwa utaishi kama mtu wa kawaida katika uhafifu wa akilia na hisia zako. Ikiwa utaweza kuvunja chochote, yeye anataka kukupa wewe ndani na kupitia uhusiano wake wakaribu kufikiri kwa dhambi*, kunaweza kutuweka mbali na kumjua yeye. Waefeso 4:1 inasema, “Kwa hiyo nawasihi, mimi niliyemfungwa katika BWANA, mwenende kama inavyoustahili wito wenu

mlioitiwa" Waefeso 4:23 inasema, "mfanywe wapywa katika roho ya nia zenu."

*Paulo aliomba kwamba kanisa litajua na kuwa na uhusiano mwema naye Mungu.*

*Waefeso 3:16-20*

*(16) Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake,kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani.*

*(17) Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo.*

*(18) Ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo na kina*

*(19) Na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.*

*(20) Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu.*

Kuadhibu kufikiri kwetu ni kazi kubwa. Kuwa mzembe kwa kazi ya Mungu katika haya maisha yetu ya kiasili. Tafadhali jua hatuwezi kujaribu kupunguza rehema na neema ya Mungu, kazi yake Mungu, kazi iliyokamilika yake Yesupale msalabani, kwa kutoa shauri mambo mengine ya wokovu kwa matendo ama kisheria. Hatudokezi kwamba Mungu amekaa nyuma akitazama vile tunaweza tenda vyema, la! Alitufanyia yote. Hata hivyo akatuonya sisi nilazima tushinde, na hili ni jambo linalotumiwa vitani. Kuzaliwa kwetu upya ni huru. Hata hivyo kukaa kwetu tukiwa tumefungwa katika maisha yake Mungu kudumisha wakati mwema na uhusiano wa karibu naye, huturuhusu kutufanya sisi wazima, kututumia kwa utukufu wake, na kuleta kusudi la ufalme hapa duniani. Vita vya kiroho vinahitajika sana katika maisha ya fikira zetu kama zimefunganishwa kwa Neno na kukataa kombora la mawazo ya shetani. Kazi ya shetani ni kuchukua mawazo yetu ili aweze kuyatoa kutoka kwa maisha yake Mungu. Fikira zetu ni kiwanja marufu cha shetani na kina matunda mengi.

**Mungu tayari ametoa suluhisho**

***Tunahitaji tu kuweka kufikiria kwetu kwake.***

Unahitaji kujua kwa kweli kwamba Mungu alifanya chochote kilichohitajika ili aweze kuponya kwa ukamilifu majeraha vyako.

Kupitia kazi kazi yake Yesu. Kifo chake, uhai, kufufuka na kupaa juu ili aweza kumaliza mengi zaidi yatosha ili uwe mzima sehemu yetu ni kuamini kweli. Kufanya mafikira yetu kuwa mapya na ya kweli ni njia ndefu na inaweza kuchukua muda. Ni halisi kabisa hata wakati ule inaonekana si halisi. Mafikira yetu yanaweza badilika . Haya mabadiliko huwa yanadhuru maisha yetu yote. Naweza shuhudia huu ukweli kwa maisha yako, na katika maisha ya wengine wengi. Mhariri wangu wa kuchangia, Micheal Vincent anashuhudia jinsi alivyoweza kushinda ngome za kuhisi mjinga, kutokamilika na kutokuwa mzuri ya kutosha.

Kutoka wakati Micheal alipoanza shule walimwelezea kutoka siku ya kwanza kuwa hataweza kusoma kama watoto wale wengine. Alipokuwa akienda shuleni na uongo ukiwa umepigwa kwa nguvu na ngome ikawa imejengwa. Mwaka baada ya mwaka Micheal akawa nyuma ya watoto wa rika yake shuleni.

Kutokana na huu mtindo wa itikadi alishindwa alipokuwa akijaribu kusoma. Akiwa na miaka 37, baada ya miaka 20 ya pombe na dawa za kulevya kupita kiasi. Micheal akajipata yeye mwenyewe akiwa katika mpango wa kiKristo kuhusu pombe na madawa ya kulevya. Moja tu katika huu mpango akaanza kutafakari na kukumbua maandiko kwanza ukweli na roho ya uasi ikataka kuishikilia kwa uongo kwamba yeye hataweza kufanya. Baada ya kusaidiwa, kutiwa moyo na maombi kutoka kwa watu wengine, kwa hu mpango, akaanza kutafakari maandiko moja kwa moja. Haikukawia sana kabla ya kuweza kutafakari zote kumi na sita ndio akae katika huu mpango.Siku moja kwa maombi akahisi amejawa na hasira. Akahis chukizo kwake Mungu kwa sababu wakati wote aliamini kwamba Mungu alikuwa na makosa kwa kumwumba.

Baaada ya kuuliza na kupokea msamaha kutoka kwake Mungu akakanusha nadhiri ile hangeweza kusoma. Tena akashukuru Mungu kwa kumuumba na akaamini Mungu hakukosea wakati alipomwumba na akapata nafasi kwamba hata kama hakuwahi kusoma kitabu yeye alikuwa jinsi Mungu alimwumba, kwa wakati huu kulikuwa na kifungo cha kiroho kiliweza kuvunjwa maishani mwake. Mungu aliweza kuutuliza moyo wake, akampa utulivu kusoma neno moja

kwa wakati na kuanza kutafakari maandiko mengi. Leo miaka saba imepita amesoma mamia ya vitabu vya wakKristo yeye husoma Biblia kila siku na hutembea kw ushindi mkuu juu ya ngome zile zilizokuwa maishani mwake.

***Ukweli halisi ni kigeuzi***

kwa mfano, Wagalatia 2:20, "Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilionao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu."

Warumi 6:3-4, "Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesutulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyotufunika katika watu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.

Sio tu dhambi zako ziliweza kuchukuliwa, lakini tena mtu yule aliyetenda dhambi aliwekwa katika kifo na ukaweza kufufuliwa naye Kristo na sasa ameketi na yeye katika makao ya mbinguni. Uliweza kuzaliwa mara ya pili katika kabisa watu wapya. Jamaa ya watu.wakati utakapoanza kuamini hu ukweli, mawazo yako yatakuwa yanafanywa upya. Wakati hili limetendeka hii njia ya uponyo wa ndani anaweza kuwa na uhuru kufanya kazi yake ndani yako.

Hii ni kazi nyingi na ya ndani kuliko uponyaji wa sikitiko. Hata wale wasioamini wanaweza kupokea uponyo wa masikitiko. Ilhali ni mwana tu wa Mungu aliye mwanafunzi anaweza kubadilishwa kwa njia isiyo ya kawaida. Wakati akili zake zimefanywa upya ndio ziweze kuamini, sita kiakili, lakini kwa ufufuo wa kuelewa, kwamba wewe umeweza kusulubishwa naye Kristo kwamba wewe kwa uhakika ulikuwa naye wakati alipigiliwa misumari pale msalabani, sasa utaweza kupata uhuru halisi.

**Mifano ya mawazo haribifu**

Tunaweza kupokea mawazo

1. Kinyume na tabia nzuri za Mungu.
2. Kinyume na utambulisho wa Kristo.
3. Kinyume na wengine.

Kumpenda Mungu kwa akili zako ni amri, Yesuakasema, Mathayo 22:37-39, “Akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii; “mpende jirani yako kama nafsi yako.”

**Mawazo yasiyotaratibu hutoka wapi?**

Mawazo mengi huja kutoamrishwa kutoka kwenye uhusiano uliovunjika, mara nyingi kutoka kwa baba. Hali zetu za awali na hata sasa zikiwa mbaya, zaweza kutupa mawazo ya kinyume. Mawazo ya kuharibu yanaweza kuja kutokana na mafikira yetu. Yale tunayotazama kwa macho yetu na kusikia na yale tumeamua kuweka akilini mwetu katika jeshi la shetani laweza kupituga ikiwa amezilenga akili zetu.

Tunapookolewa naye Yesu, roho zetu hufanywa upya na nzima. Wakati tutakapoenda mbinguni mili yetu itafanywa upya na nzima. Ilhali wakati tuko hapa duniani tunakimbizana na uponyo na ufanisi wa nafsi zetu, ikiwa hiari yetu, akili na uhalisi wetu. Warumi 12:1-2, “Basi, ndugu zangu, nawasihi kwa huruma zake Mungu , itoeni mili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, na kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.” Inaifanya kuwa wazi ya kwamba sisi tunafa tufuate kufanywa upya katika akili zetu.

Tunapozaliwa kuwa kiumbe kipya, sisi hupitia alama za kimwili na mtu wa kale ndani ya mafikira yetu. Sisi si watu wawili sawa kama vile wengine hujaribu mafundisho, si watu wawili wanao kaa ndani yetu. Sisi ni watu waliofufuka, kiumbe kipya kwa Kristo. Ilhali ‘utu wa kale’ una acha mafikira ya kale ndani ya mawazo yetu na hapo ndipo vita vimechacha. Mungu anataka yafanywe upya, shetani naye anataka yatutawale.

**Teka nyara mawazo yako.**

***Wakati unaposikia neno, mbegu inapandwa, huo ndio ukweli wa maisha!*** Maneno huwa mafikira na tena huzaa matunda. Shetani hupanda maneno yale huja kuwa mafikira.(Mathayo 13:25) Haya mawazo baadaye huzaa matunda ya kishetani.

***Hapa kuna mambo rahisi ya kuweza kuteka mawazo yako nyara na kufanya upya akili zako.***

***1. Teka nyara akili zako***

Viwanja vya ndege vya kisasa vinamahali panaposhughulikia usalama ambapo kila mtu na kila kipande cha mzigo hukaguliwa ili kuona iwapo kuna silaha hatari kabla ya kuabiri ndege. Unatakiwa kufanya vivyo hivyo. Wakati wazo fulani linapoingia kwa mawazo yako ngojea na ujiulize, je wazo hili nilakiungu? Je wazo limetoka kwa shetani au kwa mwili wangu? Hapa unakata kauli ya kuambia wazo lile, “si kubali uingie, na kuteka nyara, nakuondoa katika jina la Yesu!”

Baada ya mazoezi machache kutakuwa na nafasi njema ya kutambua mawazo yale yametoka kwa Mungu. Mara nyingine kwangu nahisi kwamba ni umeme ambao umepita katika moyo wangu.

***Badilisha mawazo yako kwa mawazo ya kiungu.*** Huwezi tu wacha mawazo yawe wazi lazima uyajaze na mambo mazuri.

***2. Anza kutafakari Neno la Mungu,*** mwulize akusaidie kushika maandiko. Kisha andika chini na ujifunze kwa moyo. Yatafune na uyatafakari mchana kutwa.Tafakari hadithi ya Biblia na uiwaze mifano na njia yetu ya kufikiria, hii ndiyo sababu maandiko yetu ambayo tunatumia Wakorintho wa pili 10:3-5 ambayo imenakiliwa hapo mbeeleni inasema tuangushe chini mawazo ama kwa tafsiri zingine neno mabishano. Neno hili karibu kufanana na mawazo. Mawazo yetu hufanya kupitia picha ama mawazo badala ya maneno.

***3. Nena Neno.*** Ifanye iwe tabia kunena tabia kunena neno la Mungu kwa sauti, huwezi kuwacha mawazo machafu tena unene kitu tofauti. Hebu jaribu.

## Mukhtasari

Kwa mukhtasari Yesualitupa angano la Adamu ambalo linaondoa dhambi zetu. Faida moja ya hii ni ilituweze kumjua kwa njia ya karibu. Wakati tuko katika hali ya sasa ya kumjua nguvu zake hufanya kazi ndani yetu, na kwa sababu ya wengine duniani. Shetani

anajua kwamba mawazo yetu yanaweza kufanya tusipate nguvu za Mungu, hivyo yeye huingilia sana mawazo yetu.

**Niliyateka nyara mawazo yako. Je wewe utanifanyia hivyo.**
Wafilipi 2:5 "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu."

Mistari hii inayofuata imezungumzia kuhusu akili ni kunyenyekea na shauku ya kuuchukua msalaba wake. Ni lazima tuchukue msalaba wetu wakati tunakuwa na fikira ambayo imepita kiasi kuweza kutawaliwa.

**Dondoo kutoka 'Purpose Driven Life Daily Devotions.**

Purpose DrivenLife.com a ministry of Saddleback Church
1.Saddleback Pkwy Lake Forest, CA92630(800) 633-8876

*"Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo; Maana ndiko zitokako chemchemi za uzima" Mithali 4:23*

*Moja wazo utambulisho wa 'kisaikologio' kwa muda uliopita ni kwamba kubadilisha jinsi ya kufikiria kwako.*

*Kwa miaka elfu iliyopita, Solomon aliweza kujua wakati alipoandika Mithali 4:23 "Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo; maana ndiko zitokako chemichemi za uzima"*

*Biblia inasema mawazo yetu hutawala eneo si ndani ya maisha yetu."*

*Kutafsiri kwangu kunatawala hali yangu. Sio vile hufanyika maishani mwangu kunajalisha lakini ni jinsi utachagua kuiona hali hiyo. Jinsi ninavyotenda yategemea kama hali itanifanya niwe na uchungu ama niwe mwema, ikiwa naweza kuona chochote kama kizuizi ama nafasi ya kukua- kizuizi ama ngazi ya kupanda. Yakobo 1:2-4, "Ndugu zangu , hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali, mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno."*

*Maoni yangu hutawala mwinamo wangu. Kwa maneno mengine mawazo yangu hudhuru namna yangu huamua hisia zangu. Ninahisi mwinamo ni kwa sababu nimechagua kufikiri mawazo ya mwinamo kuhusu kazi yangu, familia ama chochote kile. Wakati huwezi kutawala hisia zako. Unaweza chagua utafikiri nini na hayo ndiyo utatawala hisia zako. Zaburi 55:2, "Unisikilize na kunijibu, nimetangatanga nikilalama na kuugua"*

*Itikadi zangu kutawala tabia zangu. Sisi hutenda kulingana na itikadi zetu, hata kama yale mawazo ni ya uongo. Kwa mfano kama mtoto,ukiamini kivuli kwa chumba chako cha kula kilikuwa cha jitu, mwili wako utakuwa na hofu. Hata kama si ukweli ndio sababu ni ya muhimu sana kujua ya kwamba unapata habari iliyo kweli msukumo wake kuhusu wewe mwenyewe, kuhusu maisha, na kuhusu Mungu, hutawala kutenda kwako.*

*Yohana 8:31, "Basi Yesuakawaambia wale Wayahudi waliomwamini, Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli"*

*Jinsi mimi hunena kujihusu kunatawala jinsi ninavyojiona. Mara nyingi huongea kujihusu kwa wewe mwenyewe kwa kutojua. Wakati unapoingia chumba kilichojaa wageni, wewe hujifikiria nini? Kueneza udhabiti wako, ni lazima uamue na uwache kujiona duni.*

*Mithali 23:7, "Maana aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo. Akuambia, Haya, kula, kunywa; lakini moyo wake hauwi pamoja nawe"*

*Hiari yangu hutawala uwezo wa kutenda kwangu. Washindi hutarajia kushinda jinsi wanavyojiona. Hutawala kwa kufanya kwako. Mohammed Ali alikosa katika michezo miwili kwa kazi yake. Baada ya hayo, alisema jambo hawajawahii kulisema maishani mwake.' ikiwa nitakosa ama nitashindwa katika vita hii..... Marko 9:23, "Yesuakawmambia. Ukiweza! Yote yawezekana kwake aaminiye"*

*Je unadhani utawahi kile unajitahidi kuwa. Kwa maneno mengine ndoto zako zitategemea mwisho wako. Ili uweze kumaliza jambo ni lazima kwanza uwe na kusudi; lengo, tumaini, na maono.*

*Mithali 29:18, "Pasipo maono, watu hukosa kujizuia; Bali ana heri mtu yule aishikaye sheria"*

*Kuweza kurarua chini ngome hizi inaweza kuchukua miaka mingi. Inategemea kidonda kimeweza kukatwa kiasi gani, na ni kwa muda gani, umekuwa ukiamini hii ngome. Tunaweza kushuhudia kwa kuchukua na kuteka mawazo nyara kwa haraka kwa kutafakari Neno, kumbuka kwa moyo, kila siku kuweza kutembea naye kwa mienendo yetu kwake Mungu hizi ngome zitaweza kuharibiwa haraka. Jinsi tu unavyo mwamini Mungu na kumtumaini yeye na kuruhusu upendo wake ukusaidie kuona ukweli utaweza kushinda. Palipo na roho wake Mungu kuna uhuru.*

# Sura ya 14
# Kuishi Jinsi Ulivyo

Hauwezi kuwa huru ikiwa huishi kulingana vile ulivyo

Katika kitabu tumeweza kupatiana nafasi kupitia kila mlango, kuweza kujua toleo za Mungu za uponyo wa ndani. Tumehimiza nguvu zake za msalaba kuwa mahitaji ya uponyo wako na kubadilika kwa maisha yako. Sasa katika hili somo lilopita tunahimiza kujijua wewe ni nani ndani ya Kristo kwa imani ya Neno la Mungu tumeweza kuelezea kupata ufunuo wa ndani kwa hili utaanza kubadili mawazo yako ni lazima yafanywe upya. Badili maisha yako ya nje.tena tumeweza kuhimiza ni lazima kabisa uwe umejitolea na uwe wazi kwake Mungu ndio uweze kuwa na aina hiyo ya imani ili uweze kuona na kuamini, kweli umeweza kusulubishwa naye YesuKristo na amefufuka na wewe tayari. Tena tunahimiza kwamba kufikiri kwako ni lazima yafanywe upya ili ukweli uweze kuona ufufuo huu wa ajabu.

Ilhali tunaweza rahisisha nguvu kuu zake Mungu ikiwa hatutafanya mazoezi. Kutembea ndani ya Roho ama kwa maneno mengine kuamua kuishi maisha ya upendo. Wagalatia 5:6, "Maana katika Kristo Yesukutahiriwa hakufai neno, wala kutokutahiriwa, bali imani itendayo kazi kwa upendo"

**Usikuwe mwangalifu kupita kiasi**

Kama mengi ya mambo ya kiroho, kutembea ndani ya Roho kunaweza kosa kueleweka kutokana na tofauti mbili za kupita kiasi, zote mbili zinaweza sababisha kutofaulu kukuu katika maisha yetu. kupita kiasi ni kuisha maisha kama kana kwamba chochote kimeenda maishani mwao. Watu wengine hufikiri kwamba upendo wake Mungu na neema ya Mungu huwaruhusu hao kutoka kuweza, kufanya ama kuongeza nguvu zao ndio wawe washindi na kurusu Kristo aweze kuumbika ndani yao. Huwa wanakosea hii neema.

Kupita kiasi kwingine ni kuishi maisha yako katika ukamilifu ama utupu. "Hawa watu wanatambua kwamba Mungu angetaka

wabadilike lakini wakati wanafanya makosa dhambi na kutokubali kubadili wanahukumiwa, kuhisi kujawa kabisa na kukata tamaa.

***Ukweli umeelezwa katika Warumi 8.***

Katika warumi 6, Paulo aliandika kuhusu kazi ya ajabu yake Kristo iliyoweza  kukamilika. Katika Warumi , Paulo tena akaendelea kusema kuwa hangeweza kuishimaisha kana kwamba kazi yake Kristo haijamalizika. Tena katika Warumi 8 akapeana suluhisho.

Warumi 8:1-6

*(1) Sasa basi ,hakuna hukumu ya adhabu juu ya walio katika Kristo Yesu.*

*(2) Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesuimeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti.*

*(3) Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili.*

*(4) Ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yenu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho.*

*(5) Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili, bali wale waifuatao roho huyafikiri mambo ya roho.*

*(6) Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani.*

Tazama kwamba alisema “tembea” kulingana na mwili au Roho. Kutembea ni kitendo katika hali ya kuendelea. Inamaanisha kuendelea kuishi katika njia fulani ama nyingine. Haijasema ya kwamba ukikosea utahukumiwa.....Paulo haongei kuhusu ukamilifu, lakini usiwahi kufa moyo. Utaona maelezo ya kutembea katika Roho hapo chini kuwa tutafanya makosa. Hata kama Mungu yeye huona kujaribu kwetu yeye huona dani ya mioyo yetu vile tunavyosukuma ilikuweza kumpendeza, yale anaona kutubu kwetu wakati tunapoanguka na anasema “kuja sasa inuka, ninafuruhisha ninapendezwa nawe, utafaulu.”

**Wakati uchungu ulio ndani yako hupita uchungu wa kubadili sasa unaweza ponywa**

Hili ni wazo mimi husikia mara nyingi kutoka kwa Michael na Karen Vincent, marafiki wangu na wa hariri wenzangu. Sasa tunajua Mungu ni nani tumeweza kujua ya kwamba Yesu alitulipia deni kwa uponyo urefu wa ndani na tunajua ni nini Yesu alituumba tuwe ndani yake. Tunahitaji kubadili mienendo yetu kwa kukubaliana wewe kweli ni nani. Si ya kutosha kwamba Mungu ametenda mambo haya yote makuu kwetu sisi, ikiwa hatuyafanyi kila siku, hata kila wakati, chaguo kwamba tutabadili mienendo yetu ili tuweze kulingana na ukweli wa usawa wetu.

Kubadili kukuu ni lazima uweze kuamua na ufanye ushirika na Mungu na Neno lake. Siongei kuhusu kuweza kuombea mahitaji yako. La hasha, naongea kuhusu kuweka ndani kabisa katika Neno lake, na kutoa moyo wako uwe wazi kwake Mungu. Fanya haya mazoezi kila siku ya kusifu na kushukuru na wakati mwingine rekodi wakati wako na yeye, unaweza andika, hiki ndicho kile tunachokita kitabu cha kunakili mambo kila siku. Imani huja pekee kwa kusikia Neno lake Mungu. Wakati unaposikia Neno,ufunuo uko na mwanya wa kuweza kulia wewe ndani ya moyowako.wakati hili linatendeka mwangaza wake unafanya miujiza ndani yako na kwako wewe.

***Onyo!***

WaKristo wengi hawachukui maisha yao ya kuomba, wakati wao wa kunena naye Mungu, kwa kuajibika. Naweza gundua hawa watu wale wanajaribu kuenenda katika Roho. Wanaonekana kuwa na “harufu”kuhusu hao. Haya sinenei wale waaminio, wale hawajakomaa ama waamio wachanga, ama wale wasio elimika. Kwa neno lake Mungu, mara nyingi wanaweza kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu tena waaminio walio komaa, kuchukua wakati na kuweza kusafisha moyo na kunena naye Mungu ndiye huleta uzima na hii ndiyo dhamana ya kuishi. Nayo hii ndiyo itaweza kuhudumia mahitaji yako yote. Hii ndiyo itatupa furaha.

***Yesu anahitaji kuumbika ndani yako.***

Wakati unahitaji Roho Mtakatifu kuliko maisha yenyewe, sasa hapo Kristo ataumbika ndani yako. (Wagalatia 4:19) inasema, “Vitoto

vyangu, ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu." Oswald Chambers akaandika mafundisho siyo Kristo kwangu mimi, mpaka nitie bidii na kuwa Yesuameumbika ndani yangu.

***Tumeokolewa kwa Imani***

Warumi 4:2-6, "Kwa maana ikiwa Ibrahimu alihesabiwa haki kwa ajili ya matendo yake,analo la kujisifia; lakini si mbele za Mungu. Maana maandiko yasemaje? Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki, lakini kwa mtu afanyaye kazi, ujira wake hauhesabiwi kuwa ni neema, bali kuwa ni deni. Lakini kwa mtu asiyefanya kazi, bali anamwamini yeye ambaye amhesabia haki asiyekuwa mtauwa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki. Kama vile Daudi aunenavyo uheri wake mtu yule ambaye Mungu amhesabia kuwa na haki pasipo matendo."

***Imani yetu imekamilika na kutiwa sahihi na tendo***

Yakobo 2:14, "Ndugu zangu, yafaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo imani, lakini hana matendo? Je! Ile imani yaweza kumwokoa?"

Yakobo 2:17-18, " Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo imekufa nafsini mwake. Lakini mtu atasema,Wewe unayo imani, nami ninayo matendo. Nionyeshe imani yako pasipo matendo, nami nikuonyeshe imani yangu kwa njia ya matendo yangu."

***Heshima kwa mfalme inahitajika.***

Yohana 14:21, " Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake."

Biblia imeweka wazi kwamba sisi tumeokolewa kutoka kuzimu tukiwa humu duniani na hata wakati tuko hapa ulimwenguni, wakati tunapofanya Yesukuwa Mungu wetu kumfanya yeye Mungu inamaanisha kupeana, kujitegemea kwetu na kumtii kama mfalme. Tazama katika sura iliyo hapo juu kwamba tunapozidi kumtii ndio anajidhihirisha. Kwa ukuu ndani yetu, na kuwa halisi kwetu sisi. Na sasa inakuwa mtindo unaoendelea,tunatii, anajidhihirisha yeye mwenyewe, tena tunamwona zaidi na kumtii yeye zaidi. Punde si punde tunakuwa moja naye na anatukuka kupitia matunda tunayozaa.

**Jihadhari kwa kumtafuta Mungu wakati wako wa starehe tu.**
Nimejua watu wale wameweza kukutana na Mungu, lakini wakachukulia kwa urahisi kwamba, kwa kuwa Mungu ni upendo sasa atakuwa sawa na sisi, vile tu anaweza kutufariji sisi tuhisi kama ni lazima.

***Kutoshereka huja tu baada ya hofu yake Mungu***

Matendo ya Mitume 9:31, "Basi kanisa likapata raha katika Uyahudi wote wa Galilaya na Samaria, likajengwa, likiendelea na kuongezeka katika kicho cha Bwana, na faraja ya Roho Mtakatifu."

***Kazi zetu hasa si kazi zetu, ni kazi za neema kwa Kristo kuishi ndani yetu na kupitia sisi.***

(Wafilipi 2:12-13). "Basi, wapendwa wangu, kama vile mlivyotii sikuzote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi sana mimi nsispokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu,kutimiza kusudi lake jema."

***Imani hufanyakazi kupitia upendo.***

Unaweza soma Neno la Mungu usiku na mchana, na ulitafakari kuhusu na uungame mpaka upite kabisa, lakini ikiwa huenendi katika upendo ni bure.

***Vunjvunja miungu yako***

katika kitabu cha Waamuzi 6-8, Gideoni na wana wa Israeli walikuwa katika kifungo hata wakati ule waliishi katika nchi yao ya ahadi. Mungu akaja na akawa na kazi nyingi pamoja na Gedeoni akaweza kumwondoa ili aweze kuwakomboa wana wa Israeli. Mungu akaweza kueneza urafiki wa karibu sana na Gideoni na akaweza kumwonesha agano la damu. Gideoni akaanza kubadili hali ya kufikiri kutoka kwa maskini aliyeshindwa na kupata kuwa shujaa mkuu wa vita kwake Mungu. Ilhali Gideoni alikuwa achukue usukani na kuharibu miungu ya familia kama Gideon hataweza kusimama kinyume na adui wako mpaka utembee katika upendo na uwache njia zako za kale.

**Kuenenda kwa Roho**

Wagalatia 5:16 inasema, “Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtatimiza kamwe tamaa za mwili” Waefeso 4:1 inasema, “Kwa hiyo na wasihi, mimi niliye mfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa.”

Warumi 8:1 inasema, “Sasa, baasi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu”

Baada ya kusoma Warumi 8:8, “Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu” utapata ya kwamba ameongea kuhusu sisi kuweza kutembea kulingana na Roho lakini si kulingana na mwili. Anaelezea ya kwamba kuna ushindi katika mienendo mingine na kushindwa kabisa kwa mienendo ile mingine.

Wagalatia 6:7-8, “Kwa kuwa yeye aliyekufa amehesabiwa haki mbali na dhambi. Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye.”

Kuenenda na Roho ni rahisi, lakini kuna njia tofauti ya kuishi na njia rahisi najua ni kuwa sawa naye Mungu kila siku. Ni hatua na huenda hivi.

1. Wewe endelea kusoma Neno lake Mungu (kioo) na uweze kumwuliza Mungu jinsi ya kuishi. Mwulize na utafute ni kiwango gani chake anataka maishani mwako kwa mfano linasema hakuna kudanganya kuweza kuwasaliana na marafiki wako kwa upendo, kunyenyekea chini ya mamlaka, kutenda familia yako kwa upendo, usiwe mlevi, usiwe mchoyo, usikasirike, kila wakati samehe hata kama ni nini? Na mengineo.

2. Weza kuamua kuishi jinsi Mungu anataka wewe uishi kwa upendo, ukijua ya kwamba ni Mungu pekee anayeweza ishi maisha ya dhamani yake.

3. Unapoanguka utaanguka, kuwa kabisa mwaminifu kwako wewe opendo, ukijua ya kwamba ni Mungu na wale wengine wamekuzunguka ama wako karibu nawe, tubu (Geuka) kwamba ufalme wa Mungu umekaribia (karibu sana)

4. Ungama dhambi zako kwa Mungu (1 Yohana 1:9), “Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.”

5. Ungama jinsi Neno la Mungu linavyosema kuhusu hali yako ya wema. (Wagalatia 2:20) Ambayo yasema, "Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu."
6. Ukiendelea kuishi hivi,tabia hizo za kale na hali ya kale ya kutenda dhambi, inaanza kupotea. Neema yake Mungu inachukua usukani na anakupa wewe tabia yake Mungu badala ya tabia yako ya kale.
7. Neema inaingia kwa ajili ya dhambi zako. Wewe huwezi kuwa mwenye haki kwa yale mambo unatenda., ama ulitenda, kwa hivyo ndivyo haki yako iko, ilikuwa tu uchafu ndani yake utakapoenda kwa Roho, Mungu hukuypa nguvu za kushinda na kushughulika kila matukio ya dhambi imetendwa na ili kwamba upokee baraka usizostahili.
8. Si neema pekee huondoa dhambi zako, si tu Mungu hukupa wewe baraka zile hukustahi, lakini neema ile uliyoipokea ni nguvu hasa za kuondoa dhambi zako, ama shida unayoishughulika wakati huo. Zekaria 4:7 ambayo inasema, "Nani wewe, Ee mlima mkubwa? Mbele ya Zerubabeli utakuwa nchi tambarare; naye atalileta lile jiwe la kuwekwa juu kabisa pamoja na vigelele vya , Neema, neema, ilikalie". Mungu hunena "Neema" kwa hali yako na mlima unaweza kuondolewa.

**Vumilia: kuna habari njema katika sura hii.**

Wakati unapoungama dhambi zako kwa Mungu, zinaenda hadi kwa msalaba wake Yesu, na kutoka hapo kwenda kaburini. Huo ni ufufuo kweli.

Wakati unapopanda dhambi zako, zinaenda mpaka kaburini na Mungu anaifufua kwa jambo maridadi sana, usawa kama wa tabia zake.

1 Wakorintho 15:42 inasema, "Kadhalika na kiyama ya watu. Hupandwa katika uharibifu; hufufuliwa katika kutoharibika"

Wagalatia 6:8 inasema, “Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho katika Roho atavuna uzima wa milele.”

Paulo akaelezea kwamba tunaweza ama kutana na hizi nguvu za ufufuo tukiwa tungali na mwili huu.

“Ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake. Ili nipate kwa njia yote kuifikia kiama ya wafu” (Wafilipi 3:10-11).

***Hii inafanya kazi kwa njia gani?***

Hii inafanya kazi kwa njia tofauti maishani mwetu, mpaka kupitia huzuni, ugumu wa kushinda mateso na majaribu maishani mwetu. Hata kama hapa nataka kukuonyesha jinsi ya kuenenda kwa Roho , kuweza kutumia nguvu za Mungu za ufufuo kwa ajili ya dhambi na hali yetu ya dhambi.

**Sasa hapa kuna orodha ambayo tumetumia katika somo letu. Mto Unaotiririka kama mwongozo wa kuruhusu Mungu aweze kufunua hisia na matendo yaliyo ndani yetu ambayo hayaambatani na tabia ya Mungu.**

**Kujichunguza Kiroho**

• **Upendo -** Je unawatendea wengine kwa upendo wa Mungu usio na

• **Ubinafsi -** Kuweka mahitaji yako mwenyewe juu ya mahitaji ya wengine. Upendo hujishughulisha na ustawi wa mtu mwingine – je wewe unajijali mwenyewe zaidi na kujali tu jinsi unavyojisikia?

• **Kuiba -** Je unaweza kukumbuka fedha ulizopokea kwa mali iliyokuwa si.

• **Kulaghai -** Je, ulipata kitu chochote kutoka kwa mtu fulani kwa njia isiyo

• **Kusema uongo -** Aina yoyote ya udanganyifu wa kukusudia

• **Kashfa -** Kumsema vibaya mtu fulani. Kumkashifu mtu siyo lazima useme uongo - Je, umewahi kuwasema wengine bila upendo?

• **Ufisadi -** Je, unajisikia hatia kuamsha tamaa usizoweza kuzitimiza kwa haki? Ufasiki, uchafu wote, hata kama ni juu ya mwili wako

• **Ulevi -** Utumiaji wa madawa ya kulevya, karamu za ulevi.

• **Lugha chafu au matusi -** maneno maovu, mazungumzo mabaya au yasiyo na maana, uchafu, mazungumzo machafu, ya kipumbavu, ya kipuzi, ya

• **Wivu -** Kwa kawaida mahali penye mazungumzo yanayohusu makosa au kushindwa kwa wengine, kuna wivu ulioji.cha.

• **Utovu wa shukrani -** Ni mara ngapi wengine wamekufanyia vitu lakini

• **Hasira -** Je, umewahi kukasirika?

• **Kulaani -** Umetumia lugha ya matusi.

• **Utani -** Maneno yasiyohitajika, maongezi ya kipumbavu, kuongea na kutenda kama punguani. Masihara na mzaha na utani wa vitendo unaoelekea kudhoo.sha viwango vitakatifu na vyenye thamani vya maisha. Je, umewahi kulitania kabila fulani au sehemu fulani ya ulimwengu, taifa au mkoa katika nchi yako, au mwanasiasa fulani? Mizaha ya kikabila au kimikoa haina nafasi katika utakatifu.

• **Ukali -** Ulijibu mapigo, ulinung'unika au kurudisha mabaya kwa mabaya?

• **Tabia -** Je, kila wakati una uchu upitao kiasi? Na vipi kuhusu tabia yako ya ulaji?

• **Hali ya kuwa shingo upande -** Unaweza kukumbuka nyakati ambazo kwa makusudi kabisa ulikwepa kufanya wajibu wako kwa ukamilifu?

• **Kizuizi -** Umeharibu imani au matumaini ya wengine kwa kupoteza bure muda wao? Je, umemghilibu mtu aliyekuwa na imani na wewe?

• **Unafiki -** Je, maisha uliyoishi siku za nyuma, yamewafanya baadhi ya watu waone kwamba yale uliyoyasema juu ya Kristo na Injili yake ni ya uongo?

• **Kuvunja nadhiri -** Je, kuna nadhiri yoyote uliyoweka mbele za Mungu ambayo hukuitimiza?

• **Kutokusamehe -** Je, una kinyongo au uchungu dhidi ya mtu mwingine, rafiki au adui?

• **Mafarakano -** Misuguano, roho ya kuwa na vikundi vinavyotofautiana.

• Kutamani, kuishi kitajiri na kutapanya mali, ulafi, Kutumia pesa kupita kiasi kwa kununua vitu madukani. Kupoteza muda bure.

• **Kutowatendea vyema**, au kwa upendo na heshima, wake, waume, watoto na wazazi.

**• Kutoridhika,** kuwa na wivu kwa sababu wengine wana vitu lakini wewe huna.

**• Kuabudu sanamu** - Shauku yoyote katika maisha yako inayozidi shauku ya kuishi na Mungu.

**• Ugomvi -** Umechochea ugomvi kwa maneno yasiyohitajika?

**• Uchawi -** Kumtawala mwingine kwa hila ili kutimiza haja zako.

**• Kuasi mamlaka** - Mkuu wako wa kazi, mwalimu, mzazi, kiongozi wa kiroho, nk.

**• Kuupenda ulimwengu -** Pamoja na: tamaa za macho - unasoma au kutazama nini? Tamaa za mwili - unatamani nini? Kiburi cha uzima - Ni jambo gani katika maisha unalo.kiri kwamba unaweza kulifanya bila Mungu kuhusika? - Kujifanya kuwa mkubwa au mdogo kuliko jinsi ulivyo kwa njia ya mawazo au kwa kuishi.

**• Kiburi -** ni dhambi kubwa kuliko zote. Chunguza maeneo haya.

- Je, unaangalia tu kushindwa au makosa ya wengine au unajishughulisha tu na mahitaji yako ya kiroho?
- Unajihesabia haki na kuwakosoa wengine au una huruma na moyo wa kusamehe, ukitafuta yaliyo bora kwa wengine?
- Je, unawaangalia wengine kwa dharau au unawaheshimu wengine wote na kuwaona bora kuliko wewe?
- Je, unajitegemea na kujitosheleza mwenyewe au unawategemea wengine na kutambua kwamba unawahitaji?
- Ni lazima udumishe hali ya kuwatawala wengine au uko tayari kuacha kutawala?
- Je, ni lazima uthibitishe kwamba uko sahihi, au uko tayari kuiachia haki ya kuwa sahihi?
- Una roho ya kuhitaji tu au roho ya utoaji?
- Unatamani kutumikiwa au una hamasa ya kuwahudumia wengine?
- Unatamani kupandishwa cheo au unafurahi wengine wanapopandishwa cheo?
- Unahitaji kupewa sifa au unafurahi wakati wengine wanapotambuliwa?

• Unasikia kujiamini kwamba unajua mengi, au yale ambayo bado hujajifunza yanakufanya uwe mnyenyekevu?
• Unajifahamu jinsi ulivyo au hujishughulishi na maisha yako kabisa?
• Unawaepuka watu au unatafuta kuwa karibu na wengine? Uko tayari kuchukua jukumu la kuwapenda watu kwa moyo?
• Unafanya haraka kuwalaumu wengine au uko tayari kukubali kuwajibika?
• Wewe ni mtu usiyetaka kukaribiwa na wengine au ni mtu rahisi kuwasikia wengine wanapokusihi?
• Wewe ni mtu unayejitetea unapokosolewa au unakubali kukosolewa kwa unyenyekevu na moyo mweupe?
• Unajishughulisha kutafuta kuheshimiwa au kuwa kama ulivyo?
• Unajishughulisha na yale ambayo wengine wanafikiri au yale anayofikiri Mungu?
• Unajitahidi kudumisha hali yako au hadhi uliyo nayo?
• Je, unaona vigumu kuwashirikisha wengine mahitaji yako ya kiroho au uko tayari kuwa wazi?
• Unajaribu ku.cha dhambi zako au uko tayari kuonekana wakati unapokosea?
• Unajisikia tabu kusema, “Nilikosea, tafadhali nisamehe”?
• Unapoungama dhambi, unaungama kwa ujumla, au unakiri na kuzitaja kabisa dhambi zile ulizotenda?
• Unajutia dhambi zako unapokamatwa au unasikitika kwa kuzitenda na unafanya haraka kutubu?
• Wakati hali ya kutoelewana au migongano inapotokea, unangojea wengine waje kuomba msamaha au wewe ndiye unayeanza kufanya hivyo?
• Je, unajilinganisha na wengine na kujiona kwamba unastahili heshima au je, huwa unajilinganisha na utakatifu wa Mungu na kusikia hitaji kubwa la kupewa rehema?
• Je, una.kiri una mambo machache au huna kabisa mambo ya kutubu au kila siku una moyo wa toba?
• Je, una.kiri kila mtu anahitaji uamsho au kila siku unasikia hitaji la kupata upya ujazo wa Roho Mtakatifu?

- Unajivuna unapokaa na Mkristo mpya au unafurahia ari yake? Uko tayari kujifunza kutoka kwake?
- Je, unaogopa unapokaa na Mkristo aliyekomaa zaidi yako, au una njaa ya kujifunza mambo mbalimbali yanayotokana na uzoefu wake?

**Sasa unaweza kupanda mbegu ya kuungama ndhambi zako na utubu, tena tarajia kuvuna, ufufuo wa uhai wa Yesu kama malipo!**

**Pahali pengine unaweza pata ukaguzi wa ndani wa kiroho uko kwa Daily Moral Inventory by Dunkin.**

Hapa kuna tovuti ya Daily Moral Inventory chart.

http:/www.isob-bible.org/freetobe2008/dailymoralnew.pdf

# Sura ya 15
# Vita ya Kiroho

Hauwezi kuwa huru kama huijui mikakati ya shetani

**Tunahitaji kujuea ya kwamba tunaishi katika dunia ndani ya dunia.**

Hii dunia tuionavyo ni tu giza, inajihidhirisha kwa ukweli wa ulimwengu usioonekana na kwamba tunaweza ona kwa macho yetu ya kiroho wakati Mungu anayafungua kwetu sisi.

Ndani ya huo ulimwengu wa kiroho kuna Mungu na mapepo, mashetani na malaika, kuna hilo eneo ama hali ya ulimwengu unaotawaliwa naye shetani. Hii ni halisi. Ikiwa tunaendelea kujaribu kutawala na kufanya huu ulimwengu unaonekana, sisi ni duni kwa nguvu zetu, sisi ni lazima tujue ya kwamba, tuwananchi wa ulimwengu wa kiroho kwanza. Katika huo ulimwengu wa kiroho kwanza.

Katika huo ulimwengu wa kiroho sisi zote huanza kama wanachi wa hali ya ulimwengu, ufalme wa shetani ilhali Mungu yeye hutupa chaguo kuwa wananchi wa mbinguni na kuingia ndani ya ufalme wake Mungu.

Moja tu,tunapokuwa wananchi wa ufalme wake Mungu, tena ni lazima.

**1.Tujue sisi ninani** (Keti Waefeso 2:6)

**2.Tuishi kulingana na sisi ni nani?** (Tembea Waefeso 4:1)

**3.Na mwishowe , tujue ya kutenda kwa adui wetu wa kiroho Shetani** (Simama Waefeso 6:11)

Tukijaribu kutoka kwa mambo haya matatu hatuwezi kuishi kulingana na vile Yesualipanga tuweze kuishi. Somo la vita za kiroho,ufalme wa kishetani na mapepo zimeenea, na hatutaweza kwa kujaribu kulifanya hili somo kuyahusu yote. Pengine tungetaka kupeana jambo lote ama mambo yote kwa kufanya na vitendo kwamba sisi sote tunahitaji kujua hili. Kuna urahisi wa kitoto tungetaka kupeana.

**Ndondoo kutoka Watcham Nee, "A Table in the Wilderness"[21]**

*"Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani" Waefeso 6:11*

*'Kusimama' ni kitendo na inamaanisha "shika eneo lako" si ya usemi wa kisasa, ama amri la kwenda kuvamia jimbo la kigeni ndio uweze kukaa na kuliteka. Mungu haja twaamuru tufanye hivyo. "Simama" inadokeza ya kwamba, hilo eneo linaletewa furugu na shetani ni lake Mungu aliyebeba chukizo kwa ufalme wa shetani, ndiyo faida kutoka kifo na ufufuo, ushindi mkuu. Leo tunapigana vita kuweka na kuimarisha ushindi alioupata pengine hii ndiyo sababu silaha imeelezwa hapa kwa kujikinga kukuu. Kwa kuwa Jimbo lilikuwa lake. Tunapigana ili kuweza kupata eneo la kusimama. Tunahitaji tu kushika dhidi ya wajaribu wote.*

**Yafuatayo ni mambo ya kawaida kwa njia zile shetani hufanya, na mengine ya hatua halisi sana unaweza chukua ili uweze kujiweka wewe mwenyewe salama kutokana na ujanja wake.**

***1. Sisi huishi katika ulimwengu ulioanguka kuhisi "hicho kishindo"***

Mambo hutendeka wakati mwingine , inaweza kuwa sio wewe umelengwa na shetani na mipango yake, unaweza kuhisi au unapitia magonjwa, maumivu na changamoto zingine na uzito kwa kuwa umenyenyekea kwa 'ulimwengu ulioanguka' kwamba umekuwa chini ya dhambi. Ilhali haifai wewe uwe mhadhiriwa wa laana za kizazi na mambo mengine kama hayo. Wakati unapopitia mambo haya, kwa urahisi waweza kumwuliza Mungu aongee na wewe na akuonyeshe jinsi ya kuomba, na ikiwa inahitajika ni hatua gani yapaswa kuchukuliwa wakati umefanyika kama hivi, unaweza kwa uhakika kuwa wazi kumsikia Mungu akinena, naakisha tenda, chochote unapitia kitakuwa cha dhamana.

[21] Nee, Watcham, A Table in the Wilderness. Tyndale Housing Publishers. Wheaton, ILL, 1965 ukurasa kutoka Novemba 6.

Mungu anataka kukupeleka katika njia ya kuzaa mbegu, kutoa matunda. Yeye hatakuacha kama yatima katika majaribu ukimtafuta yeye kwa moyo wako wote.

***2. Ikiwa "hutaenenda" jinsi sisi ni nani, tutapitia kutawaliwa na shetani.***

Katika sura tulizopitia "mwenendo" wetu na Bwana, hatufai kuhisi kana kwamba tumehukumiwa wakati sisi wakamilifu kuelekea kwake. Tunapokuja kwake kwa msamaha, kuwa watoto watiifu, na kumwuliza atusafishe mioyo, tunaweza jihisi tukiwa na pumziko katika utunzi wake.

***3. Shetani hujaribu kuiba Neno la Mungu baada ya kupandwa kama mbegu.***

Hii ni kuvamiwa mbele ndio uweze kupatikana kutosimama na Neno. Ama unaweza litaja kama pigo la wenye kosa kwa ajili ya kuwa mwenye haki. Mungu anataka kujitolea kwa mahitaji yako kupitia kupanda. Neno lake ndani ya Roho zetu na tena kukaa na kuona ikiweza kuzaa matunda yake. Hili ndilo jeshi ambalo shetani hupigana nalo. Shetani aliweza kusadiki Adamu na Hawa yakwamba wanaweza kuendelea na maisha yao bila Neno lake Mungu.(Mwanzo 3) shetani akamjaribu Yesukwa jambo hilo tu katika Luka 4. Na atatatumia,mambo kama haya tu kwetu sisi. Ikiwa shetani anaweza kukufanya uweze kujitegemea bila Neno la Mungu kuhitajikana pahali popote maishani mwako, amefaulu. Shetani anataka wewe uweze kufanya au kutenda kulingana na hisia zako na kufikiri kubaya kuliko Neno la Mungu.kutoamini Neno lake Mungu ni chombo kikuu na cha muhimu kwake shetani. Na hii ndiyo asili ya vita za kiroho ni kuhusu kuamini ukweli tusiouona anakuhisi na akili zetu za kiasili tano. Yesualikuwa anawafunza wanafunzi wake katika Marko 4:9-11 inayosema, "Akasema, Aliye na masikio ya kusikia, na asikie. Naye alipokuwa peke yake, wale watu waliozunguka, na wale thenashara, walimwuliza habari za ile mifano. Akawaambia, ninyi mmejaliwa kuijua siri ya ufalme wa Mungu, bali kwa wale walio nje yote hufanywa kwa mifano"

**Ufalme wote wa Mungu hufanya kazi kama fumbo lililo katika Marko sura ya nane.**

Juzi niliweza kupata barua pepe kutoka kwa mchungaji katika Filipino, aliyekuwa akisoma kitabu chetu

"Kukua au kufa" kwa maneno haya, "sasa naelewa kwamba Mungu ni mkulima na sisi ndilo shamba lake. Sikuwa na wazo hili lakini sasa nimeweza kulipata. Ahsante sana." hili ni rahisi sana tena la mihimu, ni ya undani sana tena waumini wengi hukosa kwa sababu ya urahisi wake. Yesuakayaita mafumbo ya ufalme wa Mungu.(Marko 4:11)

Mungu hupanda mbegu ya Neno lake ndani ya moyo wako (Haijalishi hali ya moyo wako). Hizi mbegu zinawakilisha makusudi yake Mungu ndani ya maisha yako wewe. Umezaliwa mara ya pili hili huwa kusudi lake la kwanza. La pili ni kuwa na ujazo wa Roho Mtakatifu. Kuweza kuponywa mwili, hisia na akili na mahitaji yako kuweza na kukutana naye Mungu. Neno hukulea wewe katika uhusiano mwema katika maisha na kuweza kukutana na kusudi zote za Mungu kwa ajili yake , hata huduma.

Mungu hulitumia Neno lake kuweka kusudi lake ndani ya maisha yako. Matunda ndio jinsi ya kusudi ile tunapaswa tuishi maishani. Petero akasema yale yote tunahitaji kwa kiungu na maisha ili tupewe kwetu, kwa ahadi zake Mungu. 2 Petero 1:3-4. Ahadi zake na mbegu la Neno lake ni jambo tu moja. Adamu kabla ya kutenda dhambi alikuwa aweze kuzaa matunda kwa lile shamba. Baada ya kutenda dhambi Mungu akaweza kumwambia kwamba chochote atahitaji kitakuwa chini ya laana na ataweza kukipata kwa jasho la kipaji chake. Kweli Yesualiweza kuchukua laana, na sasa tunaweza kurudi kawaida na kuweza kuzaa matunda.

Juzijuzi niliweza kushuhudia familia ya huduma yote, ikiwa na mabadiliko makubwa sana, kwa kupata ufunuo kutoka kwa kitabu chetu cha kua au kufa . Waliweza kugundua njia ya mbegu/matunda na waliweza kuwekwa huru kimaajabu. Wakati mwingine walienda kuhubiri kwa ibada, hawakuhubiri, walisimama tu na kuuliza kila mtu aweze kuiba na Yesuakajionyesha. Watu wengi wakaja katika madhabahu ili kuweza kukombolewa, watu ishirini na tano walikuwa

wameanguka na kuwa chini ya nguvu za Mungu.Yesuakajionanisha kwa sababu ya watu wanne walioamua kuwa wa kuzaa matunda.Yohana 15:8 yakatendeka.

***Kuna urahisi wa kitoto wa jinsin ufalme wa Mungu hufanya kazi.***

Tunapomruhusu Mungu aisafishe mioyo yetu, na kuwa na ushirika Mungu. Yeye huongea. Neno lake kwetu sisi, na hiyo inakuwa mbegu ndani ya moyo wako, na ile inalenga kuzaa matunda. Matunda ndiyo tabia zetu, mahitaji yetu na kwa kuhusika kwetu katika kumtukuza yeye na wengine. Yohana 15: 8 inasema, “Hivyo hutukuzwa Baba yangu , kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanfunzi wangu.” Wakati unakuwa wa kuzaa matunda, popote uendapo Yesuataweza kufanyika halisi kwa wengine. Hilo rafiki yangu, ni la nguvu! Haijalishi ambavyo shetani hupigana ngumi kwa kuchanganya watu na dini za aina zote, orodha na mashauri kwa kuweka fumbo ya kuwa ufalme umefichika.

***Tazama katika fumbo la yule mkulima kwamba shetani huja na kuiba neno.***

Hii ndiyo silaha ya pekee ile shetani yuko naye kinyume cha mwanadamu kuweza kuiba Neno ama kutufanya macho kutokana na neno (2 Wakorintho 4:4) inasema, “ambao ndani yao Mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasio amini, isiwazukie nuru ya injili wa utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu.”

Wakati tu neno likisha pandika katika moyo wetu, ni lazima usimame ama ungojee kinyume na hali za kupangwa mpaka ukomae. “kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama.”(Waefeso 6:13)

Kuvamiwa kwa mbele hupatana ikiwa utasimama katika pengo lako, kuweko jimbo umeipata. Unaweza kufanya hivi kwa kuendelea kujibudurisha utambulisho wako katika Kristo, kuendelea kutubu kwa njia zako kupitia maisha, kama unavyoenenda katika Roho na kunena Neno la Mungu kinyume na utu wa shetani ule wa kuvamia.

**Naamini hata Biblia hutufunza kwamba wakati huu wakungoja, Tunahitaji kutumia Neno la Mungu kama silaha.**
Waefeso 6:17b inasema, "upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu."

Huu muda wa kungoja unaweza kuwa ni siku tu,miezi,miaka ama baaada ya miaka kumi . Haijalishi ni miaka mingapi ama ni ni kipindi gani. Wakati huu kuna kusudi nyingi zinaweza kuimarika, si tu ya kuweza kusafisha tabia zetu. Mungu anaweza kutupa sisi ahadi, ama maono, hata hivyo ni lazima tena atutakase ili tuwe vyombo kuweza kubeba maono.

***Wakati tunanena Neno la Mungu, Yesuhulichukua na kulipeleka kwa Baba na kumwuliza yeye aweze kulitenda.***

Tunaambiwa, "Lakini ufahamu neno hili, ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari." Waebrania 3:1 Yesuhuchukua kuungama kwetu kwa Baba kama kuhani mkuu, na Baba huona yote kutimiziwa kulingana na neno la Mungu. Shetani naye huchukua kuungama kwetu kwa kinyume kwetu na kulitenda kulingana na vile umesema. Wakati Neno la Mungu limeweza kunenwa na kuomba juu ya huyo mtu ama hali hii huwa ya nguvu mno. Mungu aliumba vitu vyote kupitia Neno. Yesundiye Neno. Yesuakatupa mamlaka, ili tuweze kulitumia Neno lake kama kwamba ni yeye anayelisema neno hilo.

Yohana 1:1-3 inasema, "Hapo mwanzo kulikuwapo Neno, naye Neno alikuwapo kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika." Yohana 16:23

***Sasa tunaweza kuingia katika pumziko na kuruhusu Neno la Mungu kutenda kazi.***

Waebrania 4:1 inasema, "Basi ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha Yake, na tuogope, mmoja wenu asije akaonekana ameikosa. Waebrania 4:12 inasema, "Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. "

***Malaika huenda kazini wakati wanaposikia Neno la Mungu***

Zabari 103:20 inasema “Mhimidini Bwana enyi malaika zake, Ninyi mliohodari, mtendaye neno lake, Mkiisikilza sauti ya neno lake”.

***Mapepo hutoweka!***

Zaburi 149:5-9 inasema “Watauwa na washangilie utukufu, waimbe kwa sauti kuu vitandani mwao. Sifa kuu za Mungu na ziwe vinywani mwao. Na upanga mkali kuwili mikononi mwao. Ili kufanya kisasi juu ya mataifa. Na adhabu juu ya kabila za watu. Wawafunge wafalme wao kwa minyororo, Nawakuu wao kwa pingu za chuma. Kuwafanyia hukumu iliyoandikwa; Hiyo ndiyo heshima ya watauwa wake wote. Haleluya.”

**Pasaka**

Wakati pasaka iliweza kuamuriwa kwa wana wa Israeli katika Kutoka 12 wana wa Israeli walioambiwa waweke alama ya kondoo asiye na hatia kwa milango yao na malaika wa kifo (Pepo) alikuwa apite na hangewaguza wao. Yesundiye kondoo wake Mungu, na tunaweza weka damu yake juu ya milango na juu ya wapendwa wetu na wale wote sisi huombea. Aje?

Ufunuo wa Yohana 12:11inasema, “Ndugu zetu wameshinda kwa damu ya Mwanakondoo na kwa nguvu ya ukweli walioutangaza; maana hawakuyathamini maisha yao kuwa kitu sana, wakawa tayari kufa.”

Maneno ya midomo yetu yanaweza kuachilia damu. Tazama kutoka 12 ya kwamba mradi tu damu, na kuachiliwa kwa milango yao, tena Mungu na shetani wanaweza kuiona. Hisopa ilikuwa mmea wa kawaida, na haikuonekana kuwa na umaana mwingi. Maneno ya midomo yetu haionekani kuwa ya maana sana, lakini wakati tunatumbukiza maneno yetu ndani ya Neno lake Mungu (Naye ndiye Yesumwenyewe) na uyapake kama damu. Mungu huona na hata shetani huona.

**Kuwa mwangalifu kwa yale wewe husema!**

Marko 11:21-24, “Petero akakumbuka habari yake, akamwambia, Rabi, tazama,mtini uliolaani umenyauka. Yesuakajibu akamwambia,

mwaminini Mungu. Amin, nawaambia, yeyote atakayeuambia mlima huu ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake. Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote ambaye myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu."

***Thibitisho la Mungu la Msingi wa Imani***

*TGIF Today God is first by Os Hillman*[22]

*Waamuzi 3:2, "ili kwamba vizazi vya wana wa Israeli wapate kujua ili kuwafundisha vita, hasa wao ambao hawakujua vita kabla ya wakati ule. "*

*Mungu aliweza kuleta nchi ya wana wa Israeli katika nchi ya Ahadi ya Canaan kupitia Yoshua. Baada ya Yoshua aliweza kupigana. Kupigana na kujaribiwa kwa watu wake Mungu ni njia yake Mungu ya muhimu sana inayowezeshawatoto wake kufaulu katika vita vya kiroho. Hii ndiyo sababu hatuwezi tukaishi maisha bila majaribu. Haya hutumwa kwa ajili ya imani yetu iweze kuonekana kama ni halisi au ni maneno rahisi na matupu. Waamuzi 3:4, "Naye aliwaacha ili awajaribu Israeli kwa hao, apate kujua kwamba watasikiliza amri za BWANA, alizowaamuru baba zao, kwa mkono wa Musa."*

*Mungu huruhusu hali kama hizi ili kuweza kudhibitishwa. Ni wakati tu , tunajaribu kwa vita tunaweza kuwa mashujaa walio na ustadi. Unaweza kuwa na ujasiri kwamba Mungu ataruhusu majaribu yaweze kuja kupitia hali kama mkubwa wako asiye na akili,mchuuzi anayekataa, maneno ya uongo kuhusu tabia zako ama uhusiano mgumu ule unahitaji upendo mkubwa. Vita hutumwa kwako wewe ili uweze kujaribu ni nini unajua kwa akili zako, ndiyo yaweze kuwa sehemu ya moyo wako. Utaweza kugundua , ukisha pita hii mitihani ama unahitaji vita vile vitakuletea wewe nafasi ya kujua jinsi ya vita*

---

[22] Imetolewa kwa idhini kutoka kitabu TGIF Today God Is First, na Os Hillman. Hali miliki 2003. Imechapishwa kwa idhini. Ili kuopea barua pepe bila malipo kila siku tembelea tovuti ya TGIF: www.TodayGodIsFirst.com au www.MarketplaceLeadrrs.org.

*vya kiroho. Usiwe na hofu kwa ajili ya vita vilivyo mbele zako. Mungu ameshakwisha kukupa ushindi ukisha kumtegemea na kumtii yeye pekee. Sasa utakuwa shujaa wake Mungu, aliye na ustadi katika vita vya kiroho.*

Unaweza kulipata neno la maombi katika tovuti hii http:/www.isob-bible.org/abf/prayerbook.htm

# Sura ya 16.
# Jiwe Lako Limeondolewa

Katika kitabu hiki chote,tumekuwa tukielekeza macho yetu kwa uponyo wa ndani, kutokana na majeraha vya kale. Hivi majeraha vya kujeruhiwa vibaya kukataliwa, hatia, hofu, umaskini wa kujidharau, kutojisamehe, yote huwa vizuizi katika maisha ya utele wa Mungu ambaye angetutakia . Sisi twaweze kuishi kwa hili somo tutaita hivi vizuizi "mawe". Mawe yako yamekuwa majeraha vile vinavyokuweka katika hali ya kifo.

Tunajua ile njia Yesualiweza kuipitia katika maisha yake mapya. Kwanza aliweza kusulubiwa, tena akazikwa na wakaweza kulifunika shimo lake kwa jiwe. Serikali ya Kirumi ilihakikisha jiwe kubwa sana litalizuia kaburi lake, ili pasipatikane yeyote atakaye uchukua huo mwili na kuweza kutangaza ufufuo wake. Kama tunavyojua jiwe kuu , haliwezi kulinganishwa na nguvu zake Mungu za ufufuo. Hali za kidunia, hata hizo huweka mawe mazito kwa kaburi zetu ili kutuweka katika kifungu.

Ikiwa umesikia na kuutenda ukweli tuliopatiana katika kitabu hiki, wewe ni mtihaniwa wa nguvu zake Mungu za ufufuo, kutoa ama kuondoa jiwe lako na kukuleta kwa mpango wa ufanisi wake Mungu maishani mwako.

**Matokeo ya kufanikiwa**

3 Yohana 1:2-4 inasema, " Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo. Maana nalifurahi mno walipokuja ndugu na kuishuhudia kweli yako, kama uendavyo katika kweli. Sina furaha iliyo kuu kuliko hii, kusikia ya kwamba watoto wangu wanakwenda katika kweli."

***Yohana aliweza kuunganisha ufanisi katika mambo matatu.***

1. Ukweli wa wanafunzi wake
2. Kwamba wanafunzi wake walienenda, ama kuishi maisha yao kwa ukweli
3. Yohana aliweza kulinganisha nguvu zao za ufanisi na ufanisi wa miyo yao. Alisema "kama vile" ikiwa nafsi yako inapopata

ufanisi kwa hivyo hata wewe maisha yako yanaweza kupata ufanisi kuwa na safari ya kufana, kupewa ufanisi.

Zaburi 35:27 inasema, "Washangilie na kufurahi, wapendezwao na haki yangu. Naam, waseme daima, Atukuzwe BWANA, Apendezwaye na amani ya mtumishi wake."

Neno ufanisi kwa Kihibrania humaanisha:

Amani, wema, hali njema, salama, ufanisi, kutokuwa na hatia, uzima, ukamilifu, kutoshereka kwako na Mungu.

**Mungu anaweza kukuaminia ufanisi wake wakati nafsi yako imeweza kuponywa.**

Wakati hiari yako, akili na hisia zinakuja kufanana na mfano wake Mungu, Mungu anaweza kukuamini na ufanisi wake kwa nini? Kwa sababu anajua kwamba una uwezo na una nguvu za kutosha kuweza kupata ufanisi wake, hata kama ufanisi umekupata wewe. Ufanisi kutokana na hali ya dunia kwa urahisi unaweza kukuweka mbali na uhusiano wa karibu naye Mungu.

***Ufanisi wa kiungu ni gani?***

Maelezo ya Mungu kuhusu ufanisi ni tofauti kutokana na maelelzo ya kidunia. Mungu ana njia za kusisimua za kuweka siri zingine kwake mwenyewe. Yote yale naweza kusema ukisha peana maisha yako yote kabisa kwake Yesukama Mungu, bila kupigwa na chochote na kuishi hayo maisha kwa kutii vizuri. Kile unachoweza, ataleta, uwezo wake wa ufanisi kwako kwamba umekuwa wakutoelewa vibaya sana, na waKristo wengi sana.

Waefeso 3:20 inasema, "Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu." Naamini kuwa ufanisi na sehemu ya kiasili ya kupita kiasi kwa pande mbili tofauti. Wengine husema kwamba Mungu anataka tuwe na uzima, utajiri na tusipitie mateso. Wakati nilikutana na Mungu mnamo 1979 niliamini hilo. Waliweza kuelezea Mungu kwa ufanisi wake na maelezo ya kidunia kuhusu ufanisi. Wengine husema Mungu anataka kutuweka tukiwa tumenyenyekea kwa kuwa maskini. Hizi zote ni kupita kiasi na si kweli. Mungu hutamani ufanisi wa ufalme wake Mungu kwetu sisi.

Ufanisi wa kifalme ni tofauti kabisa na mara nyingine maelezo yake hupotelea kwa sababu za wanadamu. Naamini kwamba ufukara haufai kuwa mwisho wetu, lakini iwe kingilio chetu. Katika ufanisi, aina ya mlango kupitia tunapoingia ufanisi bila kifo na ufufuo unaweza kumtoa mtu kutoka kwa Mungu.

***Mambo mengine ya ufanisi wa kiungu.***

***Tunda la roho.***

Naamini ya kwamba ufanisi wa kifalme ni wa kwanza ni kudhihirisha matunda ya kiroho. Wagalatia 5:23 inasema, "upole, kiasi, juu ya mambo kama hayo hakuna sheria."

***Utoaji wa ufanisi wa kiungu***

Tena naamini kwamba inahusu, kutwaliwa kwake kwa maisha yako ya hapa duniani, hata kutokuwa na upungufu wa fedha, chaguo lake la Mungu na shughuli za maisha yako, afya, uhusiano na mengine yana shughulika na maisha yako hapa duniani. Naamini tena inahusu zaidi yetu kuishi tu ili kuendelea kuwa watu wa kupeana. Inastahili tuwape maskini huduma na makanisa yale yanaeneza maagano yake Mungu.

Kumbukumbu la Torati 8:18 inasema, "Bali atamkumbuka BWANA Mungu wako, maana ndiye akupaye nguvu za kupata utajiri; ili alifanye imara agano lake alilowapa baba yako kama hivi leo."

Nataka kufanya hili kuwa wazi, kwamba ninapotaja fedha na kupewa, hakuna kiwango kimewezwa kuwekwa. Ufanisi wa kifedha kwa watu wa nchi fulani unaweza kuwa labda shamba ndogo na mbonga za kula na pengine wauze zingine, na zingine kutumia kuwapa maskini. Hu ndio ufanisi kwa wengi. Kwa wengine unamanisha kuwa na uwezo wa kanisa nzuri na huduma iliyo na nguvu. Pale mchungaji na familia yake wanashughulikiwa vyema. Kwa wengine, Mungu angetaka kuwapa pesa nyingi ili wawe na miradi mikubwa ya ufalme wake Mungu. Hatufai kujilinganisha na wengine.

Wala tuwe tumeshushwa mioyo ikiwa bado hatujaweza kuupata ufanisi wa kifedha. Jambo kuu la kuangazia katika ufanisi wa nafsi yako, kama vile Yohana wa tatu alisema, kuruhusu ukweli kuwa ndani yako, na tena kutembea kwa kweli. Ruhusu Mungu aiponye

hiari yako, mawazo yako na hisia zako kama vile tumekuwa tukijadilia katika nakala hii. Mpatie wakati. Usiwe mtu ambaye hawezi kuvumilia. Usilenge macho yako katika ufanisi wapese lakini tazamia uhusiano wako na yeye, na mienendo yako na yeye, kumbuka ninaamini ya kwamnba ufanisi wake Mungu unakuja kupitia mlango wa "umaskini". Wakati ninasema umaskini ninamaanisha kwa wale wenu si wa nchi za Magharibi wale wanaopitia hali ngumu kwa sababu ya kuzorota kwa uchumi ama hali ya kisiasa, niko na mawaidha kwenu. Usiangalie ama usitazame waKristo wa magharibi kwa sababu wametoka nchi zizofanikiwa ili waweze kukusaidia wewe. Hiyo ni kuabudu miungu. Kumtazamia Mungu kwa ufanisi wako, atakutwalia mahitaji yako yote.

***Kumtukuza Mungu***

Mwishowe, naamini ya kuwa ufanisi unahusu pia kuweza kutumiwa naye Mugnu kueneza ufalme wake katiak eneo letu la utawala. Kutukuza inamaanisha kutambua siri hii inaweza kuwa kama mama anaye lea watoto, ama shughuli mpaka kanisa na kazi ya kueneza injili.

**Ufanisi haumaanishi kutokuwa na mateso ama majaribu ama changamoto**

Kuna aina nyingi tofauti za ufanisi. Mungu yuko nazo kwa watu tofauti. Waamini katika kanisa la mateso ni lazima waishi na maelezo tofauti ya ufanisi. Nimeweza kutembelea waaminio wa Uchina wale wasemao kuwa wano ufanisi katika mafungo ya magerezani kwa chakula kidogo, kwa sababu wanaweza kuona ufalme wa Mungu ukienea kupitia mateso yao. Kanisa lake Mungu huenea na kupanuka, katiak nchi nyingizipitiazo mateso.watu wanaongezeka kwa njia kuu sana. Waaminio wale wameamini kwa kuponywa kwa kiasili na hawajapataama haijadhihirika bado, wanafaa waendelee kumtafuta Mungu na kwa wakati uo huo wasihisi ya kwamba wamehukumiwa ama ni duni kwa sababu hawajaona uponyo wao. Mungu hushughulika na wandamu

**Kuondolewa kwa jiwe kunalinganishwa na ufufuo.**
Mungu ameweza kufanya shughuli na wewe pale msalabani. Hufai kuteseka kwa ghadhabu ya dhambi. Ilhali alijitambulisha kwako na akakuhusisha kwa ufufuo. Wakati jiwe lako limeondolewa, unahusika kwa matunda ya ufufuo naye Mungu. Tazama mifano hi ambayo imeandikwa katiak Isay kuwaonyesha jinsi ufanisi ni matunda kutoka ufukara.

*Isaya 35:1-10*
*1 Ee BWANA, utete nao wanaoteta nami, Upigane nao wanaopigana nami.*
*2 Uishike ngao na kigao, Usimame unisaidie.*
*3 Uutoe na mkuki uwapinge wanaonifuatia, Uiambie nafsi yangu, Mimi ni wokovu wako.*
*4 Waaibishwe wafedheheshwe. Wanaoitafuta nafsi yangu.Warudishwe nyuma wafadhaishwe nyuma, wafadhaishwe, Wanaonizuilia mabaya.*
*5 Wawe kama makapi mbele ya upepo,Malaika wa BWANA akiwaangusha chini.*
*6 Njia yao na iwe giza na utelezi, Malaika wa BWANA akiwafuatia.*
*7 Maana bila sababu wamenifichia wavu, Bila sababu wameichimbia shimo nafsi yangu.*
*8 Uharibifu na umpate kwa ghafula, Na wavu alioufiche umnase yeye mwenyewe;kwa uharibifu aanguke ndani yake.*
*9 Na nafsi yangu itamfurahia BWANA, Na kuushangilia wokovu wake.*
*10 Mifupa yangu yote itasema, BWANA, ni nani aliye kama Wewe? Umponyaye maskini na mtu aliye hodari kumshinda yeye, Naam, maskini na mhitaji na mtu amtekaye.*

Isaya 61 ilikuwa utabiri wa huduma ya Yesu. Imeanza na shughuli kwa maskini na waliofanyika, kufunguliwa kutoka gerezani na kuachilia waliotekwa nyara. Inaendelea kuongea kuhusu ufanisi wa

fedha na mwishowe kuhusu kukombolewa kwa watu wa Mungu kumtumikia yeye kama kuhani ama mhudumu wa Agano Jipya.

Isaya 61:1-11,

*(1) Roho ya BWANA MUNGU i juu yangu; kwa sababu BWANA amenitia mafuta niwahubiti wanyenyekevuhabari njema; amenituma ili kuwanganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao,na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao.*

*(2) Kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa na siku ya kisasi cha Mungu wetu; kuwafariji wote waliao.*

*(3) Kuwaagizia hao waliao katika Sayuni, wapewe taji ya maua badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito; wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na BWANA, ili atukuzwe.*

*(4) Nao watajenga mahali pa kale palipoharibiwa, watapainua mahali palipokuwa ukiwa zamani, watatengeneza miji iliyoharibiwa, mahali palipoachwa kizazi baada ya kizazi.*

*(5) Na wageni watasimama na kulisha makundi yenu, na watu wa kabila nyingine watakuwa wakulima wenu, na watunzaji wa mizabibu yenu.*

*(7) Bali ninyi mtaitwa makuhani wa BWANA; watu watawaiteni wahudumu wa Mungu wwetu; mtakula utajiri wa mataifa, na kujisifia utukufu wao.*

*(13) Badala ya aibu yenu mtapata maradufu, na badala ya fedheha wataifurahia sehemu yao; basi katika nchi yao watamiliki maradufu; furaha yao itakuwa ya milele.*

*(8) Maana mimi, BWANA, naipenda hukumu ya haki, nauchukia wivi na uovu; naminitawalipa malipo katika kweli,nitaagana nao agano la milele.*

*(9) Na kizazi chao kitajulikana katika mataifa, na uzao wao katika kabila za watu; wote wawaonao watakiri ya kuwa wao ni kizazi kilichobarikiwa na BWANA.*

*(10) Nitafurahi sana katika BWANA, nafsi yangu itashangilia katika Mungu wangu; maana itoavyo amenivika mavazi ya wokovu, amenifunika vazi la haki, kama bwana arusi ajipambavyo kwa*

*kilemba cha maua, na kama bibi arusi ajipambavyo kwa vyombo vya dhahabu.*

*(11) Maana kama nchi itoavyo machipuko yake, na kama bustani ioteshavyo vitu vilivyopandwa ndani yake; ndivyo BWANA MUNGU atakavyootesha haki na sifa mbele ya mataifa yote.*

**Furaha ya asubuhi hunena juu ya ufufuo**

Zaburi 30:5 inasema, "Maana ghadhabu zake ni za kitambo kidogo, katika radhi yake mna uhai; Huenda kilio huja kukaa usiku, lakini asubuhi huwa furaha."

Ufanisi wa kiungu, kwa maono yangu, ndio humtukuza Yesu, amam yey humfanya ajulikane.

Yohana 15:8 inasema, "Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu." Yohana 12:24 inasema, "Amin, amin, nawaambia, chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali iyo hiyo peke yake; bali ikifa, hutoa mazao mengi."

**Naamini ya kwamba ikiwa tunaweza kupitia njia iliyowekwa na wa mtume Paulo katiak Wafilipi 3, kwamba tutakuwa kwa njia za Mungu kuelekea ufanisi ule anataka kwetu sisi.**

Ikiwa kuna kusudi langu lenye dhabiti ni kwamba yey ndio niweze kuendelea na kuwa wa ndani sana na wakaribu kumjua na yeye kujua na kutambua na kuelewa maajabu ya utu wake kwa nguvu sana na kwa wazi zaidi na ndio kwa hiyo njia sawa niweze kujua nguvu zinazoteremka kutoka kwa ufufuo wake na ndio hutumika kwa waaminio, na kwamba naweza gawanya naye mateso yake, kama tunaweza kuendelea kubadilishwa katika roho ndaniya usawa wake , na kifo chake katika tumaini. Kwamba ikiwa inawezekana niweze kupata kiroho na uadilifu. Ufufuo unao niinua kutoka kwa wafu hata wakati niko kwa huu mwili.

Si kwamba nimefika (huu ukamilifu) ama nimesha kuwa tayari kufanywa mkanilifu lakini na shindilia mbele kuweza kushika ama fahamu na kuifanya iwe yangu, kwamba ile Kristo Yesu (Masihi) ameshaipata kwangu mimi na kuyafanya yawe yangu(Wafilipi 3:10-12)

***Dondoo kutoka kwa Dr. Kirk Walters- Administrative Mchungaji Mount Paran North Church of God***

*Anataka tuweze kumalizia safari vizuri.*

*Wakati mwingi tunaangalia kwa mambo madog, maelezo duni kwa kujipima kwetu na ufanisi, hiyo ndiyo iliyobaki kwa benki zetu ama nguvu za kuweka bishara kubwa. Mungu huangalia picha kubwa ya ufanisi kidokeze kikubwa chetu cha kuonyesha kufaulu kwetu maishani ni hali ya nafsi yetu. Yohana akasema yeye huomba ili tuweze kufanikiwa kwa mambo yote hata uzima wa mwili, lakini anafunga maombi haya yote kwa kiwango cha ufanisi wa kiroho.*

*Kazi yetu nikuishi na kwaamini kwa njia hii kwamba mwishowe wa safari tutaimba "Ni vyema na nafsi yangu" kazi yake Mungu, ikiwa tumeishi na kuaminika vizuri ni kututazama na hukumu kamilifu na kutangaza vyema san mzuri na mtumishi aliye mwaminifu. Ingia katika furaha yake Bwana. Huu ndio ufanisi wa kweli.*

---

[i] **Maneno ya Mwisho**

[1] The spiritual Man, Watchman Nee mwandishi.

[2]Katiaka kumbukumbu nyingi zinazofanywa kwa Dunklin Memorial Church. Tumeweza kuweka Dondoo kutoak kitabu cha uponyo wa ndani.twawashukuru kwa hiyo huduma ya ajabu iko Florida kwamba wameweza kuleta ama wamechangia mambo ya dhaman au kwa mwili wake Kristo. Wengi wa viongozi wao na waandishi wamesahkombolewa kutokana na tabia mbaya zilizopita kiasi na sasa wanmtumikia YesuKristo.

Haki ya Kumili © 1992 na Dunklin Memorial Church- kimetumiwa na idhini ya ISOB.

**Kiambatisho A**
**Uhalisi wangu kamili**

Ni na amini

Ya kwamab katika KristoYesu dhambi zangu zote zilizopita, ziko, na zile zitaja zimeweza kusamehewa kabisa hakuna chochote ningeweza kufanya ndio niweze kukipokea kipawa cha bure kwa imani na hakuna chochote ningeweza kufanya ndio ni poteze hii. Upendo wake wa kiajabu usio na kifani kabisa.

Katika Kristo nimeshapewa jiana jipya la uatmbulisho. Sasa mimi siko ndani ya Adamu. Mimi ni kiumbe kipya! Yesuyey hukaa katika mkono wa Mungu wa kulia akiendelea kutufanya sisi maombi. Yeye haoni ama hajaaibika, na hata wakati nimeanguka ananikumbusha kwa upendo mimi hasa ninani. Shetani kamwe hana nguvu juu yangu kwa sababu yeyye alishindwa miaka mingi hapo awali pale msalabani.

Wakati shetani alijaribu kuleta mambo yangu ya kale ili anishushe moyo kwa haraka nitamkumbusha hatima ama siku zangu za baadaye. Mkuu ni YesuMungu aliye ndani yangu kuliko sheria ama mipango haina muda katika huu ulimwengu uliopungukiwa. Ndani ya Kristo mimi si mfungwa wa hisia zangu. Ukweli kunihusu ni jinsi Mungu anasema, ‘haijalishi ama hakunaa cha kunishtua’, kwa masikitiko yangu kutoka sasa nimeweza kuwa na mawazo yake Kristo, sasa mimi sio mfungwa wa uongo wake shetani. Roho Mtakatifu yeye hutufunulia ujanja wake. Chochote na kila mawazo yale yameletwa kwangu ni lazima yapite kupitia ukweli/ uongo “chujio” ikiwa

wazo si safi, takatifu na utukufu kwa Baba, hii ikowazi imetokana na adui katika jina la Yesu nitalitupilia Mbali hilo wazo si la Mungu, na nilazima atoroke.

Katika Kristo Yesu nimeweza kuinuka na kutembea katika uhai mpya, uhai tele, uzima wa milele, maisha yake/ uhai wake. Kwa kweli tayari mimi nimeshafanywa raia wa mbinguni furaha kiasi gani imejaa nafsini mwangu. Kwa ajili babangu yuko kila wakati na mimi na katika upande wangu, nani awezayekujaribu kuja kinyume nami? Mimi ni zaidi ya mshindi. Ushindi tayari ni wangu katika Kristo kuna tumaini la milele. Uongo na hofu sio marafiki wangu kuendelea, kwa ajili ni mamboya uongo kutoka kwake shetani, na haikubaliani na ukweli a,ma uhalisi wangu. Sasa mimi ni na uhai kwa ukweli na kufa kwa dhambi. Yesuni yote juu ya maisha yangu. Yeye ni kila kitu maishani mwangu. Sitaabudu chochote au yeyote. Hakuna mwingine juu yake, yeye ni chochote ninachohitaji. Yeye ni njia, ukweli, na uhai wangu. Yeye anatosha.

- Jina la mwaandishi huyu halijulikani

**Ombi langu la mwisho kwako.**

Waefeso 3:16-21 inasema, "Namwomba Mungu, kadiri ya utajiri wa utukufu wake, awajalieni kwa uwezo wa Roho wake, nguvu ya kuwa imara ndani yenu, naye Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani. Namwomba mpate kuwa na mzizi na msingi katika mapendo kusudi muweze kufahamu pamoja na watu wote wa Mungu jinsi upendo wa Kristo ueneavyo kwa mapana na marefu, kwa kimo na kina. Naam, mpate kujua upendo wa Kristo upitao elimu yote, mjazwe kabisa utimilifu wote wa Mungu. Kwake yeye ambaye kwa nguvu yake ifanyayo kazi ndani yetu, aweza kufanya mambo makuu zaidi ya yale tuwezayo kuomba au kufikiria; kwake Mungu uwe utukufu katika kanisa na katika Kristo Yesu, nyakati zote, milele na milele! Amina."